# USAWIRI WA UOVU KATIKA RIWAYA TEULE ZA BEN R. MTOBWA

**TASNIFU YA**

**ANYANGO A. PAMELA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asili na haijatolewa kwa madhumuni ya kutuzwa shahada yoyote katika chuo chochote

………………………………. …………………………

**ANYANGO A. PAMELA** **TAREHE**

**C50/25231/2011**

Tasnifu hii imewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi

…………………………………. ……………………….

**DKT. RICHARD WAFULA** **TAREHE**

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

…………………………………….. …………………………..

**PROF. CATHERINE NDUNGO** **TAREHE**

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mama yangu mpendwa Agnes Apondi Anyango kwa kunipa moyo wa kuendelea na masomo yangu hadi upeoni. Mume wangu Job Omondi Ogolah, Wanangu Glenn Ogolah Omondi, Neville Hawala Omondi na mpwa wangu mpendwa Castro Romeo Ramoto kwa uvumilivu wenu na kunitumainisha. Mungu awabariki kwa kuwa na moyo wa uvumilivu na uelewa**.**

## SHUKRANI

Kwanza ninachukua nafasi hii kumshukuru Rabuka kwa kunijalia baraka, afya njema na azma ya kutimiza malengo yangu. Hakuna jambo lolote ambalo lingetimia bila yeye kunileta umbali huu, kwa kunipa hekima, moyo wenye uvumilivu na matumaini tele.

Pili ninawashukuru sana wasimamizi wangu Dkt. Richard Wafula na Prof. Catherine Ndungo. Msaada mlionipa, fikra, maarifa na mwongozo wa kila namna ulinifaa sana kufikia kiwango hiki. Pia siwezi kusahau mwongozo na ushawishi niliopewa na wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili hasa wale wa fasihi kama vile: Dkt. Masinde, Dkt. Ngugi, Dkt. Maitaria, Bi. Mudhune, Dkt. Chacha, Dkt.Gakuo, Dkt. Osore, Dkt. Mwihaki, Prof. King'ei na wengine wote. Mungu awape maisha marefu.

Ninachukua nafasi hii tena kumshukuru mume wangu Job Mark Omondi Ogolah kwa kunihimiza kuendelea na masomo, kunitia moyo na kuniunga mkono katika harakati ya kufuata ndoto yangu hadi mwisho. Siwezi kuwasahau babangu marehemu Alfred Anyango Omondi aliyenitandikia zulia la elimu na kunitegea kitendawili cha elimu ambacho nimeng'ang'ana kukitegua tangu utotoni.

Aidha ninawashukuru ndugu zangu wapendwa: Jennipher Akinyi Anyango, Francis Apanga Anyango, Gorrety Anyango na David Walter Anyango. Siwezi kumsahau marehemu Petronila Anyango na Margret Adhiambo Anyango au Peggy. Peggy aligundua siri ya talanta zangu na kunifumbulia fumbo la elimu. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Mawaidha na mwongozo wako ulinifaa sana katika nyanja ya elimu.

Isitoshe, ningependa kuwapongeza wanafunzi wenzangu ambao tuliogelea nao katika bahari ya masomo kwa ushirikiano wao. Mlinipa moyo wakati mlima ulipoendelea kuwa mgumu kukwea. Wanafunzi hawa ni pamoja na Lena, Elizabeth Mue, Dorothy,

Hassan, Haule, Syllvan, Githaka, Chari, Omtimba, Sululu, Kellen, Alice, Sudi, Gladys,Teresia na wengine ambao sijawataja.

Mwisho, ninawashukuru rafiki zangu walionifaa kwa njia mbalimbali katika safari hii. Hawa ni pamoja na Edmund Ogalo, Violet Isiche, Noel Kutwa, Jacinta Ogutu, Helda Riagi, Ann Hawala, Josephine Adhiambo, Sabina Ogutu, Dkt Sabenzia Wekesa, Peri, Nancy Wekesa na Jenipher Anyango Jeff. Mchango wao katika juhudi zangu za kukamilisha kazi hii haukadiriki, Mungu awabariki.

## IKISIRI

Utafiti huu umelenga kuelezea uovu katika jamii kama unavyosawiriwa na Ben R. Mtobwa. Maswala yanayotendeka ni nyeti na ibuka katika jamii ya sasa. Riwaya ambazo zimeshughulikiwa ni *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984) *na Tutarudi na Roho Zetu* (1987). Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha aina ya maovu, kueleza kiini cha uovu huo, kuonyesha athari ya uovu huu na kuangalia mbinu za upelelezi zinazotumiwa na mwandishi kukabiliana na uhalifu. Mwandishi huyu anatumia fasihi kuyasawiri maovu yanayotokea katika jamii. Mwandishi huyu anatumia fasihi kuyasawiri maovu yanayotokea katika jamii. Aidha, anaonyesha namna wahusika katika riwaya hizi wamesukumwa na jamii zao kuwa waovu. Utafiti huu umeongozwa na mihimili ya nadharia mbili kutimiza malengo yake. Nadharia ya Maadili na ile ya Uhalisia. Nadharia ya Maadili iliasisiwa na wanafalsafa Plato (c443) na Jean Jacques Rousseau (1712-1778). Waitifaki wa nadharia hii ni Tolstoy (1960), Hough (1966), Palmer (1992), na wengine. Nadharia hii ya Maadili imekusudiwa kushughulikia mtazamo wa mwandishi kuhusu uovu. Nadharia ya Uhalisia iliasisiwa na Hegel. Waitifaki wa nadharia hii ni Georg Lukacs (1972) na wengine. Nadharia hii imeshughulikia mambo ya kihalisia katika jamii. Mihimili ya nadharia hizi imeuongoza uhakiki wa riwaya zilizoteuliwa ili kupata data inayotosheleza utafiti huu. Data hiyo imerekodiwa na kuchanganuliwa kulingana na maswali ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia. Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo katika sura tano. Sura ya kwanza imeshughulikia mada ya utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, sababu za kuchagua mada, misingi ya nadharia, mbinu za utafiti na uchanganuzi wa data. Sura ya pili imejadili historia ya mwandishi na kuandika machache kuhusu dhana ya uovu. Sura ya tatu imejadili kiini, athari na mbinu za upelelezi zinazotumika kumaliza uovu katika *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984). Sura ya nne imejadili kiini, athari ya uovu huo kwa wanajamii na mbinu za upelelezi zilizotumika kuzuia uovu katika T*utarudi na Roho Zetu* (1987). Sura ya tano imejumuisha muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti na mapendekezo. Utafiti huu unanuiwa kuwa wenye manufaa kwa wahakiki wa fasihi, wakuza mitaala, wapenzi wa lugha ya Kiswahili na jamii kwa jumla.

## ABSTRACT


### Portrayal of evil in Ben R. Mtobwa's novels

This research seeks to depict evil in the society as potrayed by Ben R. Mtobwa in his novels namely: *Salamu Kutoka Kuzimu (1984)* and *Tutarudi na Roho Zetu (1987)*. The books exploit a particular kind of evil found in the society. This study set out to classify the types of evil, discuss causes of such evil, effects of evil and possible detective methods highlighted by Ben R. Mtobwa in his novels. The writer uses literature to highlight types of evil experienced in the society. In these novels, the writer tries to bring out the fact that this evil characters are people who have been pushed by the same society to become what they are. The tenets of two theories, the Moral theory and Realism theory guided this research to achieve its objectives. Moral theory is mostly associated with Plato (c443) and Jean Jacques Rousseau. According to Jean Jacques Rousseau (1712-1778), human beings are corrupted by the very society in which they live. The theory was later amplified by Tolstoy (1960), Hough (1966), Palmer (1992) and others. This theory has helped in explaining the authors perception in regard to evil. Realism theory was put forward by Georg Hegel with Georg Lukacs (1972) and others being its proponents. This theory deals with real societal issues. This research was conducted in the library where browsing of the internet, reading of books, journals and a variety of theses related to the topic of research was done to give this research a basis. The data for the study was extracted from the selected texts and purposively sampled. The data collected was analysed and the finding presented through explanations, discussion alongside examples and a summary given thereafter. The report of the study is presented in five chapters. First chapter includes research topic, objectives of the study, research question, justification of the study, scope of the study, literature review and theoretical frame work. In the second chapter discussed the history of the writer and the concept of evil. In chapter three causes, effects and possible methods used by the detective to combat evil in *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984) has been discussed. In chapter four, the study has discussed causes, effects and possible ways used to combat evil in *Tutarudi na Roho Zetu* (1987). Chapter five looked at the summery of the research, reseach findings, and recommendations for further studies. This research will benefit literary critics, researchers, scholars, Kiswahili lovers and the society as a whole.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| Fasihi pendwa - | Dhana hii hutumiwa kuielezea fasihi ambayo hudhamiriwa kuburudisha. Sifa kuu ya fasihi ya aina hii ni kuwa inapendwa na watu wengi. |
| Maadili - | Wema au mambo ya haki. |
| Mazingira - | Dhana inayotumiwa kuelezea muktadha wa kimaumbile wa tukio, hadithi au tendo katika fasihi. |
| Riwaya dhati - | Riwaya dhati ni riwaya ambayo inajishughulisha moja kwa moja na maswala ya kila siku na jamii ya Kiswahili; Maswala yanayotambuliwa kuwa halali kushughulikiwa na fasihi ya Kiswahili. |
| Riwaya pendwa - | Ni hadithi inayohusika na upelelezi wa vituko na kadhia za kijambazi zinazotokea katika sehemu mbalimbali na mara nyingi huambatana na mapenzi ya kilimbwende. |
| Uovu - | Matendo mabaya yanayowatia binadamu wengine uchungu au huzuni. |

## YALIYOMO


**UNGAMO ...... ii**

**TABARUKU ...... iii**

**SHUKRANI ...... iv**

**IKISIRI ...... vi**

**ABSTRACT ...... vii**

**UFAFANUZI WA ISTILAHI ...... viii**

**SURA YA KWANZA ...... 1**

**1.0 Utangulizi ...... 1**

1.1 Usuli wa utafiti ...... **1**

1.2 Suala la Utafiti ...... **5**

1.3 Maswali ya utafiti ...... **6**

1.4 Malengo ya utafiti ...... **6**

1.5 Sababu za kuchagua Mada ya Utafiti ...... **6**

1.6 Upeo na Mipaka ...... **9**

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada ...... **10**

1.8 Misingi ya Nadharia ...... **25**

1.8.1 Nadharia ya Maadili ...... **25**

1.8.2 Nadharia ya Uhalisia ...... **29**

1.9 Mbinu za Utafiti ...... **33**

1.9.0 Utangulizi ...... **33**

1.9.1 Muundo wa Utafiti ...... **33**

1.9.2 Mahali pa Utafiti ...... **33**

1.9.3 Uteuzi wa Sampuli ...... **34**

1.9.4 Ukusanyaji wa Data ...... **34**

1.9.5 Uchanganuzi wa Data ................................................................................ **34**

1.9.6 Uwasilishaji wa matokeo ........................................................................ **35**

**SURA YA PILI** .......................................................................................... **36**

**HISTORIA YA MWANDISHI, DHANA YA UOVU NA AINA ZA UOVU** ....... **36**

2.0 Utangulizi .................................................................................................. **36**

2.1 Historia na maisha ya Ben R. Mtobwa ................................................... **37**

2.1.1 Tajriba na Sifa zake ............................................................................... **38**

2.2 Dhana ya Uovu ......................................................................................... **42**

2.2.0 Utangulizi ................................................................................................ **42**

2.2.1 Maana ya Uovu kulingana na wataalamu mbalimbali ........................ **43**

2.2.2 Wema na Uovu ......................................................................................... **45**

2.2.3 Maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu uovu .................................... **47**

2.2.4 Aina za uovu ............................................................................................ **51**

2.2.4.1 Mauaji ya kikatili kama aina ya uovu. ............................................... **53**

2.3 Mawazo ya Ben Mtobwa katika riwaya zake ........................................... **54**

**SURA YA TATU** ......................................................................................... **58**

**MAUAJI, ATHARI ZAKE NA MIKAKATI YA KUSHINDA UOVU KATIKA RIWAYA YA *SALAMU KUTOKA KUZIMU*** .......................................................... **58**

3.0 Utangulizi .................................................................................................. **58**

3.1.0 Kiini cha uovu katika Riwaya ................................................................ **63**

3.1.1 Mazingira kama kiini kikuu cha uovu ................................................... **63**

3.2.1 Mauaji katika misingi ya kisiasa ............................................................ **68**

3.2.2 Mauaji kusetiri ushahidi .......................................................................... **68**

3.2.4 Tamaa ya mali na uongozi ..................................................................... **69**

3.2.5 Mauaji ya kujiokoa .................................................................................. **70**

3.3.0 Utekelezaji wa mauaji........................................................................ **71**

3.4.0 Athari ya mauaji ya kikatili.................................................................. **75**

3.4.1 Athari kwa wanajamii........................................................................ **75**

3.4.2 Athari kwa polisi.............................................................................. **77**

3.4.3 Athari kwa mpelelezi na wasaiizi wake................................................ **79**

3.4.4 Athari za kijinsia.............................................................................. **83**

3.5 Mikakati ya kukabiliana na uovu............................................................ **85**

3.5.0 Utangulizi........................................................................................ **85**

3.5.1 Mpelelezi kutumia vifaa ..................................................................... **86**

3. 5. 2 Mpelelezi hulazimika kubadili sura na hulka ...................................... **86**

3.5.3 Ushirikiano kati ya mpelelezi na watu wengine ...................................... **88**

3.5.3.1 Ushirikiano kati ya mpelelezi na wasaidizi wake.................................. **88**

3.5.3.2 Mpelelezi hushirikiana na polisi ....................................................... **89**

3.5.3.3 Ahadi ya tuzo kwa wanajamii............................................................ **91**

3.5.3.4 Wanajamii walishirikiana na wapelelezi ............................................. **92**

3.5.4 Mpelelezi kujisingizia kifo ................................................................. **93**

3.5.5 Matumizi ya Ishara ........................................................................... **94**

3.6 Hitimisho........................................................................................... **95**

**SURA YA NNE .......................................................................................... 96**

**MAUAJI, ATHARI ZAKE NA MIKAKATI YA KUANGAMIZA UOVU**

**KATIKA RIWAYA YA *TUTARUDI NA ROHO ZETU.* ..................................... 96**

4.0 Utangulizi........................................................................................... **96**

4.1.0 Kiini cha uovu................................................................................... **100**

4.1.1 Mazingira kama kiini kikuu cha maovu................................................ **100**

4.2.2 Mauaji katika misingi ya kisiasa........................................................ **103**

4.2.3 Mauaji ya kujinusuru ........................................................................ 104

4.2.4 Ubaguzi wa Rangi ........................................................................ 105

4.3 Utekelezaji wa mauaji ........................................................................ 106

4.3.0 Athari za mauaji ya kikatili ........................................................................ 108

4.3.1 Athari ya uovu kwa wanajamii ........................................................................ 113

4.3.4 Athari ya uovu kwa polisi ........................................................................ 115

4.3.5 Athari ya kiuana ........................................................................ 116

4.4.0 Mikakati kushika wahalifu inayotumika ........................................................................ 117

4.4.1 Kubadilisha hulka, jina na sura ........................................................................ 117

4.4.2 Kutumia siri ........................................................................ 119

4.4.3 Mpelelezi anatumia usaidizi wa watu wengine ........................................................................ 119

4.4.4 Ishara ........................................................................ 122

4.4.5 Vifaa ........................................................................ 124

4.4.6 Maarifa ........................................................................ 125

4.4.7 Sadfa ........................................................................ 128

**SURA YA TANO ........................................................................ 130**

**MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ........................................................................ 130**

5.1 Muhtasari wa Utafiti ........................................................................ 130

5.2 Matokeo ya Utafiti ........................................................................ 132

5.3 Changamoto za Utafiti ........................................................................ 139

5.4 Mchango wa Utafiti ........................................................................ 139

5.5 Mapendekezo ........................................................................ 140

**MAREJELEO ........................................................................ 142**

**VIAMBATISHO ........................................................................ 151**

KIAMBATISHO CHA 1: MAHOJIANO KATI YA MTAFITI NA REYSTUTA MTOBWA MTANDAONI ........................................................................................ **151**

KIAMBATISHO CHA 2: MAHOJIANO MTANDAONI KATI YA MTAFITI NA PROFESA MLINZI MULOKOZI .............................................................................. **154**

KIAMBATISHO 3: MUUAJI WA KIKATILI, ONYANCHA AKIONYESHA ALIKOZIKA WAHASIRIWA....................................................................................... **156**

KIAMBATISHO 4: KIONGOZI WA KIIMLA WA UGANDA.............................. **157**

KIAMBATISHO 5: KIONGOZI WA KIIMLA WA UJERUMANI, ADOLF HITLER .................................................................................................................. **158**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia masuala ya kimsingi katika utafiti ambayo ni usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia, na mbinu za utafiti zilizohusisha eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo.

## 1.1 Usuli wa utafiti

Kutokana na udurusu wa mtafiti, kuna aina nyingi za riwaya miongoni mwa hizo ni riwaya pendwa. Kuna haja ya kuchunguza jinsi fasihi hususan riwaya pendwa za Kiswahili zinavyoshughulikia swala la uovu. Utafiti umedhamiria kuchunguza jinsi ambavyo Ben R. Mtobwa ameangazia uovu katika riwaya zake. Mtobwa ni mmoja miongoni mwa waandishi chipukizi wa karne hii ya ishirini na moja waliotumia riwaya pendwa kuangazia uhalifu na uozo unaopatikana katika jamii. Kulingana na Madumulla (1988), wasanii wa riwaya pendwa wameipa fasihi ujumi wa kisasa. Mambo kama vile madanguro na mazingira machafu yanayopatikana katika jamii na jinsi mazingira mabaya hupanda mbegu ya uovu ndani ya mwanadamu, huangaziwa.

Kulingana na Wamitila (2003), riwaya ni kazi ya kinadhari na kibunilizi ambayo huwa na urefu wa kutosha. Njogu na Chimera (1999), wanasema kwamba riwaya ni utungo mrefu wa kubuni na wenye ploti, uliotumia lugha ya nadhari. Wataalamu kama Madumulla (1988), Bertoncini (1989) na Mwita (1995), wanasema kwamba kuna makundi mawili ya riwaya za Kiswahili: riwaya pendwa na riwaya dhati. Ashley (1989) anasema riwaya pendwa ni riwaya zinazosomwa na watu wengi. Anaelezea kwamba tukitaka kuelewa tofauti kati ya riwaya pendwa na dhati ni

kwamba, wasomi wengi wa riwaya pendwa hawana uwezo mwingi wa kuhakiki. Kulingana na Gromov (2008), Ben R. Mtobwa anashikilia nafasi kubwa barani Afrika kama mmoja kati ya waandishi wachache wanaotumia lugha ya Kiswahili kuandika riwaya za upelelezi. Utafiti huu umetumia riwaya za upelelezi zilizoandikwa na Ben R.Mtobwa kwa vile zinagusia sana mambo ya uovu. Kulingana na Kettle (1960) riwaya nzuri haistahili tu kutaja kuhusu maisha, bali kitu fulani katika maisha, kama vile mauaji ya kikatili.

Kuna waandishi na wahakiki wa masimulizi ambao wameshughulikia riwaya pendwa hasa zile za upelelezi. Miongoni mwao ni; Mohammed Said Abdulla, Faraji Katalambulla, Hammie Rajab, Eddie Ganzel na wengine. Mwandishi Ben R. Mtobwa ni miongoni mwa waandishi wa aina hiyo ya riwaya. Waandishi hawa walishughulikia zaidi ujuzi wa mpelelezi kuliko dhamira ya kufichua maovu ya kijamii. Syambo na Mazrui (1992), wanasema kuwa riwaya za upelelezi katika lugha ya Kiswahili zilianza kubuniwa katika miaka ya 1950. Mohammed Said Abdulla aliandika riwaya yake ya kwanza mwaka wa 1957. Miaka ya 1980, 1990 na 2000, ilishuhudia waandishi wengi sana wa riwaya za upelelezi hasa zile za Kiswahili nchini Tanzania. Riwaya hizi zina historia ndefu zaidi katika nchi za Kimagharibi. Kulingana na Gates (2006) Allan Edgar Poe ndiye aliyeanzisha riwaya za upelelezi katika miaka ya 1840.

Wahakiki wengi wamechukulia aina hizi za riwaya kama zenye kusudi la kutumbuiza au kusisimua tu. Madumulla (1988) anasema wahakiki wamepuuza riwaya hii kama kitu kisichofaa pengine hata pasipo kuisoma. Licha ya kupuuzwa huko na wahakiki, riwaya hizi hupenya na kufikia wasomaji wa tabaka mbalimbali za wanajamii. Fauka ya hayo, riwaya za Ben R. Mtobwa hazilengi kufurahisha tu bali zinatudhihirishia

mambo muhimu ya maisha. Hata hivyo, anatumia riwaya za upelelezi ambazo kulingana na Gibbe (1991) huibua kwa undani maovu ya jamii ambayo waandishi wa riwaya dhati wameyakimbia.

Utafiti huu umechunguza maudhui ya uovu katika jamii katika kazi teule za Ben R. Mtobwa. Maovu hayo yamejitokeza kwa njia mbalimbali kama vile: mauaji ya kikatili, ulevi, ukahaba, ufisadi, unafiki, ubaguzi wa rangi. Utafiti huu basi umekusudia kuchunguza jinsi ambavyo mwandishi huyu amesawiri uovu huu katika riwaya zake, hasa msimamo wake kuhusu kiini cha uovu na athari zake kwa wanajamii. Kwa vile riwaya teule za Ben R. Mtobwa ni za upelelezi, mauaji ya kikatili ni uovu ambao umejitokeza zaidi kuliko maovu mengine. Auden (1962), anasema kuwa mauaji ni uhalifu wa unaodhuru Mungu pamoja na jamii. Ni dhambi inayofanya jamii kuchukua nafasi ya mhasiriwa. Hivyo basi, tumetumia aina hii ya uovu kuweka wazi mtazamo wa mwandishi. Utafiti huu pia umelenga kuonyesha jinsi ambavyo mwandishi ametumia mbinu ya upelelezi kusawiri maudhui haya ya uovu. Aidha, umejaribu kuweka wazi mikakati inayotumika na mwandishi kukabiliana na uovu husika.

Kuna mambo mengi kuhusu uovu yanayomuathiri mwanadamu kwa njia hasi. Kulingana na Petit (1962) uovu ni kinyume cha wema. Fasihi kama kioo cha jamii ina jukumu la kusawiri maovu ili kutahadharisha jamii na kuielekeza kwenye mema. Uovu ni mojawapo ya maudhui ambayo husawiriwa katika kazi nyingi za fasihi ili kumithilisha uhalisia na maisha ya jamii. Ukosefu wa uadilifu ni kiundo msingi cha kuelewa uovu. Uovu hufanya mtu kukosa hulka njema na sifa bora ya kumfanya aitwe mwanadamu. Mwandishi anapoangazia uovu anampa mwanadamu uhuru wa kuchagua kuwa mwadilifu au muovu.

Kwa vile riwaya teule za Ben R. Mtobwa zimeshughulikia uovu na wema, ambapo mpelelezi huwasilisha wema naye mhalifu huwasilisha uovu, ni dhahiri kuwa maudhui ya riwaya hizi yamejikita kwenye maadili. Uovu kama vile mauaji ya kikatili umekuwa kero ulimwenguni ambapo siku haiwezi kupita bila visa vya mauaji. Tendo la kuua ni uovu unaoshutumiwa na walimwengu sawia na kisheria ambapo hakuna aliye na kibali cha kumtoa mwenzake uhai kwa sababu yoyote ile. Hivyo basi, utafiti huu umezungumzia uovu katika misingi ya mahusiano ya kibinadamu.

Ben R. Mtobwa anasawiri uovu huu kwa njia ya kipekee. Anadhihirisha mabadiliko ambapo anatumia riwaya zake kwa njia ya kisasa kuweka wazi maswala mazito yanayotokea katika jamii. Miongoni mwa waandishi wengi, tumechagua riwaya zake kwa vile ameandika riwaya za upelelezi za kisasa ambazo zina mafunzo zaidi kuliko zile za hapo awali. Upelelezi unakuwa ndiyo nguzo kuu ya kusawiri uovu katika kazi zake. Haangazii tu uovu bali hata kinachowachochea waovu hao kutenda uovu. Ingawa anatumia mpelelezi, mpelelezi yule anatumia nguvu zaidi kutatua shida zile. Maovu ndiyo yanayopewa kipaumbele bali `si mpelelezi kama anavyofanya Mohammed Said Abdalla na waandishi wengine wa jadi.

Ben R. Mtobwa ni mwandishi ambaye anaonyesha uhai wa fasihi kwa kugusia maswala nyeti na ibuka yanayopeana changamoto katika karne hii. Swala la uovu limekuwa donda sugu kwa wanajamii siyo Afrika mashariki tu bali ulimwenguni kote. Mwandishi huyu amebadilisha riwaya zake na kuzitumia kama gurudumu la kufunulia jamii kuhusu uovu. Utafiti huu ulitumia vitabu vya Mtobwa kuonyesha kinachomfanya mwanadamu kugeuka na kuwa na tabia za unyama na kumfanya mwanadamu kukosa utu.

Mwandishi huyu anachukua nafasi ya soko lake kubwa kuingiza mambo ya kijamii katika riwaya zake. Ben R. Mtobwa ameweza kugeuza riwaya zake kuwa za mafundisho na chombo cha kuzidisha tahadhari au ufahamu katika jamii, hasa kwa wasomi wa riwaya hizo. Kulingana na wataalamu Jenkins, (1994) Auden, (1962) na wengine, uovu kama vile mauaji ni sifa kubwa katika riwaya za upelelezi. Waandishi wengine wameshughulikia kwa jumla mambo ya uhalifu, utafiti huu umechunguza jinsi Ben R. Mtobwa anavyosawiri sifa ya uovu katika kazi zake. Katika kuchunguza usawiri huo, tumezingatia kuangazia uovu unaopatikana katika jamii, kiini chake na athari zake.

### 1.2 Suala la Utafiti

Utafiti huu umeeleza, kufafanua na kuchanganua riwaya mbili za Ben R. Mtobwa kwa lengo la kuonyesha jinsi anavyosawiri uovu, hasa mauaji ya kikatili. Riwaya zilizotumiwa kufanikisha utafiti huu ni: *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984), na *Tutarudi na Roho Zetu (*1987), Mtobwa anasimulia kuhusu uovu kupitia hadithi za upelelezi. Utafiti huu umelenga kubainisha wazi mtazamo wa Ben R. Mtobwa kuhusu uovu. Kuna haja ya kuelewa uovu wenyewe na athari yake juu ya wanajamii katika maisha ya sasa ili kuwatahadharisha dhidi ya uovu huo. Ingawa waandishi wa awali kama Mohammed Said Abdalla na Faraj Katalambulla wameshughulikia uovu na kutumia upelelezi kama mbinu ya kuwatambua waovu. Aidha, wao wamelenga zaidi umahiri wa wapelelezi wala si usuli, sura na uovu katika mkabala mpana wa kiuchangamano. Utafiti huu umeainisha uovu na kufafanua mbinu zinazotumika na Ben R. Mtobwa kumaliza uovu katika riwaya zake teule. Hata hivyo, utafiti huu umechanganua riwaya hizo kwa lengo la kudhihiri mtazamo wake kuhusu uovu. Katika kufanya hivyo, tumeonyesha jinsi Ben R. Mtobwa anavyotofautiana na watangulizi wake.

## 1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

i) Je, uovu upo, na kama upo umebainika vipi katika riwaya teule za Ben R.Mtobwa?

ii) Je, kiini au chanzo cha uovu ni nini hasa kwa kurejelea riwaya za Ben R. Mtobwa?

iii) Je, ni nini athari za uovu kwa wanajamii kwa mujibu wa Ben R. Mtobwa?

iv) Riwaya za Ben R. Mtobwa zinapendekeza mikakati ipi ya kukabiliana na uovu huu katika jamii?

## 1.4 Malengo ya utafiti

Malengo ya utafiti huu ni:

i. Kubainisha aina ya uovu katika riwaya za Ben R. Mtobwa.

ii. Kuelezea kiini cha uovu kwa mujibu wa riwaya za Ben R. Mtobwa.

iii. Kuelezea athari ya uovu kwa wanajamii kama yanavyojitokeza katika riwaya za Ben R. Mtobwa.

iv. Kuonyesha mikakati ya kukabiliana na uovu katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa .

## 1.5 Sababu za kuchagua Mada ya Utafiti

Maudhui ni masuala yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi yoyote. Hivyo basi, mshawasha wa kuchagua mada kuhusu usawiri wa uovu katika riwaya za Mtobwa ulifanyika kwa misingi ya sababu zifuatazo:

Riwaya ya Kiswahili ni utanzu unaoendelea kukua, hivyo basi utafiti ulipaswa kufanywa ili kutufahamisha iwapo mtunzi amezingatia uovu katika jamii za wakati huu. Maudhui hayo sharti yalenge jamii ya sasa ili wanaposoma wapate hisia za ndani au mhemko fulani unaowezesha kuhusisha matukio hayo na hali halisi. Kwa hivyo, utafiti wetu unafaa kubaini iwapo mtunzi ameibua maudhui mapya ya kuzingatia nyakati za sasa au zile kongwe zisizoeleweka na jamii ya sasa. Utambuzi wa maudhui huwa miongoni mwa vipengele muhimu vya lugha ya fasihi. Uteuzi mwafaka wa maudhui unadhihirisha umahiri wa mtunzi. Riwaya za Ben R. Mtobwa zinashughulikia maisha ya wanadamu hasa jamii ya karne hii ya ishirini na moja. Kwanza, uovu kama vile mauaji ya kikatili ni kati ya maovu yanayoangazwa Ben R. Mtobwa. Mauaja ya kikatili ni kati ya maswala ibuka na nyeti katika jamii yoyote ile. Aina hii ya uovu ndiyo inatajwa sana katika riwaya za Ben R. Mtobwa. Anatahadharisha wanajamii dhidi ya uovu kwa kuangazia athari ya mazingira mabaya kwa mwanadamu. Vilevile, msanii huyu anatoa tahadhari kuwa watu wanafaa kuwa waadilifu na kuepukana na maovu haya ambayo hutia dosari maisha ya mwanadamu.

Pili, kazi imenuia kuonyesha kuwa baadhi ya riwaya za upelelezi zina umuhimu na zinaweza kupendekezwa na wakuza mitaala kufunza fasihi katika shule za upili. Riwaya hizi zinaangazia uovu wa kikatili zaidi kuliko riwaya za kijamii. Swala la uovu linafaa kuzungumziwa ili wanafunzi na wanajamii kwa jumla waelewe malimwengu na jinsi ya kuepukana nayo. Hakuna njia bora zaidi kuliko sanaa, hasa riwaya zenye maudhui ya uovu wanazozienzi. Kumekuwa na mielekeo hasi kuhusu riwaya za upelelezi hapa Afrika Mashariki hasa miongoni mwa wataalamu. Kwa mfano A.J. Saffari katika Mwita (1995), alisema kwamba japo riwaya hizo zimeandikwa katika lugha ya Kiswahili, riwaya hizo si za Kiswahili maanake matukio yake hayaambatani na uhalisi wa utamaduni wa Kiswahili. Kezilahabi

(1975), anasema kwamba ingawa riwaya hizi zina ufundi wa kipekee, zinazua hali ya kuogofya na maadili ya wasiwasi. Madumulla (1988), naye amesema kuwa riwaya pendwa imekuwa ikipuuzwa kwa kiasi kikubwa na mashirika makubwa ya uchapishaji na wahakiki pia. S A. Mohamed katika Mwita (1995) anasema kwamba hizo si riwaya za Kiswahili bali ni mwigo duni wa riwaya za Uropa. Hivyo basi, utafiti huu ulijaribu kudhihirisha kuwa riwaya pendwa zina nafasi katika uendelezaji wa fasihi ya Kiswahili. Isitoshe, ulionyesha kwamba riwaya hizi zina mchango wa kimaudhui na kisanaa ambao ukitambuliwa na kuhakikiwa, utakuwa na mchango bora kwa fasihi ya Kiswahili.

Tatu, Ben R. Mtobwa ni mtunzi chipukizi na ilikuwa vyema kuchanganua kazi zake ili kubaini nafasi yake miongoni mwa watunzi wakongwe wa riwaya za upelelezi hapa Afrika Mashariki. Kwa kufanya hivyo, tunahimiza waandishi wengine kufuata mkondo huo wa uandishi. Lengo hili ndilo lilituchochea kuchagua riwaya zake. Baadhi ya watunzi wa riwaya za upelelezi zilizoandikwa katika lugha ya Kiswahili hapa Afrika Mashariki ni pamoja na Mohammed Said Abdulla na Faraj Katalambulla. Katika kuguzia maudhui uovu unaojitokeza katika jamii, analenga kutahadharisha jamii kupitia sanaa. Anatumia njia ya kipekee (mbinu ya upelelezi) kuweka wazi maswala yanayokumba jamii.

Nne, tulizingatia kufanya utafiti huu kwa lengo la kutaka kuelewa sura mbalimbali ya maovu na jinsi yanavyojitokeza katika jamii. Ben R. Mtobwa anatumia wahusika wake kisanaa kuweka wazi aina ya maovu yapatikanayo katika jamii. Tuliposoma vitabu vya Mtobwa, vilitusaidia kuelewa kutokana na tajriba ya wale wahusika ikiwa zile tabia za uovu zimetokana na mazingira au uasilia. Kuna aina mbalimbali za riwaya ambazo huzungumzia uovu na hata riwaya za kimajazi ambazo zimeandikwa

kuhusu maswala ya kijamii. Mwandishi kama Shaaban Robert katika kazi zake nyingi anaangazia uadilifu kama njia bora zaidi ya kumfanya mwanadamu aishi vyema na binadamu wenzake. Kwa mfano katika kitabu chake cha *Utubora Mkulima (1968)* na *Siku ya Watenzi Wote (1968)*. Anatumia wahusika wenye maadili mema kama mifano ya wanadamu wanaofaa kuigwa. Hii ina maana kwamba anakemea uovu na kuhubiri uadilifu katika riwaya zake.

Tano, usomaji wa awali ulibainisha kuwa tafiti nyingi zilifanywa lakini hakuna utafiti wa kina uliofanywa kuhusu uovu katika riwaya za Ben R. Mtobwa. Wao hawazungumzii kwa undani, athari ya uovu kwa wanajamii wengine. Riwaya za upelelezi kama zile za Mohammed Said Abdulla, zinakemea uovu. Kwa mfano Mohammed Said Abdulla (1968) anatumia mhusika mkuu (Bwana Msa), kutegua vitendawili kuhusu watu wanaofanya maovu katika jamii. Mpelelezi huyu anasawiriwa kama mtu mwenye akili nyingi anayechunguza na kuwatambua wale waovu.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Mtobwa ni mwandishi anayejulikana kwa kuandika riwaya pendwa. Yeye ni mmoja kati ya wale waandishi wachache ambao wamejikita katika uandishi wa riwaya za upelelezi. Anashikilia nafasi kubwa kati ya waandishi wa riwaya pendwa katika lugha ya Kiswahili barani Afrika. Kati ya vitabu ambavyo ameandika ni: *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984), *Najisikia kuua Tena* (1984*), Tutarudi na Roho Zetu* (1987), *Pesa zako Zinanuka (*1984) *Nyuma ya Mapazia (*1996), *Lazima Ufe Joram (*1983), *Mtambo wa Mauti* (2004), *Roho ya Paka (*1996), *Dimbwi la Damu (*1984*), Dar es salaam Usiku (*1989) *na Malaika wa Shetani (*1988).

Utafiti huu umejikita katika kushughulikia riwaya mbili za Ben R. Mtobwa kimaksudi ili kutimiza malengo ya utafiti. Riwaya hizo ni: *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984*) na Tutarudi na Roho Zetu (*1987). Ingawa kuna waandishi wengi walioshughulikia uovu, tulichagua riwaya za Ben R. Mtobwa kwa vile anawasilisha maudhui haya kwa njia ya kipekee. Mbali na kutambua uovu, anaweka wazi athari zake na mikakati ya kumaliza uovu katika jamii. Riwaya ambazo tulichagua zina mawanda mapana ya kutosha kuwakilisha mtazamo wa mwandishi huyu kuhusu swala la uovu. Utafiti ulizingatia zaidi mauaji ya kikatili kwa vile ndio uovu unaojitokeza zaidi katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa. Zinaangazia hasa mauaji ya kikatili kwa kina na hasa kiini kikuu cha mauaji hayo. Isitoshe, vitabu hivyo viwili ni kama vinaendelezana. Ben R. Mtobwa anatumia upelelezi kama mbinu ya kufichua mauaji ya kiholela yanayotokea katika jamii.

**1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada**

Utafiti mwingi haujafanywa kuhusu kazi za Ben R. Mtobwa ambaye ni mtunzi wa riwaya pendwa za Kiswahili katika karne hii ya ishirini na moja Gromov (2008). Aidha, kuna wataalamu wachache ambao walishughulikia kazi zake katika maandishi yao. Kwa mfano Mikhail Gromov (1996, 2008 na 2008) Mahiri Mwita (1995) Ranka Primorac na Gromov (2008). Baadhi yao wamezungumzia kazi zake kwa jumla hasa umaarufu wake katika uandishi wa riwaya za upelelezi. Hata hivyo kuna wataalam mbalimbali ambao wameshughulikia maswala mbalimbali katika riwaya za upelelezi na riwaya kwa jumla.

Gromov (1996) Katika kazi yake 'Tanzanian Prose in the 90s' anasema miaka hiyo ilishuhudia riwaya dhati zenye maudhui ya hadithi za mapenzi. Anaendelea kusema kuwa migogoro katika hadithi miaka ya 1970 na 1980 ilikuwa ni hali ya kuchagua

kati ya wema na uovu. Anamtaja Ben R. Mtobwa kama mwandishi mashuhuri wa riwaya pendwa. Anamwona kama mwandishi wa kipekee anayehitimisha hadithi za mapenzi bila kutoa suluhisho. Anataja *Dar es salaam Usiku* (1989) kama mfano mzuri wa riwaya za mapenzi iliyoandikwa bila kufuata tamaduni ya wema na uovu kama riwaya zingine. Riwaya hii haitoi mawaidha kwa msomaji ila, inamchochea kumulika matatizo aliyoyaguzia. Gromov anamwona kama mwandishi wa kipekee wa riwaya pendwa za kimapenzi, kwani wakati riwaya zingine za aina hii hukamilika kwa kuonyesha kuwa jamii iliyotengana hukutana na kuungana kwa furaha, Mtobwa naye anakamilisha hadithi hii kwa kuonyesha wahusika ambao maisha yao ya kimapenzi yanasambaratika, yanakanganya na yanaisha kwa huzuni. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu imetusaidia kuelewa kwamba Ben R. Mtobwa hudhihiri mtazamo wa kipekee katiku kazi zake. Hivyo basi ilitusaidia kuelewa upekee wake kuhusu kiini cha uovu na mikakati ya kupigana nao. Kuna tofauti kati ya kazi hii na yetu kwa sababu Gromov na wenzake wamechunguza riwaya za Tanzania katika miaka ya 1990 na wameangazia tu riwaya moja ya Ben R. Mtobwa. Isitoshe, riwaya aliyoishughulikia ni ya kijamii ilhali riwaya zilizotumika katika utafiti huu ni za upelelezi.Wao wanazungumzia usitawi wa riwaya za Ben R. Mtobwa na waandishi wengine katika miaka ya 1990. Kwa upande mwingine, utafiti huu umejikita katika kushughulikia maudhui ya uovu katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa .

Gromov (2008) ameandika Mahojiano kati yake na Ben R. Mtobwa, ambapo wanajadiliana kuhusu riwaya za Mtobwa kwa jumla. Anatueleza kwamba, kwa maoni ya Mtobwa vitabu vyake vinalenga kufunza jamii hasa vijana ambao ndio wapenzi wa riwaya za upelelezi. Anasema kwamba wanapokuwa wanashambulia mambo yanayoguza serikali au utawala, wao huyaweka katika riwaya kwa njia ya kisanii ili watu waelewe. Kulingana na Gromov hadithi za Ben R. Mtobwa hulenga sana vijana,

hii ni kwa sababu wao ndiyo wanaopenda riwaya za upelelezi. Anasema kwamba mtu anaposoma riwaya hizi hahitaji kufikiri mno, anaburudika na kujifunza maswala mazito ya maisha. Anazungumzia walengwa wake na lengo lake, sisi kama wahakiki kazi hii ilitufaa, kwa sababu imetuangazia lengo la msanii. Kuna tofauti kati ya kazi hii na yetu kwa sababu sisi tulilenga kubainisha maovu anayoangazia na mtazamo wa mwandishi kuhusu uovu.

Gromov (2008) kazi hii imeshughulikia riwaya zilizochapishwa kutoka miaka ya 2000. Anasema kuna aina mbili za riwaya pendwa: zile za mapenzi na uhalifu na za upelelezi. Anazungumzia mwelekeo wa riwaya pendwa hapa Afrika Mashariki hasa Kenya na Tanzania. Anatujulisha kuwa Kenya kinyume na Tanzania, imekuwa na mwandishi mmoja tu aliyejaribu kuandika riwaya za upelelezi. Gromov anasema Godfrey Levy aliwahi kuchapisha vitabu vitatu tu katika mwaka wa 1970, 1980 na 1990. Anaamini kuwa Kenya inakosa waandishi wa riwaya za upelelezi za Kiswahili zinazoweza kusomwa na watu wa nyanja zote za maisha. Anatueleza kuwa wanafunzi wengi wa Kenya hawashughuliki kusoma riwaya za Kiswahili baada ya shule. Anamtaja Ben R. Mtobwa kama mwandishi anayeandika riwaya za upelelezi zenye kuvutia watu wenye mapato ya kadri. Kazi hii ilitufaa kuelewa mielekeo ya watu kuhusu riwaya za upelelezi, na pia kutudhihirishia nafasi ya Ben R. Mtobwa hapa Afrika Mashariki kama mwandishi mashuhuri wa riwaya hizo. Kuna tofauti kati ya kazi hii na yetu kwa sababu sisi tulishughulikia usawiri wa uovu katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa.

Gromov na Primorac (2008) katika makala yao ya 'The Journal of Commonwealth Literature' wameandika kuhusu kumbukumbu za Ben R. Mtobwa. Wanatuelezea kwamba Mtobwa alitafsiri vitabu vyake kadhaa ambavyo vilisomwa kimataifa. Kwa mfano kitabu chake *Dar es salaam Usiku* (1994) amekitafsiri kuwa *Dar es salaam*

*At Night (1989).* Gromov na Primorac wanasema Ben R. Mtobwa ametumia uandishi wa kisasa wa riwaya pendwa kusawiri shida nyeti za kijamii bali si kuburudisha tu. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu imetusaidia kuelewa historia ya mwandishi huyu na sifa zake. Kuna tofauti kati ya kazi yetu na kazi hii kwa sababu wao wameandika kumbukumbu za Mtobwa ilhali kazi hii ilichunguza uovu unaoshughulikiwa katika kazi zake.

Kulingana na Mwita (1995) ameandika nafasi ya riwaya pendwa katika uendelezaji wa fasihi. Anabainisha riwaya pendwa na kuzungumzia wataalamu wanaozitetea na hata wale wanaoziponda riwaya hizo. Amesema riwaya pendwa inachangia sana katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Aidha katika kutumia nyenzo hii, waandishi wa fasihi pendwa hawa wanahakiki kwa mtazamo mkali udhaifu wa vyombo vya serikali katika utekelezaji wa majukumu waliyopewa katika nyadhifa zao. Katika riwaya pendwa wafanyikazi wa umma wafisadi na askari wazembe wasiofanya bidii kumaliza uovu wanamulikwa. Mwita anasema Ben R. Mtobwa ni mwandishi anayeonyesha uovu bila uoga. Anasema kwamba mtazamo wake ni tofauti na wale waandishi wengine wanaoguzia mambo haya ya uovu kijuujuu. Kazi hii ni muhimu kwetu maanake imetusaidia kuelewa maoni ya wataalam mbalimbali kuhusu riwaya pendwa. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu sisi tulitumia riwaya za Ben R. Mtobwa ambazo ni za upelelezi kuangazia uovo unaopatikana katika jamii na kuonyesha kiini pamoja na athari zake.

Kuna wahakiki walioshughulikia riwaya za upelelezi nazo zinakaribiana na hizo kazi za Ben R. Mtobwa. Kwa mfano:

Malmgren (2001) katika kitabu *Anatomy of Murder: Mystery, detection and Crime fiction.* anazungugumzia mauaji ya kikatili kama maudhui makuu katika riwaya za

upelelezi. Anamtaja Haycraft (1941) aliyeandika historia ya fasihi katika makala 'Murder for Pleasure: 'The life and Times of Detective Story.' Anasema riwaya bunilizi nyingi hutumia mauaji kama maudhui makuu. Aina hii ya bunilizi huwa kiundo msingi cha riwaya nyingi za upelelezi. Bunilizi hii inashughulikia jambo kuu katika maisha, kifo. Kazi hii ilikuwa muhimu katika utafiti wetu kwa sababu ilishughulikia maudhui tuliyolenga kutafiti.Tofauti iliyoko ni kwamba, sisi tulitafiti usawiri wa uovu wa aina hii katika riwaya za Ben R. Mtobwa ilhali wao waliangalia umuhimu wa maudhui mauaji katika riwaya za upelelezi kwa jumla.

Kezilahabi (1975) amehakiki riwaya za upelelezi. Anasema una ufundi wa kipekee lakini pia anaelezea udhaifu wake katika tukio la uovu, uajabu na mambo ya ajabu. Anasema yana hali ya kuogofya na maadili ya wasiwasi. Tulitumia riwaya hizi kuonyesha uovu unaogubika jamii. Kazi hii ilitusaidia kubainisha aina ya maovu tuliyofaa kujadili, kile ambacho tulielewa ni kwamba, mwanadamu hawezi kuwa muadilifu ikiwa haelewi ni maovu yepi yanamzunguka. Ndiyo maana kazi yetu ni tofauti sana na ya Kezilahabi maanake sisi tulitumia riwaya za Ben R. Mtobwa ambazo ni za upelelezi siyo tu kubainisha maovu bali pia kudhibitisha kwamba mazingira yana mchango mkubwa katika kusababisha maovu haya.

Auden (1962) anasema kwamba kusoma hadithi za upelelezi huleta mazoea kama vile kuzoea pombe. Anataja sifa kadhaa za riwaya za upelelezi. Anasema utaratibu katika riwaya za upelelezi ni kwamba kifo hutokea, wengi hushukiwa lakini mtu mmoja tu ambaye ndiye muuaji huangamizwa, aidha hufa au hushikwa. Kulingana na Auden wakati mwingine muuaji huwa anajulikana na hakuna washukiwa wa kuwekelewa shtuma lakini ushahidi unakosekana. Anatambua kwamba mara nyingi hadithi za upelelezi hujikita kwenye uovu na wema. Hadithi hizi hulenga kuzungumzia ukosefu wa maadili mema. Huwa na mvutano kati ya wenye hatia na wasio na hatia.

Anabainisha uhalifu unaopatikana katika riwaya za upelelezi. Shauku katika uchunguzi wa mauaji ni mtazamo wa wengi wasiyo na hatia na kusononeka kwa aliye na hatia. Hivyo basi, shauku katika riwaya za upelelezi ni upembuzi wa wale wasio na hatia na wenye hatia au wahalifu. Anasema kuna uhalifu unaohusu uhusiano wa mtu na Mungu na hata jirani yake, uhalifu dhidi ya Mungu na jamii, na uhalifu dhidi ya Mungu. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu inagusia mambo mengi kuhusu riwaya za upelelezi ikiwemo sifa na kiini cha mauaji katika riwaya hizo. Sifa anazozungumzia pia zilikuwa muhimu katika uchambuzi wa riwaya za Ben R. Mtobwa. Kazi hii ni tofauti na yetu kwa vile sisi tulishughulikia usawiri wa uovu katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa.

Leroy (1979) amezungumzia changamoto ambazo wahakiki wa riwaya za upelelezi hupitia. Anatuelezea kwamba riwaya za upelelezi hazijafanyiwa utafiti sana kwa sababu moja au nyingine. Anasema fasihi bunilizi za upelelezi huwa aidha pana mno au finyu, ndiyo maana kumekuwa na changamoto katika uhakiki wa riwaya za upelelezi. Kila hadithi huwa na mtazamo wake, kwani kuna wakati mitazamo hiyo huwa mema au uwe na upungufu. Anatueleza kuwa uhakiki wa riwaya za upelelezi huwa tofauti na zile za riwaya dhati tangu jadi. Kulingana na Leroy, wahusika wa riwaya za upelelezi huwa muhimu zaidi kuliko msanii aliyebuni kitabu hicho au mbinu zao za utungaji. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu inaangazia umuhimu wa riwaya za upelelezi na mbinu za kuzihakiki riwaya. Pia ilitusaidia kuelewa changamoto zilizotukabili tulipokuwa tunahakiki. Isitoshe pia alitueleza tofauti kati ya riwaya pendwa na riwaya dhati. Kuna tofauti kati ya kazi hii na yetu kwa sababu utafiti wetu ulihusu kuchunguza mtazamo wa Ben R. Mtobwa kuhusu uovu katika riwaya zake ambazo ni za upelelezi.

Chesterton katika Haycraft (1992) anaamini kwamba hadithi za upelelezi ndizo zenye usanaa zaidi. Anasema hadithi nzuri za upelelezi zina sifa zaidi kuliko zile mbaya. Ingawa kuna watu wanaoamini kwamba hakuna riwaya nzuri za upelelezi, hadithi hizi ndizo aina ya riwaya pendwa ya jadi zaidi. Hapa ndipo maisha ya kisasa hudhihirishwa hasa pale wanapotaja miji mikuu na hata mavazi ya kisasa. Kulingana naye, riwaya hizi hutukumbusha ulimwengu uliojaa vurugu, wahalifu na wasaliti. Hutufanya kuwa na jicho pevu tunapotizama watu kwani katika kila kikundi cha watu kumi na mmoja huenda ikawa mmoja ni mhuni. Kazi hii iltufaa kwa sababu ilituwezesha kuelewa umuhimu wa riwaya teule zilizotumika katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu Ben R.Mtobwa amatumia riwaya za upelelezi kuweka wazi swala la uovu. Ingawa kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu inajadili sifa za riwaya za upelelezi na kuelezea umuhimu wake, ni tofauti na utafiti wetu. Utafiti huu umetushughulikia usawiri wa uovu katika riwaya za Ben R. Mtobwa, ilhali yeye ameangalia sifa za riwaya za upelelezi kwa jumla.

Freeman katika Haycraft (1992) naye pia anataja sifa za riwaya za upelelezi. Anasema riwaya ya upelelezi huwa na sehemu nne ambapo anasema sehemu ya kwanza hushughulikia uhalifu. Uhalifu huunda chanzo asilia cha uchunguzi. Mwili wa hadithi hutoa vidokezo kuhusu hadithi, mpelelezi hutangaza hitimisho na baadaye kutangaza thibitisho la suluhisho au jibu. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu ilitupa mpangilio wa riwaya za upelelezi na umuhimu wake. Kuna tofauti kati ya kazi hii na yetu kwa sababu wao wameshughulikia sifa na mpangilio wa kazi za riwaya za upelelezi, ilhali sisi tutatumia vitabu hivyo kuangalia jinsi ambavyo uovu umesawiriwa katika vitabu vya Ben R. Mtobwa

Scaggs (2005) ameandika kuhusu riwaya za upelelezi ambapo anataja Bibilia kama chimbuko la upelelezi. Dorothy Layers katika Scaggs anatoa mfano wa Daniel katika

Bibilia na Jinsi alivyotumia mbinu ya upelelezi kumaliza wizi hekeluni. Scaggs anasema kuwa katika riwaya bunilizi za upelelezi ni lazima kwanza tuelewe kiini cha uhalifu. Kwake yeye, ana maoni kwamba ni jukumu la mpelelezi kutuangazia uhusiano kati ya chanzo na mwisho wa uhalifu. Matukio ya uhalifu yanatusaidia kuchora mipaka kati ya wema na uovu, hasa tabia zisizokubalika katika jamii. Mipaka hiyo husaidia kuunda sheria ambazo hutumika kudumisha haki katika jamii. Ana imani kwamba uhalifu ni lazima uadhibiwe kwani hata katika Bibilia Mungu alimuadhibu Kaini kwa kumuua Abeli. Utafiti wetu ni tofauti kabisa na huu kwa sababu umeshughulikia uovu katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa. Ingawa tafiti zote mbili zinataja uhalifu, yeye aliangazia uhalifu katika riwaya za upelelezi kwa jumla.

Kamau (1992) amefanya utafiti kuhusu ufundi katika riwaya za Muhammed Said Abdalla. Anashughulikia hasa matumizi ya lugha katika riwaya hizo za upelelezi. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu ametumia riwaya za upelelezi katika uchunguzi jinsi ambavyo sisi tulifanya. Ametoa sifa za riwaya za upelelezi ambazo zilitusaidia kuhakiki riwaya za Ben Mtobwa. Isitoshe, sifa hizo zilitufaa kuelewa mkondo wa riwaya za mwandishi huyu. Kazi ya Kamau ilitupa mwongozo wa kulinganisha riwaya za Ben Mtobwa kwa vile ametoa muhtasari wa hadithi zote za Mohammed Said Abdalla. Kazi hii ni tofauti na yetu kwa sababu Kamau amejadili ufundi katika riwaya za Mohammed Said Abdalla, ilhali sisi tulishughulikia uovu katika riwaya teule za Ben Mtobwa.

Hussein katika Topan (1971) amehakiki ufundi wa riwaya ya *Msimu Wa Watu wa Kale.* Anasema kwamba ufundi wa Abdalla umejiruhusu kutawaliwa moja kwa moja na mithali ya kigeni. Yeye anaamini kuwa lengo kuu la riwaya za Abdalla ni kuburudisha bali si kuelimisha. Anasema nchi huwa na mauaji au maasi mengi

ambayo polisi pekee yao hawawezi kuyachunguza. Ukubwa wa nchi, wingi wa watu, maendeleo na ustaarabu wa kisasa husababisha maasi. Maasi haya husababisha haja ya mpelelezi wa siri kuchunguza. Anaamini kuwa mambo kama vile habari za mpelelezi wa siri katika miaka ya 1957 ilikuwa nadra sana katika Bara la Afrika na hasa Unguja. Imani yake ni kwamba vitabu vya Mohammed vimetawaliwa na kujengwa na mithali ya Sharlock Holmes. Kazi hii ni muhimu maanake ilituongoza kutathmini na kulinganisha kazi ya Mohammed said Abdalla na za Ben R. Mtobwa. Tofauti iliyoko ni kwamba Hussein amehakiki kazi ya Mohamed Said Abdalla ilhali sisi tulitumia vitabu vya Ben R Mtobwa katika uchunguzi wetu.

Senkoro (1987) akijadili fasihi katika enzi za ubepari anasema riwaya za upelelezi hushughulikia tu swala la kusisimua na kupumbaza. Senkoro alionelea kwamba riwaya hizi hazikujihusisha na matatizo halisi ya wanyonge na zilipoyashughulikia zilipotosha ukweli wa matatizo hayo. Senkoro anaungama kuwa riwaya hizi zilisisimua kutokana na fani yake ya kuvutia. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu ilitusaidia kujadili dhima ya riwaya za upelelezi. Tulipotalii fasihi katika enzi za ubepari, tuligundua kwamba mbali na kuburudika kuna maovu yanayoangaziwa ambayo yanafaa kuchunguzwa. Kuna mengi ya kujifunza katika riwaya hizi pendwa ambayo yanasawiri hali halisi ilivyo katika jamii. Kazi hii ya Senkoro ni tofauti na yetu kwa sababu anazungumzia riwaya pendwa kwa jumla na hata kuzungumzia udhaifu wa riwaya za upelelezi. Kwa upande wetu sisi tulitumia riwaya za upelelezi zilizoandikwa na Ben R. Mtobwa kuangazia uovu katika jamii, kiini chake na athari zake.

Kalas (2009) ametaja kuwa mambo ya upelelezi yana mizizi katika Biblia. Anasema kiini cha upelelezi ni Biblia. Anapeana mifano kadhaa ya hadithi za upelelezi katika

Bibilia ikiwemo hadithi ya Judah na Tamar, Jacob na Leah, Judah na ndugu yake Joseph. Kazi hii ilitusaidia kuelewa na kujadili dhima na kina cha hadithi za upelelezi. Isitoshe, inatudhihirishia kwamba, mbinu ya upelelezi ilikuwa njia bora ya kumaliza uovu katika enzi hizo. Kazi hii ni tofauti na yetu kwa sababu wao walichunguza hadithi za upelelezi katika Biblia takatifu ilhali sisi tulichunguza usawiri wa uovu katika riwaya za Ben R. Mtobwa.

Wink (1980) katika makala ya *Detective Fiction: A Collection of Critical Essays* anataja Macdonald (1977), na Grella (1976) ambao wameshughulikia riwaya za upelelezi. Wink anataja wahakiki wengi wanaozungumzia ubunifu wa riwaya za upelelezi katika hadithi zao. Anataja Barzun (1961) ambaye anasema upelelezi huangazia ukweli wa hali ilivyo katika jamii. Isitoshe, anatuangazia jinsi Natty Bumppo alivyosema kuwa lazima kuwe na mtu anaeweza kuilinda jamii kutokana na jamii yenyewe. Mtu asiyefungwa na urasimi wa kijamii ambao mara nyingi umetukuka kiasi cha kutojali haki hata angalau kidogo tu. Barzun (1961), amesema katika makala yake *Detection and The Literary Art* kwamba mauaji hufanya hadithi za upelelezi kuwa na msisimuo fulani. Haya humpa msomaji shauku ya kutaka kujua kilichotokea baadaye. Ni katika riwaya za upelelezi tu ambapo nguli huonekana mwerevu sana kama anavyosawiriwa na mwandishi. Jamii huwa na shauku ya moja kwa moja katika uovu huu. Katika maisha ya kawaida adhabu kali huepukwa. Hata hivyo, katika fasihi ya upelelezi muuaji hafai kuishi. Wahakiki hawa wanazungumzia dhima ya riwaya za upelelezi ilhali sisi tulishughulikia usawiri wa uovu katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa.

Macdonald (1977) amesema kuna uhusiano wa kipekee kati ya mwandishi na mpelelezi katika riwaya za upelelezi. Tangu jadi hasa wakati wa Poe na Chandler na

enzi hizi, nguli au jasusi mkuu katika hadithi hizi huwakilisha mwandishi. Mara nyingi hujaribu kuweka wazi maoni yake katika jamii na fikra zake za kimaadili katika matendo. Ameziainisha hadithi za upelelezi ambapo zingine ni za kihistoria, zingine zimewekwa katika muktadha wa kimofolojia na muktadha wa kuhakiki. Kuna tofauti kati ya kazi hii na utafiti wetu kwa sababu Macdonald anachunguza uhusiano kati ya nguli na mwandishi wa riwaya hizo na changamoto ya kuchunguza riwaya za upelelezi ilhali sisi tulichunguza usawiri wa uovu katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa.

Price-Anisman (1982 vol.i) anasema kwamba kuna vitabu vya upelelezi vyenye manufaa sana kwa mwanafunzi. Kuna istilahi za upelelezi katika hadithi ambazo huweza kutumiwa katika kazi zote. Yeye ni mmoja kati ya watetezi wa riwaya hizi ambazo anaamini huweza kufaidi wanafunzi kupata ustadi. Anasema wanafunzi hao huishi katika mazingira yenye fujo na ukosefu wa matumaini hivyo basi huwa na uelewa kuhusu wema na uovu, uhalifu na wahalifu, haki na uovu. Anaamini kwamba athari ya hadithi hizi hutosha kumsaidia mwanafunzi kuwa na uhuru wa kujiamulia mambo. Waovu na wapelelezi ambao ndio washiriki wakuu, mwishowe huonyesha uadilifu na ukosefu wa maadili. Swala la mauaji huondoa ubunifu na kudhihiri uhalisia ambao wanafunzi wanaelewa. Kazi hii ni muhimu kwetu maanake ilitusaidia kujadili dhima ya riwaya za upelelezi. Kuna tofauti kati ya kazi hii na yetu kwa sababu yeye anaangazia umuhimu wa riwaya za upelelezi kwa wanafunzi ilhali sisi tulijikita katika usawiri wa uovu katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa.

Minjok (2011) anaangazia jamii ya miaka ya 1944-1965. Ameshughulikia sana kipengele cha fasihi ya jamii. Yeye analenga zaidi wasomi wengi wa wakati huo ambapo anatuambia sifa za usomi wa hadithi za upelelezi ni wa kihistoria bali si wa kisasa tu. Kazi hii ilitusaidia kuelewa chanzo au historia ya umaarufu wa hadithi za

upelelezi. Utafiti wetu ni tofauti maanake sisi tulishughulikia uovu unavyosawirIwa katika riwaya za upelelezi zilizoandikwa na Ben R. Mtobwa.

Wrong katika Haycraft (1992) aliandika makala 'Crime & Detection' ambapo anatetea riwaya za upelelezi kwa kusema kuwa ni sanaa iliyokuwepo tangu jadi. Anatoa mifano ya watu waliodhihirisha kuwa wapelelezi hodari katika enzi za kale. Anapeana mfano wa Daniel katika Bibilia na zile kesi alizotatua kwa kutumia upelelezi. Anarejelea hadithi ya Susanna na wazee wawili waliodai kwamba walimshika akiwa mikononi mwa mpenziwe. Daniel alidhihirisha umaahiri wake katika upelelezi kwa kutatua kesi hiyo. Kisa hicho cha kudhihirisha kuwa mwanamke yule hakuwa na hatia kinaonyesha kuwa alikuwa mpelelezi hodari wa enzi zake. Mfano mwingine anaotoa ni wa Herodotus kule Misri, ambaye anaamini alitumia mbinu zisizo za kawaida kuwatambua wahalifu. Kazi hii ni tofauti na yetu inashughulikia wapelelezi katika hadithi za jadi ilhali sisi tulishughulikia riwaya teule za Ben R. Mtobwa ambazo ni za kisasa kutafiti kuhusu uovu katika riwaya zake.

Kuna kazi zingine zinazohusu maendeleo ya riwaya kwa jumla, kama vile:

Madumulla (1988) ameandika kuhusu kipindi maalum cha uandishi wa riwaya pendwa katika kitabu chake *Riwaya za Kiswahili*. Anaamini kwamba katika kila kipindi cha maisha kuna matukio fulani ambayo hujitokeza zaidi kuliko mengine. Anasema kipindi cha miaka ya themanini riwaya nyingi ziliandikwa ikiwemo zile za fasihi pendwa. Anaendelea kusema kuwa ni katika kipindi hicho cha miaka ya themanini ndipo fasihi ya Kiswahili iliathiriwa sana na matukio ya kiuchumi. Anatupa mwanga au taswira ya kutuwezesha kuelewa hali iliyofanya waaandishi kubobea zaidi katika matukio ya kijamii. Anasema kwamba riwaya pendwa hufichua hali halisi ya uozo unaopatikana katika jamii. Kazi hii ni muhimu kwetu maanake ilitupa uelewa kuhusu changamoto za kijamii zilizokuweko wakati huo na wimbi la uandishi

uliotumika. Inatupa nafasi nzuri zaidi ya kutambua mambo muhimu yaliyompa mwandishi msukumo wa kuchagua maudhui yake. Mwandishi huyu pia anazungumzia zaidi riwaya pendwa hasa dhima yake katika uandishi. Anaamini kwamba riwaya pendwa si tupu kama wanavyodai wataalamu wengine. Kwa vile kazi yetu inashughulikia vitabu ambavyo tunaweza kusema ni riwaya pendwa, anatupa taswira kamili ya sifa za riwaya pendwa. Kwa mujibu wa Madumulla (1988) aina hii ya fasihi inachora mstari wa mkengeuko kutoka katika hali ya maisha ya kijadi, kwenda ya kisasa yaliyoathiriwa na ubepari. Kazi hii ni tofauti na yetu maanake yeye anashughulikia waandishi wa riwaya pendwa kwa jumla pamoja na sifa zake, ilhali sisi tulishughulikia riwaya za Ben R. Mtobwa na jinsi anavyotumia riwaya zake kusawiri uovu katika jamii.

Arnold (1984) anaangazia historia ya fasihi pendwa nchini Tanzania. Anazungumzia fasihi pendwa ambapo anaelezea hatua kwa hatua historia ya fasihi pendwa nchini humo. Anasema kwamba hapo awali kuliwekwa uthibiti au ukaguzi. Kulingana na Arnold, Tanzania ilipiga marufuku fasihi pendwa kama vile vitabu vya mwandishi mashuhuri wa Kenya David Maillu. Pia wakadai kuwa waandishi Gabriel Ruhumbika na Ismaail Mbise walikuwa wameathiriwa na Ngugi Wa Thiong’o. Wao wanasema wataalam wa uandishi wanafaa kuandika mambo yanayotokana na jamii na yenye kuzungumzia watu wenye tabia bora ili kuendeleza maadili. Ana imani kwamba watu walihimizwa kufanya hivyo kwa kutumia lugha yenye kukubalika na utamaduni wao. Anahimiza watu wasiwe kama Maillu wa Kenya anayeandika kazi zisizomfaa mwanadamu. Kwake yeye riwaya pendwa haina maana isipowekewa ithibati. Anaendelea kusema kuwa tangu miaka ya sabini, fasihi pendwa iliendelea kushamiri. Anaamini kuwa siku hizi serikali hupinga tu maandishi yanayopinga au kuguzia mambo yanayoguza serikali. Anapeana mfano wa kitabu cha *Cheche* kilichopigwa

marufuku chuoni mwaka wa 1970. Anamtaja Kezilahabi, ambaye anasema riwaya pendwa za kisasa huwa na wahusika wanaoiga wale waigizaji wa filamu za Kimerikani, hasa zile za ujasusi. Kwake yeye (Kezilahabi) hadithi hizi hutoa elimu kwa majambazi wanaotesa jamii. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa maana riwaya tumeshughulikia ni riwaya za upelelezi ambazo ni sehemu ya fasihi pendwa. Pili, imetusaidia kuelewa historia ya riwaya pendwa nchini Tanzania, ambako mwandishi Ben Mtobwa anatoka. Tatu, imetusaidia kuelewa dhima ya riwaya pendwa kwa wanajamii, kama asemavyo Arnold kuwa riwaya pendwa za sasa hulenga jamii. Utafiti wetu ni tofauti na huu kwa sababu wao wameshughulikia historia ya riwaya pendwa nchini Tanzania ilhali sisi tumeshughulikia riwaya pendwa aina ya upelelezi katika riwaya za Ben R. Mtobwa. Tumejaribu kuchunguza na kuelezea jinsi anavyosawiri uovu katika riwaya zake teule.

Kuna maandishi mengine ambayo ni ya kijumla zaidi ingawa yalitufaa katika utafiti wetu, kwa mfano:

Kuna wahakiki wa riwaya kama vile Muindi (1990) Ochenja (2008) Kibet (2005) Kimani (2003), Njogu (1997) ambao wameshughulikia maswala au vipengele kadhaa vya uovu. Kazi hizo zinakaribia tu ya Mtobwa lakini si sawa. Kwa mfano Njogu anaamini kwamba fasihi haiwezi katu kujitenga na maswala ya kijamii kwani ndiyo impayo mwandishi ilhamu akaandika kazi yenye mguzo unaotokana na sanaa yake. Muindi (1990) naye ameshughulikia aina moja tu ya uovu, ambayo ni ukahaba. Kibet (2005) ameangalia matatizo kwa jumla yanayokabili jamii katika riwaya za Burhani. Kwa upande wetu tutajikita tu katika uovu unaochafua jamii. Kimani (2003), naye ametafiti swala la dhuluma dhidi ya mwanamke, na hicho ni kipengele kimoja tu cha uovu. Osore (1994), naye amehakiki vitabu vya Mohamed Suleiman Mohamed. Kazi hii ilitusaidia kwa kutambua uovu unaotendwa na wahusika katika jamii. Kazi ya

Ochenja (2008), ilitufaa kudondoa mifano zaidi ya uhalifu unaokabili jamii zetu. Tofauti kati ya kazi hizi na yetu ni kwamba wao hawajatalii swala la uovu katika riwaya teule za Ben R.Mtobwa.  Pili, hawazingatii mazingira kama kichochezi kikuu cha matendo hayo ya uovu.

Mgeni (1983) amezungumzia vipengele vingi vinavyodhihirisha wazi kwamba kuna uajabu mwingi katika riwaya za Abdalla. Anasema Saidi Abdalla anatuonyesha tajriba ya uajabu usiopatikana katika riwaya nyingi za upelelezi. Anatueleza jinsi Bwana Msa anavyofumbua mafumbo yaliyojificha kwa njia ya kiajabu. Anataja riwaya za *Kisima Cha Giningi* (1968) na hata *Siri Ya Sifuri* kama riwaya zinazodhihirisha uajabu wa hali ya juu. Mwanzo wenyewe wa *Kisima cha Giningi* unadhihirisha uajabu. Anaelezea uajabu unaohusishwa na kisima cha Giningi. Kulingana na Mgeni, maneno yenye kukanganya yanayotumika katika vitabu hivyo na Bwana Msa yenyewe yanadhihirisha uajabu. Anasema riwaya za Abdalla zinasawiri Bwana Msa (ambaye ndiye mhusika mkuu katika vitabu vyake) kama mtu wa ajabu. Kazi hii ni muhimu kwetu maanake ilitusaidia kulinganisha riwaya za Abdalla na zile za Ben R. Mtobwa. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu yeye anazungumzia uajabu katika riwaya za Said Abdalla ilhali sisi tumetafiti kuhusu usawiri uovu katika riwaya za Ben R. Mtobwa.

Miller (2004) anasema kwamba waovu lazima wawajibike kwa matendo yao. Anazungumzia video za vurugu  kama kiini cha kuongezeka kwa ujeuri. Anazungumzia athari za kitamaduni, kijamii na kisiasa. Mtaalamu huyu anatahadharisha jamii dhidi ya mabadiliko ya kitamaduni ambapo walimwengu wameingiliana sana. Maoni yake ni kwamba wanadamu wanafaa kujitahadhari na tamaduni zingine zinazoingizwa katika jamii zao hasa mila zenye kuleta vurugu katika maisha ya kila siku. Kazi hii ni muhimu kwetu maanake inaangazia athari ya

mazingira kwa wanadamu. Tofauti kati ya kazi hii na utafiti wetu ni kwamba wao wameshughulikia athari ya vyombo vya habari, ilhali sisi tumechunguza usawiri wa uovu kwa jumla katika riwaya za Ben R. Mtobwa.

Utafiti huu ni tofauti na tafiti zilizofanywa awali kwa sababu zifuatazo. Kwanza umebainisha uovu katika riwaya za Ben R. Mtobwa. Pili umeangazia kiini cha uovu na athari zake kama inavyosawiriwa katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa. Aidha, umefafanua mikakati au mbinu za upelelezi zinazotumika na mwandishi katika riwaya hizo kukabiliana na uhalifu. Kulingana na udurusu wa mtafiti, tafiti za awali hazijashughulukia suala la usawiri wa uovu katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa. Utafiti huu hivyo basi, ulijaza pengo hilo na hivyo kuendeleza taaluma ya fasihi ya Kiswahili katika kipengee cha maudhui katika riwaya za upelelezi.

### 1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia changamano ambayo imejumuisha baadhi ya mihimili ya Nadharia ya Maadili na Nadharia ya Uhalisia. Nadharia hizo mbili zimesaidia kubainisha na kuyajadili maswala yanayoangazia vipengele mbalimbali vya maisha ya kisasa. Kwanza Nadharia ya uhalisia pia imetuongoza kuelewa athari ya maovu hayo na hatua za kukabiliana na maovu haya.

#### 1.8.1 Nadharia ya Maadili

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Maadili imetuongoza kutambua maovu katika riwaya zilizoteuliwa. Nadharia hii huelezea chanzo cha uovu na wema japo inajaribu kuangazia wema zaidi. Inabainisha maana ya wema na kufunza kinyume cha maadili (uovu). Nadharia hii pia hulenga kufafanua mambo muhimu ambayo binadamu anastahili kushughulikia katika maisha yake. Nadharia ya Maadili ilituongoza

kuelewa uhusiano kati ya fasihi na tajriba za binadamu. Waasisi wa Nadharia ya Maadili wanasema kwamba fasihi ina majukumu ya kufichua maovu yaliyopo katika jamii na kuielekeza jamii kwenye mema kwa kubainisha njia za kushinda uovu. Jukumu kubwa la nadharia hii ni kufunza maadili, ingawa katika uadilifu kuna ukosefu wa maadili. Inaelezea fasihi kama yenye kutoa mifano miema ya kuigwa na potovu ya kuepukwa. Nadharia ya Maadili inahusishwa na mwanafalsafa Jean Jacques Rousseau katika kazi zake *Social Contract* na *Discourse of Inequality.* (1712-1778)

Rousseau (1778) katika kazi yake anasema kwamba katika maisha ya kawaida mwanadamu huwa mzuri lakini hupotoshwa na jamii ambayo hudhania imestaarabika. Anaamini binadamu anafaa kuongozwa na sheria za kiasilia (sauti ya Mungu) ambayo huchangia katika kumfanya mtu awe mwema. Yeye ana imani katika wema wa kiasilia wa mwanadamu. Anasema ujumi na maadili ambayo hupotoshwa kwa wanajamii hutegemea maadili ambayo hupitishwa na wanajamii. Anaendelea kusema kwamba upendo katika familia ndiyo msingi au chanzo cha furaha katika maisha ya binadamu. Anasema binadamu hupotoshwa na jamii. Anaendelea kusema kwamba haki ya kiasilia na sheria, haina maana ikiwa hatuelewi maumbile ya mwanadamu. Katika kazi yake *Moral Education* anasema kwamba kutenda wema ndiko hufanya mtu kuwa mwema. Rousseau aliona kuwa hali ya kuwa na maadili ya hali ya juu kama kipawa na akawa na imani kuwa lengo kuu la elimu iwe ni kukuza maadili. Katika kazi yake '*Confessions of Rousseau*' anasema ukatili aliotendewa na mwajiri wake ulimfanya awe na tabia mbaya kama udanganyifu, wizi na kadhalika.

Kulingana na Kant (1724-1804) matilaba yetu hudhibitiwa na akili zetu.Tendo lolote la kimaadili ni lile ambalo huamuliwa na fikra. Tendo huwa la kimaadili tu ikiwa

lenye mantiki. Thamani ya tendo la kimaadili hubainishwa kwa kuchunguza sababu ya kutenda tendo hilo bali si matokeo ya tendo. Kant aliamini kwamba urazini wetu, ndiyo muhimu zaidi katika uasilia wa mwanadamu. Hicho ndicho chanzo cha hadhi yetu na ujitawala. Anaendelea kusema kwamba kila mwanadamu ana wajibu wa kimaadili kuheshimu hadhi na thamani aliyonayo yeye na hata wenzake.

Kulingana na Tolstoy (1960) sanaa nzuri ni ile inayoweza kupitisha ujumbe kwa watu wengi na inayoeleweka na kila mtu. Nadharia ya maadili ilifaa katika kubainisha ikiwa waandishi wa fasihi ya Kiswahili wanaonyesha jinsi maadili yanapotoshwa kupitia mtazamo wa binadamu wenye nyoyo za tamaa, unyama na ukatili. Tolstoy anaeleza sanaa kama uwezo wa kusimulia mambo yanayohusiana na maadili ya wanajamii. Mwitifaki huyu anaona fasihi kama zao la jamii. Anasema fasihi hueleweka tu inapohusishwa na mazingira ya kijamii yanayoizalisha. Kulingana na wahakiki wa kimagharibi, msanii huwa na ufahamu na huathiriwa na jamii yake kiasi cha kuandika yale yanayoipa jamii hiyo mwongozo mzuri. Msingi huu basi huifanya fasihi kuwa kielekezo cha jamii.

Kulingana na mwanafalsafa Hough (1966) sheria iliyo bora katika fasihi pia ni bora maishani. Katika kitabu chake the *Moral Theory* anasema fasihi lazima ihusiane na kiwango fulani ama tajriba ya mwanadamu. Fasihi lazima iwakilishe picha ya uhalisia. Anaamini fasihi hutoa wahusika wenye mifano mizuri ya kuigwa na pia wale wenye tabia mbaya za kuepukwa. Anadai kuwa sheria iliyobora katika fasihi ni bora pia maishani. Anaongezea kuwa fasihi hutoa malighafi ya kutoa uamuzi wa kimaadili jinsi ambavyo maisha hufanya. Kwake yeye, anaona fasihi kama njia ya pekee ya kuweka wanadamu katika undugu. Anaiona fasihi kama yenye mchango mkubwa katika matendo na thamani ya mwanadamu.

Palmer (1992) anachunguza umuhimu wa uelewa wa maadili katika kazi za kisanaa kama zile za fasihi. Anasema kazi hizo huchangia sana katika falsafa za kimaadili. Anasema kuwa mielekeo ya kimaadili ni muhimu katika kuelewa wanadamu. Anawashutumu wale ambao huingiza siasa katika mambo ya kisanaa kwa kusema kuwa, lazima kazi ya sanaa ihusiane na maisha ya kawaida. Anaendelea kusema kuwa ingawa anapambanua kati ya sanaa na maisha, haimaanishi kuwa kazi za sanaa ni aina tofauti na maisha bali tofauti hutokea tu katika nia na mpangilio wa kazi hizo. Kwake yeye fasihi inaweza kutupa uelewa zaidi wa kimaadili bila kututolea maelezo. Aidha, anajadili zaidi mchango wa mila hasa lugha katika sanaa na mchango wake katika ukuzaji wa maadili maishani.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) dhana ya maadili hutumiwa kuelezea usomaji na tathmini ya kazi za kifasihi kwa kuangalia uhusiano wake na ubinadamu na hasa maswala ya kimaadili badala ya kuzingatia ujumi wa kazi hiyo. Kuna kazi nyingi katika fasihi ya Kiswahili ambazo zimeegemezwa kwenye misingi ya kimaadili. Waandishi waliotajwa kwa kutilia uzito dhana ya kimaadili ni kama vile Shaaban Robert katika *Adili na Nduguze* (1962), *Utubora Mkulima* (1968) na Ali Jamaadar katika *Mui Huwa Mwema* (1978).

Kulingana na Vaughn (2008) maadili hurejelea imani kuhusu uovu na wema, uzuri au ubaya. Anasema imani hiyo hujumuisha hukumu, thamana (manufaa), kanuni, sheria, na nadharia. Vaughn ni mwenye imani kwamba maadili husaidia kuongoza matendo au mienendo yetu, kufasili thamana yetu na sheria zinazotuongoza. Maadili hutupa sababu ya kujitambua. Isitoshe Vaugnh anasema maadili hujibu maswali yanayohusu njia bora ya kuishi. Anasema nadharia ya maadili ni maelezo kuhusu kile kinachofanya tendo lolote kuonekana kuwa zuri au baya.

**Mihimili ya nadharia ya maadili ni:**

1) Fasihi ni kielelezo cha jamii. Hufichua uovu uliopo katika jamii na kuielekeza jamii hiyo kwenye mema. Mhimili huu ulitusaidia kuangazia maovu ambayo hutendwa na wanaohusika katika maovu hayo kwa mujibu wa riwaya teule za Ben R. Mtobwa.

2) Msanii huwa na dhamira ya kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili hasa kwa kukemea yale yanayopotosha jamii. Mhimili huu ulisaidia mtafiti kuona maadili yanayolengwa kupitishwa na wandishi kuwa wasomaji kupitia kazi zao.

3) Maadili ya jamii yanaweza kutokana na mahusiano kati ya wanajamii mbalimbali na mazingira yao. Mhimili huu ulituwezesha kudhihirisha majukumu ya mwanasanaa wa fasihi katika kurekebisha jamii yake kimaadili.

Mihimili hii ilitusaidia kushughulikia uovu unavyofasiriwa kimaadili. Ingawa nadharia ya maadili ilitusaidia kubainisha mtazamo wa mwandishi kuhusu uovu. Tulilazimika kutumia nadharia ya uhalisia ili kudhihirisha hali ilivyo kihalisia katika jamii siyo tu inayozungumziwa na mwandishi bali hata jamii ya sasa.

### 1.8.2 Nadharia ya Uhalisia

Nadharia hii iliasisiwa na mwanafalsafa Hegel katika kitabu cha *Aesthetics*. Alipendekeza matumizi ya neno uhalisia kuelezea kazi za kifasihi ambazo zinawakilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako kuna wahusika wanaotenda mambo kwa kulingana na jinsi wanavyochochewa waziwazi na hali waliyomo. Nadharia hii husisitiza usawiri wa uhalisi katika ukamilifu wake. Katika mtazamo wa uhalisia, yanayoshughulikiwa hayana budi kutendeka katika ulimwengu halisi.

Mwanasanaa lazima aelewe ulimwengu wake kama kitu kinachobadilika. Mchango mkubwa wa nadharia hii ni kuweka wazi hali ya maisha jinsi yalivyo.

Kulingana na Lukacs (1972) Nadharia ya Uhalisia ilianza kuhusishwa katika fasihi kwa sababu waasisi wa nadharia hii waliona kuna uhusiano mkubwa kati ya kazi za kisanaa na mtazamo wa msanii kuhusu anamopatikana. Lengo letu la kutumia nadharia hii ilikuwa ni kuihakiki kazi za msanii ili kuona ni kwa kiasi gani anadhihirisha uhalisia na umuhimu wake katika fasihi ya Kiswahili. Kulingana na mwandishi huyu, msanii anafaa kuwa kurunzi ya jamii. Jukumu la msanii ni kujaribu kuonyesha ukweli na linafaa kudhihirisha ukweli. Msanii huyu pia anafaa kutumia kipawa chake kutoa taswira ya mazingira yanayoaminika; yaani yawe na uhalisi wa kuaminika. Anasema wanauhalisia waliamini kuwa madhumuni ya mwandishi kwa jumla ni kuwarudisha watu katika ulimwengu wao wa kawaida. Hivyo basi ulimwengu anawoumba mwandishi unafaa kuwa wa kweli na halisi.

Larkin (1977) anasema kuwa wanauhalisia waliamini kuwa madhumuni ya mwandishi kwa jamii ni kuwarudisha watu katika ulimwengu wao wa kawaida na kwamba ulimwengu atakao uumba mwandishi uwe wa kweli au halisi. Jukumu la msanii linafaa kuwa la kweli na linafaa kudhihirisha ukweli. Ili kudhihirisha ukweli, msanii anafaa kutumia kipawa chake kuchora wahusika na mazingira yanayokubalika katika jamii ya wakati wake kwa sababu mazingira haya huwa halisi na yanayoaminika.

Kulingana na Qusby (1988), neno uhalisia lilitumiwa kwa mara ya kwanza huko Ufaransa katika miaka ya 1850, ili kuelezea kazi za sanaa zilizojikita katika kuusawiri ulimwengu kama ulivyo wala sio kama unavyofikiriwa katika nyakati mbalimbali.

Uhalisia hujaribu uwezavyo kuonyesha maisha kama yenye thamani. Kulingana na uhalisia wa Ufaransa, McCommell (1997) anasema kazi halisi ya kihalisia hujaribu kuonyesha hali jinsi ilivyo. Neno uhalisia lina maana ya uhakika au ukweli wa mambo. Nadharia ya uhalisia hutumika sana katika kazi za fasihi.

Ntarangwi (2004) anasema imani ya mhalisia ni kwamba anafaa kuweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli na halisi. Mhakiki basi anafaa kutazama jinsi ukweli ulivodhihirishwa katika juhudi za mtunzi za kuchora hali halisi ya mambo katika wakati maalum, asawiri wahusika, matukio, mandhari yanayokubalika na jamii ya wakati wake.

Nadharia hii hutumika kuhifadhia sifa msingi za uhalisia. Kazi hizo za fasihi zinafaa kuonyesha hali halisi ya maisha katika jamii. Pia inahusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Lazima tutambue kwamba utanzu wa riwaya unaambatana na uhalisi kwa kiasi kikubwa hivi kwamba haiwezekani kuzungumzia riwaya bila ya kurejelea mawazo yanayohusishwa na uhalisia.

Riwaya ya upelelezi ni tukio la kipelelezi ambayo hutokea, watu hufanya makosa na kujaribu kuficha. Waandishi wa riwaya hizi huonyesha vile uhalifu hutokea ; Hufichua hivyo wao na huonyesha jinsi tunavyoweza kukomesha uovu huo. Katika kuangalia mihimili ya uhalisia tulizingatia sifa za riwaya ya upelelezi kama tukio la kihalisia. Hivyo tunaona vile Mtobwa huonyesha njia kabambe za kukabiliana na maovu.

Mihimili ya uhalisia ni:

1. Ina wahusika wa kawaida na mandhari ya kawaida usimulizi wa kimuhakati (kusimulia matukio kama yalivyo katika ulimwengu halisi). Wahusika hao wa

kawaida katika riwaya ya upelelezi ni kama vile mhalifu, mpelelezi na watu wa kawaida. Wanacheza mchezo wa paka na panya huku mpelelezi anajaribu kunasa mhalifu.

2. Nadharia ya Uhalisia inaonyesha hali halisi ya kisaikolojia ya wahusika. Mbinu za uhakiki huzingatia muundo na muwala, uchambuzi na hali halisi ya wahusika. Kwa mujibu wa Wamitila mwandishi anafaa kuyaakisi maisha ya kijamii katika ngazi za maisha ya kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kisiasa. Mwandishi huangazia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake.

Mwandishi hutilia maanani mabadiliko ambayo kihistoria na jinsi ambavyo mabadiliko hayo husababisha hali mbalimbali. Kuna mahitaji fulani katika jamii ambayo hutokea katika jamii. Mauaji hutokea yanayotatanisha ambayo huonyesha wazi kwamba kuna binadamu anayesumbuliwa kisakolojia. Matukio haya hufanya jamii kuweka wahudumu fulani kama polisi kwa sababu wanaelewa kwamba kuna wahalifu. Ni lazima jamii itumie mikakati ya kuwanasa.

3. Mandhari na matukio yawe ni yale ambayo yanaweza kuonekana na kuwezekana. na matukio yawe yale ambayo yanalingana na jamii inayo rejelewa. Mwandishi wa kihalisia hutilia maanani mabadiliko ambayo yanatokea ili aweze kuwasawiri wahusika wake.

Mihimili hii imetuongoza kuangazia maovu ambayo hutokea katika jamii. Nadharia hii imefaa kuonyesha uovu unavyosawiriwa kimaadili, na pia jinsi maovu hayo hutendaka. Katika maisha kawaida huku tukitilia maanani kwamba fasihi ni kielelezo cha jamii ambapo inatupa mifano mahsusi yakukashifiwa na mingine ya kuigwa. Kuna uhalifu na pia kuna uwezekano wa kuyazuia. Riwaya ya upelelezi

huangazia mambo ya kusisimua yanayotokea hasa katika miji mikubwa kama vile: Nairobi, Johanesburg au Dar es Salaam.

Nadharia hizi mbili zimetufaa katika utafiti huu kwani, tumetumia nadharia ya uhalisia kutusaidia kueleza hali halisi, ilhali nadharia ya maadili ilishughulikia mtazamo wa mwandishi kuhusu uovu. Hivyo basi nadharia zote mbili zimechangia katika uhakiki wa kazi hii.

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI

### 1.9.0 Utangulizi

Katika sehemu hii, mbinu za utafiti ambazo zimetumika katika utafiti huu zimejadiliwa.

### 1.9.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu umefanywa kwa kuzingatia muundo wa kimaelezo, ambapo tumeelezea data ambazo zilikuwa zimekusanywa kutoka kwa riwaya teule za Kiswahili.

### 1.9.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu umefanywa maktabani kupitia usomaji katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta. Umelenga kupata data kutokana usomaji mpana wa riwaya mbili za Ben R. Mtobwa. Makala na machapisho yaliyoandikwa kuhusu mada kama vile tasnifu, majuzuu, vitabu na majarida yameshughulikiwa. Machapisho yote muhimu kuhusu utafiti huu yametumika. Aidha, maoni na ujumbe wa wataalamu wengine kupitia kwa tahakiki zao ulitambuliwa.

### 1.9.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli katika utafiti huu ni uovu unaojitokeza sana katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa. Hivyo basi, uteuzi wa sampuli uliofaa ni wa kimaksudi. Hii ni kwa sababu utafiti uililenga riwaya mbili za Ben R. Mtobwa ambazo ni*; Tutarudi na Roho Zetu* na *Salamu Kutoka Kuzimu.* Hadithi zinazopatikana katika riwaya hizi ni zile zinazogusia kiini, athari ya uovu na mikakati inayotumiwa kumaliza uovu huo. Isitoshe, uteuzi wa riwaya husika imeafiki kipindi cha maovu mengi ya kikatili yanayotokea katika jamii. Utafiti huu umetumia vifaa halisi kama vile picha zinazoonyesha maisha ya miji hasa yenye kudhihiri uovu. Mtafiti alisoma riwaya hizi kwa kina ili kupata data faafu kwa utafiti wake.

### 1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Mbinu ambayo imetumika katika ukusanyaji wa data katika utafiti huu ni usomaji wa riwaya mbili za Ben R. Mtobwa, majarida na machapisho yalioandikwa kuhusiana na mada ya utafiti. Aidha, tulisoma vitabu vya wataaamu mbalimbali vinavyotaja mambo ya uovu ili kupata uelewa zaidi kuhusu dhana hiyo. Tasnifu zilizoweza kutusaidia katika hoja ya utafiti pia zilipitiwa tuliongozwa hasa na malengo ya utafiti katika ukusanyaji wa data. Malengo yalituongoza kuyaainisha maswala yanayoshughulikiwa na waandishi wa riwaya zilizoteuliwa. Kudhihirisha kuwa uovu una kiini chake na athari zake kwa wanajamii. Aidha mwandishi Ben R. Mtobwa anaweka wazi mtazamo wake kuhusu mikakati ya kumaliza uovu. Dhamira yake katika hadithi hizo zilionyesha wazi namna mazingira huathiri utunzi wake.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Data imekusanywa kwa kunukuu katika madaftari na ikachanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Katika kufanya hivyo mtafiti alitafuta data

inayohusiana na malengo ya utafiti wenye vipengele vikuu vifuatavyo: kiini cha uovu, athari ya uovu na hatua za kuepukana na uovu huo. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuangazia maswala ya uovu unaoangaziwa. Hivyo basi, utafiti huu umehusisha kuainisha na kuangazia uovu unaojitokeza katika riwaya za *Tutarudi Na Roho Zetu* na *Salamu Kutoka Kuzimu* kwa kuongozwa na nadharia na malengo ya utafiti.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa matokeo

Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo na utoaji mifano mahsusi kwa kuzingatia sura mbalimbali. Maelezo haya yamefafanua uovu kama swala kuu katika riwaya za Ben R. Mtobwa. Uovu ambao tumeangazia zaidi ni mauaji ya kikatili ambayo yanajitokeza sana katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa. Mtafiti amefafanua kiini cha mauaji hayo, athari na mikakati inayotumika kukabiliana na swala hili la uovu. Uwasilishaji wa data umefanywa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia teule.

### Hitimisho

Yaliyoshughulikiwa katika sura hii ni masuala ya kimsingi katika utafiti ambayo ni usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, maswali ya utafiti malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti zilizohusisha eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data. Sura ifuatayo imeshughulikia historia na wasifu wa mwandishi kwa lengo la kutupa uelewa kuhusu mazingira ya mwandishi na jinsi yalivyo athiri kazi zake. Maoni mbalimbali ya wataalamu kuhusu uovu, na mtazamo wa mwandishi kuhusu uovu katika riwaya teule.

# SURA YA PILI

# HISTORIA YA MWANDISHI, DHANA YA UOVU NA AINA ZA UOVU

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia maisha ya Ben R. Mtobwa ambaye ni mtunzi wa riwaya pendwa za upelelezi katika eneo la Afrika Mashariki kwa kufafanua wasifu na historia, usuli pamoja na kazi zake. Yeye ndiye mtunzi wa riwaya za Kiswahili zilizoshughulikiwa katika utafiti huu ambazo ni *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984) na *Tutarudi na Roho Zetu* (1987). Kwa mujibu wa Madumulla (2009:71), riwaya pendwa ni riwaya ambayo inajihusisha na masuala ya mapenzi, uhalifu, ujasusi, upelelezi, burudani na kwa kiasi fulani maadili.

Kwa mujibu wa Wellek na Warren (1973), sababu kuu ya kazi yoyote kuwepo ni muumbaji wa kazi hiyo. Kwa maoni yao, hii ni njia mwafaka zaidi ya kuhakiki kazi za kisanii. Wasifu wa msanii wa kazi ya fasihi ni muhimu kwa sababu huangazia msanii na tajriba zake. Hivyo basi hurahisisha uhakiki wa kazi yoyote ya fasihi, hasa riwaya. Wellek na Warren wanaendelea kusema kuwa, kuelewa historia na maisha ya msanii hurahisisha hali ya kueleza mchakato wa kufahamu kazi zake. Uhakiki wa aina hii hutoa nafasi nzuri ya kuzingatia kazi hiyo katika muktadha wa mtunzi.

Kulingana na Keesey (1997) katika kitabu chake the *Contexts For Criticism,* wasifu wa mwandishi yeyote unafaa usomwe ili kusaidia kumfahamu mwandishi pamoja na kazi zake. Kwa maoni yake, mwandishi ni zao la wakati, kwa hivyo, ujuzi wake wakati wote unapaswa kujulikana ili usaidie katika kumuelewa mwandishi aliyehusika katika mikondo ya kijamii, kitaaluma na kisiasa. Kwa mujibu wa maelezo

haya, utafiti huu ulishughulikia maisha ya mwandishi na taaluma yake kiwakati kwa sababu ujuzi wa kipindi chote ulidhaniwa kuwa muhimu katika kuzifahamu kazi zake.

Hirsch (1960) anazungumzia umuhimu wa muktadha wa mtunzi katika ufahamu wa kazi yoyote ya fasihi. Hivyo basi, ni muhimu katika kuelewa kusudi la mwandishi na kufahamu muktadha wa kazi yake. Mtaalamu huyu anapendekeza kuwa njia bora zaidi ya kuelewa kile mwandishi alikusudia kueleza, ni kupitia uelewa wa muktadha wa kazi ya mwandishi huyo. Utafiti huu ulibaini kwamba Ben R. Mtobwa alizingatia zaidi muktadha wa miji mikubwa hasa Dar es Salaam mbali na kuwa aliweka wazi mtazamo wake kuhusu kiini cha uovu. Hivyo basi utafiti ulizingatia historia yake ili kupata uelewa zaidi kuhusu mchango wa sanaa katika kukosoa jamii husika.

### 2.1 Historia na maisha ya Ben R. Mtobwa

Gromov (2008) anaelezea kwamba mwandishi huyu anajulikana kama Benard Rashid Mtobwa. Alikuwa mwana wa Rebeka Ibrahimu. Mtobwa alizaliwa mnamo tarehe 28, Agosti, mwaka wa 1958 katika kijiji cha Ujiji, mkoa wa Kigoma, Magharibi mwa Tanzania. Mtobwa alikuwa mtoto wa pili katika jamii ya watoto saba. Kwa mujibu wa barua pepe ambayo mtafiti alipokea kutoka kwa Reystuta Mtobwa ambaye ni bintiye Ben R. Mtobwa (25/4/2015), Mtobwa alilelewa Kigoma, vijijini Mgambo, kijiji cha Muhingu. Alikuwa na mke na watoto saba. Ben R. Mtobwa katika kipindi cha utoto wake alikuwa mkarimu na mwenye kuwajibika. Kulingana na Reystuta Mtobwa, alipokuwa mtoto wa miaka kumi na mitatu, Mtobwa aliweza kumwokoa kijana mmoja kutoka ziwa la Tanganyika. Ben R. Mtobwa kuanzia makuzi yake, hakuwa mtu wa kuongea sana. Alikuwa mtu aliyependa kuingiliana na watu, mkarimu na asiyependa dhuluma au uonevu. Kutokana na mazungumzo yangu na Bw. Edmund Ogalo ambaye ni mhadhiri katika chuo kikuu cha Dar es Salaam, Mtobwa alijulikana

sana kwa lakabu ‘Joram Kiango’ ambaye ni mhusika mkuu katika riwaya zake za upelelezi (27/4/2015). Alipenda sana kusoma vitabu na hata kuandika. Ben Mtobwa aliaga dunia tarehe tisa mwezi wa 11 mwaka wa 2008 akiwa na miaka hamsini. Alizikwa katika shamba lake kule Bunju-A mjini Dar es Salaam.

### 2.1.1 Tajriba na Sifa zake

Benard Rashid Mtobwa anajulikana kimaandishi kama Ben R. Mtobwa. Ben R. Mtobwa alianza kuandika akiwa katika kidato cha tatu, katika shule ya upili ya Dodoma. Kitabu chake cha kwanza kilikuwa *Nitakusubiri (1992).* Kitabu hiki kiliandikwa na kisha kuchapishwa mwaka wa 1992. Baadaye akaandika *Zawadi ya Ushindi* (1997) ambacho kilitumika sana Tanzania na wanafunzi wa kidato cha tatu na nne. Ben R. Mtobwa alianza masomo yake akiwa katika kijiji cha Muhingu kutoka darasa la kwanza hadi la nne. Baadaye akahamia katika shule ya msingi ya Karuta ambapo alisoma darasa la tano hadi la saba. Alisoma katika shule ya sekondari ya Dodoma katika kijiji cha Kondoa, nchini Tanzania, kutoka kidato cha kwanza hadi cha nne. Baadaye alisoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Aidha, alifanya kazi katika mkoa wa Arusha nchini Tanzania katika kiwanda cha nguo cha Tafrag Tanzania Limited. Alipandishwa cheo na kuwa muangalizi mkuu hapo Tafrag. Alipoacha kufanya kazi Tafrag, alishirikiana na rafiki yake kwa jina Mdoe kuanzisha gazeti la *Mwana Habari* kabla ya kuungana na rafiki yake mwingine ajulikanaye kama Kajubi Mukajanga kuanzisha gazeti lililoitwa *Wakati ni Huu*.

Ben R. Mtobwa aliendelea kuchapisha hadithi fupi na makala katika magazeti makuu yanayosifika nchini Tanzania. Hadithi zake za awali zilitokea katika magazeti mbalimbali nchini Tanzania, Kwa mfano: *Nchi Yetu, Bara Afrika na Kiongozi*. Kwa sababu ya ukosefu wa kampuni nyingi za uchapishaji hasa zile zilizokuwa tayari

kuchapisha riwaya pendwa, alianzisha kampuni yake binafsi ijulikanayo kama *Heko Publishers Ltd*. Kwanza, kampuni hiyo ilihusika na uchapishaji wa magazeti kama vile: *Heko pamoja* na *Kalulu*. Baadaye *Kalulu* ilibadilishwa na kuitwa jina la *Kabumbu.* Kampuni hiyo ilikuwa inachapisha vitabu vya aina nyingi zikiwemo riwaya.

Primorac na Gromov (2008) wanasema kwamba Ben R. Mtobwa alikuwa mwandishi mwenye tajriba pana katika miaka ya 1980. Alikuwa mkurugenzi mkuu wa kampuni ya uchapishaji ya *Heko* Dar es salaam, Tanzania. Alihudumu katika cheo hicho hadi alipoaga dunia mwaka wa 2008. Chini ya uongozi wake, *Heko,* ilipata umaarufu sana nchini Tanzania. Alianzisha mradi wa kutumia tuzo kuinua waandishi chipukizi. Utaratibu au mpango huu wa kuwapa moyo uliwapa motisha waandishi hao chipukizi, wachapishaji wa riwaya bunilizi, vitabu na magazeti ya kila wiki. Haya yote yalichangia pakubwa katika kuinua sanaa na upigaji picha za sinema nchini Tanzania.

Ben R. Mtobwa alishiriki katika kuandika vitabu vya hadithi za watoto kama vile: *Nitakusubiri, Nani kama Mimi, Kipofu Mwenye Miwani Myeusi, Mpishi Mwenye Kibyongo, Mwalimu Mwenye Mkono Wa Bandia,Cheka Kidogo Hellena, Vipaji vya Hellena.* Pia, alijaribu kuandika vitabu vya hadithi fupi kwa mfano kitabu chenye mada *Mwanaharamu.* Isitoshe, kuna vitabu vya shule alivyoandika kwa ajili ya shule za msingi kama vile Kusoma na Kuandika. Ben R. Mtobwa alishiriki katika kuandika makala katika gazeti la *Mfanyikazi* na *Uhuru.*

Mnamo mwaka wa 2008, Mtobwa aliweza kuhutubia hadhira katika kongamano la waandishi na wataalamu wa fasihi kule Uropa. Katika kongamano hilo, Mtobwa alitoa hotuba kwa ufasaha na kuwavutia sana waliohudhuria wakiwemo waandishi katika chuo kikuu cha Gutenberg, Mainz Ujerumani. Hadhira iliyohudhuria

kongamano hilo ilidhihirisha kwamba kazi zake zinaunganisha burudani pamoja na maswala ya kijamii. Alionyesha umahiri wake katika kuangazia maswala nyeti ya kisiasa yanayokumba Tanzania kwa njia ya kisanaa. Mtobwa anazungumzia wajibu wa mtu kwa jamii yake katika kushughulikia ufisadi wa askari. Kazi zake zilitajwa kuwa mfano mzuri wa kazi za upelelezi za Kiafrika zinazogusia maswala ya karne hii ya ishirini na moja.

Ben R. Mtobwa alipendwa sana Tanzania, Afrika Mashariki na kimataifa kiasi kwamba hata baada ya kifo chake walifanya makumbusho yake tarehe 8/11/2009. Mwandishi huyu analinganishwa na waandishi kama vile Cyprian Ekwensi ambaye pia alipendezwa sana na kazi zinazozungumzia maisha ya miji. Riwaya zake zilipendwa sana na watu wenye mapato ya kadri na ya chini kama vile vitabu vya kina David Maillu wa Kenya, D .O Fagunwa (na baadaye Kalu Okpi ) wa Nigeria, Osaro Kanadu na Ike Tandor wa Ghana, na Gromolemo Mokae wa Afrika Kusini ambao pia kazi zao zilipendwa na watu walioishi mashinani. Kwa mujibu wa mtandao, Raselebeli Khoteng anamlimbikizia sifa tele Ben R. Mtobwa na kusema kwamba alikuwa amezaliwa na kipawa cha uandishi. Anasema Ben R. Mtobwa alikuwa anapenda sana kuandika utadhani “aliumwa na kimelea cha uandishi”.

Riwaya zake zilianza na *Lazima Ufe Joram* (1983) hadi *Mtambo wa Mauti* (2004). Riwaya hizi zilisifika sana hapa Afrika Mashariki. Zingine zilitafsiriwa katika lugha ya Kiingereza. Hali hii ya kutafsiri riwaya iliziwezesha riwaya hizi kupata sura ya kimataifa. Kazi zake nyingi, zinashughulikia maisha ya kisasa. Usasa huu ndio unaofanya maudhui yake kuwa ya kihalisia zaidi.

Kampuni ya *Heko* chini ya uongozi wa Ben R. Mtobwa ilihusika na utoaji wa mikanda ya filamu ambayo ilitoa filamu kama vile *Ngoswa penzi kitovu cha Uzembe,*

*Oloiboni* na *Layoni.* Ben R. Mtobwa alikuwa mtayarishi mkuu wa filamu ya '*Ngome ya Mwana Mulundi'*. Filamu hii iliongozwa na Hammie Rajab. Baadaye wakatayarisha filamu nyingine ijulikanayo kama '*Lazima Ufe Joram'*.

Maisha ya kisasa katika miji ya Kiafrika yanajitokeza kuwa maudhui makuu katika tungo zake bunilizi ambapo Joram Kiango ametumika kama mhusika mkuu. Joram Kiango ni kijana mtanashati mwenye umbo na siha ambaye anatumia ujuzi wake kutatua maswala tata ya mauaji ya kikatili. Mauaji haya ni matukio yaliyokuwa yamewalemea hata askari wa ulinzi. Katika kazi zake nyingi hasa za upelelezi, Joram anashirikiana na wahusika wa kike ambao wanadhamiriwa kuwa wapelelezi wasaidizi na wenzi kikazi na wengine kimahaba. Joram anajitokeza kama mwenye kutoa suluhisho kwa kuwatia mtegoni wahalifu.

Ben R. Mtobwa alikuwa mhariri wa maandishi na hati za waanzilishi wa riwaya za upelelezi za Kiswahili hapa Afrika. Alifanya juhudi za kukosoa jamii kwa kutumia uhakiki wa kijamii kubadili riwaya pendwa na kuzitumia kuzidisha uelewa wa jamii hasa wasomi. Anatumia riwaya zake kufichua uzandiki na ufisadi katika jamii ya sasa. Ben R. Mtobwa anatumia aina hii ya fasihi si kwa lengo la kutumbuiza tu bali kufafanua na kuchambua matatizo ya kijamii. Mtazamo wa Ben R. Mtobwa unakubaliana na wa mhakiki Madumulla (2009:44) ambaye anaamini kwamba, riwaya hizi za upelelezi hulenga kufichua uozo wa kijamii huku akiwahimiza watu wawe na bidii ya kuzitalii na kuzielewa riwaya pendwa.

Katika mahojiano kati ya Mikhail Gromov (2008) na Ben R. Mtobwa kule Mainz Ujerumani, Mtobwa alimwambia kuwa mapenzi yake makuu ni kuandika. Inadhihirika wazi kwamba, alipenda sana kusoma riwaya pendwa alipokuwa kijana. Reystuta Mtobwa alimwelezea mtafiti kwamba Ben R. Mtobwa alikuwa mtu

aliyependa kutumia kalamu kujieleza bali siyo mdomo. Tabia yake ilikuwa tofauti na yale aliyoyaandika kiasi kwamba wengi walikuwa hawaamini kama yeye ndiye mwandishi wa riwaya zake. Alikuwa ni mtu mwenye marafiki wengi ulimwenguni. Mtobwa katika mazungumzo hayo alimuelezea Gromov kuwa aliathiriwa sana na waandishi kama vile Ngugi Wa Thiong'o. Mashabiki wa riwaya zake na hasa anaowalenga katika uandishi wake ni vijana. Ben R. Mtobwa anamuambia Gromov kwamba ataandika hadi mwisho wa dunia.

Ben R. Mtobwa ameandika riwaya tatu za kijamii ambazo ni: *Pesa Zako Zinanuka* (1984), *Zawadi ya Ushindi* (1992) na *Dar es salaam Usiku* (1998). Isitoshe, ameandika vitabu vya watoto, hadithi fupi, na vitabu visivyo bunilizi. Kabla hajaaga dunia, Mtobwa aliandika msururu wa Joram Kiango unaojulikana kama *Mikataba ya Kishetani* ambao ulikuwa unasubiri kuchapishwa. Kazi nyingi za mwandishi huyu ni za upelelezi. Riwaya zake zinazosifika sana ni kama vile: *Lazima Ufe Joram* (1983), *Dimbwi la Damu* (1984), *Tutarudi na Roho Zetu* (1987), *Ninajisikia Kuua Tena* (1995), *Joram Kiango Mikonono mwa Nunda (1986), Salamu Kutoka Kuzimu (1984) Malaika wa Shetani* (1988) *Roho ya Paka* (1996) na *Mtambo wa Mauti* (2004). Mtafiti alibaini kwamba uandishi wake wa magazeti ulimpa nafasi nzuri ya kutambua maovu yaliyotokea mijini. Hivyo basi, si ajabu alipata msukumo wa kuyashughulikia kisanaa ili kuitahadharisha jamii.

## 2.2 Dhana ya Uovu

### 2.2.0 Utangulizi

Riwaya za Mtobwa zinataja maovu kadha wa kadha kama vile mauaji ya kikatili, ubakaji unafiki, ufisadi, ukahaba na ulevi. Utafiti huu umebainisha na kujadili maana na aina mbalimbali za uovu huo ili kuziweka riwaya za Mtobwa katika mkabala wake.

### 2.2.1 Maana ya Uovu kulingana na wataalamu mbalimbali

Jumuia ya binadamu daima haikosi kuwa na matatizo ambayo huambatana na migongano mbalimbali. Imedhihirika waziwazi katika ulimwengu wa leo kwamba mambo yasiyo na maana yamepewa umuhimu kuliko maadili. Ni vyema kwa mwanadamu yeyote kuelewa maana ya uovu ikiwa anataka kuwajibika ipasavyo kwa kuwa mwema. Hatuwezi kujiamini kwamba tunaelewa maana hasa ya uovu. Kuna viwango kadhaa vya uovu kama vile: uovu kwa Mungu, uovu dhidi ya mtu binafsi, uovu kwa wengine na uovu wa kijinsia. Viwango hivi vyote vimesawiriwa katika riwaya za Ben R. Mtobwa.

Oruka (1990) anaeleza uovu kama hali ya kutokuwa na uadilifu. Uovu huhusishwa na matendo mabaya kama vile: ubaguzi, kuwaumiza au hata kuwadhulumu wengine kiasi cha kuwaathiri kisaikolojia. Ni uharibifu wenye nia ya kutia wengine machungu na mateso yasiyo na kifani. Uovu ni kufanya mambo kinyume na matarajio ya wanajamii. Maovu yanayozungumziwa na Oruka (1990) ni miongoni mwa yale Ben R. Mtobwa ameyaangazia katika riwaya zake. Kwa mfano katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu* (1987), ubaguzi wa rangi unawafanya watu wengi kupoteza maisha yao. Utafiti umebaini jinsi Joram alivyoathiriwa kisaikolojia na kifo cha Neema, msichana aliyekuwa mwenziwe kikazi.

Maovu anayozungumzia Mtobwa ni yale yanayoweza kumithilisha na uhalisia wa matukio katika jamii hasa anapoangazia mauaji ya kiholela kwa kutumia bomu zinazotegwa bila kutarajiwa na mtu yeyote. Vilevile, Petit (1962) anasema kuwa uovu ni maudhui yanayosawiriwa kuonyesha uhalisia wa jamii. Katika *Tutarudi na Roho Zetu* (1987), tukio hili linaweza kumithilishwa na tukio la West Gate nchini Kenya

(Septemba mwaka wa 2013). Mtafiti amegundua kwamba Ben R. Mtobwa analinganisha maisha ya wahusika katika riwaya zake na uhalisia wa maisha.

Asemavyo Cohen (2011), kisayansi, uovu unaweza kufafanuliwa kama ukosefu wa uwezo wa kuhisi maono ya mwingine, unaodhihirishwa na hali hasi ya mazingira (hali hiyo inaweza kutokana na wazazi au jamii) na kwa kiasi kidogo kinasaba. Hivyo basi, mtu kama huyo huenda anapotenda unyama, hufurahia huku wenzake wakiumia. Kwa mfano Proper, muuaji katika *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984) anafurahia sana anapomwoma Neema akiwa marehemu. Ben R. Mtobwa anamsawiri muuaji mkuu Von Iron kama kiumbe asiyehisi huruma kwa binadamu yeyote akifa, hasa mtu wa Kiafrika. Hii ni kwa sababu ya yale matukio aliyoyashuhudia akiwa mtoto. Ben Mtobwa anaangazia sana mauaji ya kikatili katika riwaya zake za upelelezi. Lewis (1978) katika kitabu chake *Abolition of Man* anadumisha dhana kwamba matendo mengine ambayo kilimwengu yanachukuliwa kuwa uovu ni kama mauaji na ubaguzi. Lewis (1978) anaendelea kusema kuwa, uadilifu ni utu. Utu ni maumbile na maumbile yanafaa kuwaongoza wanadamu bali si kuongozwa na mwanadamu. Kulingana na utafiti huu, Ben Mtobwa anamsawiri Joram kama mwanadamu anayeongozwa na utu kupinga uovu kwa kuwasaka wauaji wa kikatili. Joram anapojificha, inambidi kubadili hulka yake na hata kuingia miongoni mao bila kujali maisha yake binafsi. Kwa hivyo, anadhihirisha utu. Joram anapokutana ana kwa ana na mhusika Waridi, upole wake na uelewa unamfanya msichana yule kumweleza ukweli kuhusu mpango wa kumuua. Hata ingawa alikuwa ameahidiwa kifo na Proper, Waridi anamwona Joram kama mtu mwema asiyestahili kifo.

### 2.2.2 Wema na Uovu

Dhana ya wema na uovu inajitokeza katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa. Kulingana na Augustin (1955), uovu ni wazo la kawaida na la kudumu katika maisha ya mwanadamu. Uovu hauna uasilia chanya ila ukosefu wa wema hupewa jina uovu. Augustin (1955) anaamini kuwa uovu huumiza na kwa hivyo hali hiyo ndiyo huleta ukosefu wa wema. Uovu ni tendo la kuamua kutofanya mema. Uovu ni kama shimo ndani ya maadili mema. Uovu ni jambo la kawaida katika maisha ya wanadamu. Binadamu huibuka kuwa muovu kwa sababu ya kufanya maamuzi mabovu ya kimaadili. Proper, ndiye mhusika anayetambuliwa kama muuaji mkuu katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984). Yeye aliamua kuwa muovu na alifurahia kuwaona binadamu wenzake. Wahalifu wenzake wanapopinga mauaji ya wajumbe, yeye anaendelea na mpango huo kivyake.

Abraham (2005) anasema kwamba watu hutambua wema kwa kutumia vigezo vilivyowekwa kisheria, nao uovu hutambuliwa kwa kurejelea makataa ya sheria. Kwa kuwa sheria huongezeka mara kwa mara, watu hurejelea sheria hizo kuwaongoza katika shughuli za kimaadili. Maadili ni mambo ya kawaida maishani ambayo hupatikana kwa kila mwanadamu anayeishi katika mahusiano ya kibinafsi, kijamii, nchini na hata kimataifa. Ben R. Mtobwa anadhihirisha kuwa mauaji ya kikatili ni kinyume cha sheria, ndiposa tunaona askari katika pembe zote za nchi wakimsaka mhalifu katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984).

Katika kuonyesha wema ukishindana na uovu, Ben Mtobwa anampa msomaji nafasi ya kujiamulia njia bora ya kufuata maishani. Hili hutegemea jinsi ambavyo msomaji ameathiriwa. Kama anavyoashiria Burgess (2005), hatuwezi kuzuia mielekeo ya kimaadili kuingia katika ukadiriaji wa vitabu hata vile vizuri vya burudani. Marshall

Gregory katika George (2005) anasema kuwa ni jukumu la mhakiki kuchanganua hadithi na athari ya kimaadili dhidi ya msomaji wa hadithi. Anaamini kuwa bunilizi nyingi hudhihirisha maisha ya kawaida, yaani uhalisi wa maisha. Maisha ya kawaida huhitaji maamuzi mwafaka na kiwango cha maadili. Utafiti huu umeng'amua kwamba, mambo anayoyataja Ben Mtobwa ni changamoto katika maisha ya sasa.

Uovu ni dhana inayotawaliwa na mwanadamu. Tukizingatia riwaya za Ben R. Mtobwa tunaona kwamba, riwaya hizo zinasawiri uovu na wema. Uovu unaosimamiwa na muuaji wa kikatili Jodor Proper, na uadilifu unaosimamiwa na mpelelezi Joram Kiango anayejaribu kukomesha uovu huo. Knoll (2008) anasema kuwa uovu hauwezi ukaelezwa kisayansi. Kwake yeye, hii ni dhana ya kinjozi isiyo kuwa ya kiasilia. Wanadamu hushughulika sana na mambo ya uovu. Mambo ya uovu dhidi ya wema yamechukua nafasi ya kichochezi kikuu kwa mafanikio chanya ya wanadamu. Ni vyema kuelewa kwamba tunapotambua uovu, basi tunakuwa na nafasi nzuri ya kuepukana nao.

Kuna umuhimu wa kuelewa uovu ndiposa wema ueleweke dhahiri. Ingawa watu wengi huhusisha dhana hizi na mambo ya kidini, wasanii huyashughulikia kwa vile ni maswala ya kawaida katika maisha ya mwanadamu. Wahakiki kama vile Gregory (2005) wanasema kuwa tunaposoma riwaya bunilizi, tunazihakiki bila kutarajia na aghalabu ni wasomaji ndio huamua ni nani muovu na ni nani mwadilifu katika riwaya. Riwaya hizi za Mtobwa zinatusawiria maovu yaliyoko katika jamii, hivyo basi yeyote anayesoma riwaya hizo ana nafasi ya kuelewa maovu yale na kutafakari jinsi ya kuyaepuka.

Uovu na wema ni kama pande mbili za shilingi. Awdhesh (2014) anasema kwamba ujuzi wa wema na uovu ndiyo ujuzi wa uhalisia. Anaendelea kusisitiza kwamba watu

wenye hekima wameelewa kuwa wema na uovu ni pande mbili za shilingi Matendo hayo yanakaa tofauti mno, lakini yote hutendwa na mwanadamu. Mwanadamu anaweza kuwa mwema au muovu, hayo yatategemea uamuzi wake kuhusu maisha. Walimwengu mara nyingi hutarajia wenzao watende wema au uovu. Haya huonekana wazi hasa pale ambapo watu wema hulimbikiziwa sifa ilhali waovu wanakashifiwa. Kulingana na ploti ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984), Joram anapendwa na wengi kwa kupinga uhalifu na mauaji. Proper anachukiwa na kuwa windo la kila mtu. Gardener (2005) anasisitiza kuhusu maadili yanayotufaa na kutufanya kuhisi vibaya kuhusu upungufu wetu na matendo yetu mabaya. Kuna wakati wanadamu hujikuta wakitenda maovu wakiwa katika harakati ya kutenda wema. Awdhesh (2014) anatupa mfano wa vijana wa kisasa ambao hufanya kitendo fulani kufurahisha vijana wenzao, lakini baadaye hujikuta wametenda maovu.

### 2.2.3 Maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu uovu

Katika sehemu hii, utafiti huu umeshughulikia maoni mbalimbali kuhusu uovu ili kuielewa dhana ya uovu. Uovu ni jambo la kihalisia na njia bora zaidi ya kuchipuza na kuimarisha uadilifu ni kuelewa uovu. Uelewa huu uliweza kupatikana kwa kuchunguza maoni mbalimbali ya wataalamu. Wengi wametoa maoni yao kuhusu dhana hii ya uovu hasa katika fasihi kwa jumla. Wamezungumzia umuhimu wa kushughulikia mambo haya katika fasihi ili kuwajuza wanajamii matukio yanayoenda kinyume na matarajio yao.

Jenkins (1994) ameandika kuhusu ujumuishaji wa maudhui ya mauaji katika riwaya pendwa. Mtaalamu huyu anasema kuwa mauaji ya kikatili ni aina ya uhalifu ambao hushughulikiwa katika riwaya nyingi hasa za upelelezi. Kule Ulaya vitabu hivi vya upelelezi vilichapishwa vingi kwa mwaka mmoja. Vilichapishwa zaidi katika kipindi

cha miaka mitatu yaani 1991 hadi mwaka wa 1993, kuliko mwaka wa 1960 hadi 1970. Vitabu hivi vilikuwa vya fasihi bunilizi na vilizungumzia uhalifu halisi. Uovu kama vile mauaji ya kikatili ni swala ambalo hujadiliwa sana katika vyombo vya habari. Kilele cha uandishi wa Ben R.Mtobwa kilisifika zaidi katika miaka ya 1990. Ndiposa tunaona kwamba Ben R. Mtobwa anaangazia sana mauaji katika riwaya zake, kwa sababu ni swala ambalo limeleta changamoto nyingi tangu wakati huo hadi sasa.

Kulingana na Kahn (1953) thamani ya vitabu haiwezi kueleweka ila tu iwekwe katika mfumo wa wema na uovu. Swala kuu katika maisha ya mwanadamu ni wema na uovu ambao hutawala. Mtazamo huu umefuatwa sana na Ben R. Mtobwa ambapo tunaona mhalifu akiwaua watu kikatili huku mpelelezi na askari wakimtafuta ili kukomesha uhalifu huo. Hii ndiyo maana riwaya hizo zinaeleweka haraka hata na watu wenye elimu ndogo.

Kukosa uadilifu ni ishara tosha au msingi wa kuelewa uovu. Hii ni kwa sababu watendaji maovu hayo husababisha madhara ya kudumu; yaani madhara ya kimaadili kwa mhasiriwa. Lara (2007) anasema kuwa matendo ya uovu lazima yajikite kwenye matukio na athari ya uovu huo kwa watu. Yote hayo yanachangia mtazamo muhimu kuhusu jinsi ya kutambua uovu unaotendwa. Iwapo utafiti huu utashughulikia mtazamo mmoja, basi utakuwa unadhoofisha uelewa wa maingiliano kati ya muovu na mhasiriwa na maana maalum ambayo matendo hayo hutuletea. Haya hutendeka tunapokuwa tunakadiria madhara ya kimaadili ya kudumu katika maisha ya mwanadamu. Imani yake ni kwamba, kukosa uadilifu katika kazi za fasihi ni muundo msingi wa kuelewa uovu kwa vile waovu husababisha madhara ya kudumu kwa wahasiriwa. Lara (2007) anaamini kwamba fasihi imechukua nafasi kubwa sana

katika uelewa wa uovu kwa kuelezea uchangamano katika hadithi hizo. Riwaya za upelelezi za Mtobwa zimechukua nafasi nzuri ya kutumia fasihi, kudhihiri uovu, hasa kiini chake na athari zake.

Kwa mujibu wa Zimbardo katika Miller (2004), uovu huweza kufasiriwa kama tabia isiyotarajiwa au inayowafanya wengine kutenda matendo yasiyodhihirisha utu, matendo ya uharibifu, kudhuru au hata kuua watu wasiokuwa na hatia. Zimbardo ana maoni kwamba uovu hujumuisha mambo ya kisasa kama vile: ugaidi, mateso, vita na uangamizaji wa kikabila. Utafiti huu umebaini kwamba, Ben Mtobwa ameangazia ugaidi na uangamizaji wa kikabila hasa ubaguzi wa rangi katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu* (1987). Mhusika Von Iron anapata fahari kuu kuwaua watu weusi. Zimbardo anawachanganua watu wanaoepukana na uovu kama mashujaa.

Aghalabu uovu huingia duniani bila kutarajiwa ndio maana watu waovu mara nyingi hawatambuliwi haraka. Baumeister (1997) anasema kuwa uovu huingia ulimwenguni bila kutambuliwa au kutarajiwa. Wale wanaotenda uovu huwa hawaoni kuwa wanawadhulumu wenzao. Kwao, hii ni njia moja ya kutosheleza nafsi zao. Wauaji wa aina hii ndiyo wanaoshughulikiwa na Ben Mtobwa. Jodor Proper ambaye ni muuaji katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984) anasawiriwa kama binadamu anayepata furaha nyingi sana anapowatoa wenzake uhai. Kila anapoenda, watu wengi hawatambui kwamba ni muovu.

Aidha, inafaa kueleweka kwamba uovu hutokea na mara nyingi hubishana na maadili mema. Mahali popote ambapo uovu hujitokeza huwa pana uhusiano kati ya wema na uovu. Huwa kuna ushindani kuhusu jinsi ambavyo wema unaweza kutawala uovu. Kulingana Shollom J. (1953), shida kuu ya mwanadamu ni wema na uovu. Hii ni kwa sababu vitabu ambavyo husomwa na kuandikwa huhusika kwa njia moja au nyingine

na shida zinazomkabili mwanadamu. Hii ndiyo maana riwaya za Mtobwa hupendwa na wengi kwa kuwa ni rahisi kuelewa.

Uovu hutendeka siyo kwa sababu kuna thamani mbaya bali kwa sababu kuna thamani ambazo hufaa kuhusishwa na wanadamu. Falsafa hii ni hali ya kulinganisha thamani yenye uzuri na ukosefu wa wema. Uovu hutokana na hali ya ubinafsi, na unafaa kueleweka kama hali ya kukosa kuingiliana vyema na binadamu wengine. Ben R. Mtobwa anausawiri uovu ukivutana na wema na hivyo anampa msomaji nafasi nzuri ya kujiamulia njia ambayo angependa kufuata. Mwandishi anafanya hivyo kwa kuangazia sababu na athari ya maovu hayo.

Kuna maovu yanayosawiri unyama wa kiwango cha juu zaidi. Uovu kama mauaji yanayofanywa na Proper, yanawaacha wengi vinywa wazi. Rana (1999) anawataja Eric Fromm na wenzake wenye imani kwamba kuna tabia za kibinadamu ambazo ni za kawaida na mengine yanayodhihirisha wazimu. Mfano mzuri ni mauaji ya kikatili kama yale yanayofanywa na Proper katika *Salamu Kutoka Kuzimu.* Kuwakata binadamu katika vipande kama nyama si jambo la kawaida. Wanadamu ni viumbe wa kijamii kwa hivyo wale wanaoua, kunajisi na kuiba huvunja utaratibu huu asilia wa kimaadili. Vivyo hivyo, Ben Mtobwa anayasawiri maovu hayo kama mambo yanayomfanya mwanadamu kukosa amani na uadilifu katika mazingira yake halisi. Anataja wahusika wengine wauaji kama viumbe wenye kukosa utu na wenye kichaa kiasi cha kufurahia mauaji hayo. Katika *Mtambo Wa Mauti (2004:196)*, mhusika Christopher Marlone ambaye raha yake ni kuua na kubaka, anamnajisi binti yake, mtoto ambaye anastahili kumuita baba. Mtu huyu anasawiriwa na Ben R. Mtobwa kama mtu mwenye kichaa cha shetani kwani furaha yake kuu ni kuwatoa wenzake uhai.

### 2.2.4 Aina za uovu

Wataalamu wana imani kwamba kuna mifano mbalimbali ya uovu na aina za uovu. Wanafalsafa wengi wanajumuisha uovu kwa makundi mawili: Uovu unaokiuka maadili na ule wa kimaumbile. Uovu unaokiuka maadili ni aina ya uovu ambao hutendwa kwa kusudi la kuwaumiza watu. Mifano ya maovu haya ni ukatili, mauaji, ubaguzi na utumwa. Uovu wa kimaumbile ni ule ambao hutokea bila kukusudiwa kama vile: kupigwa na radi, mafuriko, zilizala na magojwa yasiyotibika.

Wataalamu wengine wanaozungumzia aina za uovu ni pamoja na Augustin, Lars Svendsen na wengine. Kulingana na Augustin (1955) kuna aina tatu za uovu: Mtu binafsi atendaye uovu, jamii itendayo maovu (Kwa hiari au bila kupenda) na uharibifu wa maumbile ambayo hutendeka bila hiari ya mwanadamu. Aina ya uovu wa kwanza na wa pili huchukuliwa kama maovu ya kimaadili ambayo yanajitokeza katika riwaya za Ben Mtobwa. Utafiti huu ulishughulikia mtu binafsi atendaye uovu katika riwaya teule. Katika kikundi hiki pana mkosaji anayeasi dhidi ya maadili au utaratibu wa jamii. Mhalifu huyu hufanya kitendo kinacholeta madhara, mateso au uchungu kwa wanajamii. Mara nyingi utakuta kwamba tendo linalofanywa na mhalifu kwa makusudi huenda likawa na madhara yasiyokusudiwa.

Lars Svendsen (2010) katika kitabu chake cha *Philosophy of Evil* anasema uovu ni swala thabiti la kimaadili na halifai kuhalalishwa. Kwa maoni ya Svendsen (2010), uovu ni kipengele cha kawaida katika maisha ya sasa. Uovu huhusishwa hasa na utendaji wa kimaadili na kisiasa. Maoni yake ni kwamba uovu unafaa ukomeshwe. Svendsen anatambua aina nne za maovu. Kwanza kuna: Uovu unaohalalishwa na sababu fulani kuu. Huu ni uovu unaofanyika ili kutimiza lengo lingine tofauti. Kwa mfano mafuta yakimwagika katika bahari kule Mexico huweza kusababisha uwepo

wa chembechembe za sumu ambazo ni hatari kwa maisha ya wanadamu. Aina ya pili ya uovu ni ule uovu wa kijinga. Uovu wa kijinga unaotokea kwa sababu ya kukosa ustadi. Mfano mzuri ni ajali ya ndege kwa kosa ambalo rubani angetatua.

Katika kazi za Ben Mtobwa zilizoshughulikia, kuna aina mbili ya maovu yaliyojitokeza zaidi. Maovu haya yanatajwa na Svendsen (2010) kuwa uovu wa kidhahania: Uovu wa kidhahania ni uovu unaotendwa kwa kuhalalishwa na lengo fulani la mhalifu. Svendsven (2010) anatoa mifano ya watu kama Adolf Hitler, mwenyekiti Mao na hata Osama Bin Laden waliopewa motisha na kile ambacho waliamini kuwa ni lengo muhimu sana. Svendsen (2010) ana maoni kwamba wahalifu hao wanapotenda uovu hufurahia sana, wakiuua. Hivyo basi kulingana na mtu kama huyo, hatendi uovu tu kwa lengo la kutenda uovu, bali kwake yeye ni wema. Mhalifu wa aina hii tunaweza kusema kwamba alikuwa na tabia za kinyama. Kwa kuwa hata mwendawazimu anapovua nguo huona akiwa sawa, binadamu hawa huchukuliwa kama watu waliopagawa. Utafiti wetu ulilenga sana uovu wa kishetani na kidhahania. Katika riwaya za *Salamu Kutoka Kuzimu* na *Tutarudi na Roho Zetu*, wauaji waliuua kikatili kutimiza malengo hayo mawili. Kulingana nao, kuua ni kama aina ya mchezo.

Uovu wa pili anaozungumzia Svendsen (2010) ni uovu wa kishetani. Uovu huu wa kishetani ingawa unahusishwa na mambo ya dini, ni uovu unaotendwa kwa lengo la kuwaumiza wengine. Wakati mwingine ni hali ya kuwafurahia wengine wakiteseka. Mhalifu ambaye huwaua watu kwa msururu ambaye amezoea kuwatesa wahasiriwa ni mfano mzuri wa uovu wa aina hii. Uovu wa kishetani ndiyo uliyoshughulikiwa kwa kuwa riwaya za Ben Mtobwa zimewataja wahusika wa aina hiyo. Mfano mzuri ni mhusika Jodor Proper.

#### 2.2.4.1 Mauaji ya kikatili kama aina ya uovu.

Mtafiti anaangazia zaidi mauaji ya kikatili kati ya maovu mengine yanayoshughulikiwa na Ben R. Mtobwa. Reamer (2005) anasema kuwa kuua ni tendo la kutoa uhai wa mwanadamu kwa njia ya kusudi. Kulingana na utafiti huu, mauaji ya kikatili yana maana ya mauaji ambayo ni ya kinyama zaidi. Reamer (2005) anataja aina nne za mauaji ambayo husawiriwa katika riwaya: mauaji ya kijumla, mauaji ya mwenzi, mauaji ya mfululizo na mauaji ya kijinsia. Utafiti huu umelenga zaidi mauaji ya kijumla na ya kijinsia kwa kuwa ndiyo yanayoangaziwa sana katika kazi za Mtobwa.

Wataalamu wengine wana maoni tofauti kuhusu maana ya mauaji. Shengold (1989) anasema kuwa mbali na kutolewa uhai, pia kuna kifo cha kinafsia. Anaamini kuwa tendo kama la kumdhulumu mtoto ni kama kumnyima furaha maishani. Mateso ya kisaikolojia ambayo hujitokeza zaidi katika utu uzima huwa ni matokeo ya mambo yaliyoshuhudiwa utotoni na mhalifu. Mawazo haya yanakubaliana na yale ya Rousseau (1778) ambaye anasema kuwa  alizoea kuchapwa na yaya hadi akawa anatamani amchape kila wakati. Anaamini kwamba watoto waliokua katika mazingira ya kuteswa huwa waovu wanapokuwa watu wazima. Wao hukisiwa kuwa na chuki nyingi sana maishani.  Kumdhulumu mtu hadi ajione kama kiumbe duni humwacha na kidonda au pengo fulani ambalo hujaribu kuzibwa kwa njia zozote zile. Mateso hayo hudhuru nafsi ya mtu kiasi kwamba yeye hukosa matumaini katika maisha yake ya usoni na hatimaye kumfanya kuwa mtu mtundu sana. Vilevile, Ben R.Mtobwa anawasawiri wahusika wake wahalifu kama watu waliochochewa na mazingira wakiwa watoto na baadaye kuwa na tabia za kinyama katika utu uzima wao. Hali hii inawafanya waathiriwe kisaikolojia na hivyo kuwa waovu mno wakiwa watu wazima.

Utafiti huu umeshughulikia mauaji ya mfululizo ambapo mtu mmoja anawaua watu kwa malengo yake mwenyewe. Sababu za mauaji haya, athari na mapendekezo kuhusu uovu huu na mbinu za upelelezi anazotumia mpelelezi kuwanasa wahalifu zimechunguzwa. Vipo vifo vingi vilivyotokea kwa njia za kikatili na za ajabu lakini polisi wanashindwa kumpata mtu wa kumhusisha na mauaji hayo. Hata hivyo, mpelelezi anadakia nafasi hiyo kwa lengo la kujaribu kuukomesha uovu huo kwa lengo la kutaka kuleta amani katika jamii husika.

### 2.3 Mawazo ya Ben Mtobwa katika riwaya zake

Ben R. Mtobwa katika riwaya zake anaonyesha jinsi ulimwengu ulivyotawaliwa na uhalisi wa unafiki, ufidhuli na ukosefu wa utu ambao umewachochea wahasiriwa kuwa na nyoyo za kinyama. Unyama huu unawaathiri binadamu wenzake kwa njia hasi. Uteuzi wake wa taswira unatoa picha kamili ya changamoto kuhusu maisha asilia ya kisasa kwani anaonyesha namna uasilia na mazingira yalivyo vichochezi vikuu vya uovu.

Mwandishi amewasawiri wale warembo wa ukahaba kama watu walioathiriwa na mazingira walimolelewa. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984), Waridi alilelewa katika madanguro ambapo mbali na kuyashuhudia yale mamake alitendewa na wanaume, yeye mwenyewe alibakwa. Msichana huyo aliienzi kazi ile tangu akiwa na umri wa miaka kumi na miwili. Baadaye anahitimu kuwa mtaalamu wa kazi hiyo ya ukahaba. Alikuwa na chuki kwa wanaume kiasi cha kutompenda hata mmoja wao. Aliwaona kama binadamu waliomtumia tu ili kujinufaisha na mwili wake. Aliishia kumuua mwanaume mmoja na kutafuta nyumba katika madanguro ya kufanyia kazi ile aliyodhani ndiyo njia ya pekee ya kupata riziki.

Riwaya ya *Mtambo Wa Mauti* (2004) ina mhusika mkuu Mona Lisa au Margareth anayegeuka kuwa muuaji hatari wa watu. Kwa mtazamo wa mwandishi, Monalisa pia anaonekana kuchochewa na mazingira yanayomfanya kuwa mwenye roho ya kikatili na mhalifu. Mamake anauawa akiwa angali mwenye umri mdogo sana. Aidha, Mona Lisa anabakwa na mtu aliyemwaminia kuwa baba mlezi kwake. Vilevile, dadake ambaye ndiye jamaa yake wa pekee anauawa kinyama. Ukatili unamzonga Margareth anapokuwa mtu mzima. Binadamu aliyeishi naye kwa jina Morlene Johnson, ni mtu ambaye mipango yake yote ilikuwa ni mauaji na uangamizaji wa watu. Hivyo basi, Mona Lisa anajipata akiwa amefuzu kuwa mtaalamu wa mauaji.

Katika *Dar es Salaam Usiku* (1994), msichana ambaye ndiye mhusika mkuu, Nuru, anaibuka kuwa hawara na mnafiki kutokana na mazingira yake ya malezi. Nuru alilelewa katika madanguro licha ya kubakwa akiwa mtoto wa miaka kumi na mitatu. Mamake mzazi alimwambia akiwa kigoli kwamba alikuwa na damu moto. Hivyo basi, aliweza kutumia mwili wake kujipatia riziki. Hii ina maana kwamba alimrithisha ukahaba ambao aliamini ulikuwa wa kiasilia. Isitoshe, utafiti ulibaini kuwa hata nyanyake Nuru mzaa mama pia alizaa nje ya ndoa. Kwa hivyo ni tabia ya kiasilia. Utafiti huu umebaini kwamba maovu yanayoshuhudiwa na Nuru akiwa mtoto pamoja na uasilia wake yanachangia kumfanya muovu.

Muuaji mkuu katika *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984) ajulikanaye kama Proper alikuwa ameteswa sana na mabaharia akiwa mvulana mdogo wakati alipotoroka kwao. Baadaye anakuwa katili sugu anayechinja watu bila kujali. Ukatili huu uliweza kulinganishwa na yale aliyoshuhudia pamoja na chuki aliyokuwa nayo dhidi ya wanadamu wengine. Mawazo haya pia yanarudiwa katika *Tutarudi na Roho Zetu* (1987) ambapo mhusika mkuu Von anafurahia mauaji ya wanadamu kuliko mchezo

mwingine. Hili linatokana na hali kwamba yeye mwenyewe alishuhudia mamake akiuawa na babake ambaye baadaye alijitoa uhai. Isitoshe, alishuhudia Waafrika wakiteswa alipokuwa mtoto na hivyo basi akawa mbaguzi mbaya sana wa rangi kuwaliko makaburu wenzake.

Kinadharia sehemu hii imejaliza mhimili wa nadharia ya maadili inayosema kwamba kazi ya fasihi ni kielelezo cha jamii. Imeshughulikia maovu yaliyopo kwa upana na hivyo kuielekeza kwenye wema. Kwa jumla, utafiti huu umeweka wazi dhana ya uovu kwa kuzingatia riwaya teule za Ben Mtobwa. Kuangazia uovu katika riwaya zake teule ni njia moja ya kuongoza jamii kwenye maadili yaliyolengwa.

**Hitimisho**

Sura imeshughulikia kwa kina historia na tajriba ya mwandishi Ben Mtobwa, dhana ya uovu kulingana na wataalamu mbalimbali, maana ya uovu, uovu na wema na mawazo ya Ben Mtobwa katika riwaya zake. Kutokana na maelezo ya sura hii ni wazi kwamba uovu na maadili ni kama pande mbili ya shilingi. Hatuwezi kuelewa uadilifu au wema bila kuelewa uovu unaostahili kuepukwa na wanajamii. Utafiti wetu umebaini kwamba Mtobwa alikuwa ni mtu asiyependa dhuluma na huenda hisia hizo zilimchochea kuandika riwaya za upelelezi. Kwa kuandika riwaya hizo, mwandishi anapata nafasi nzuri ya kutoa taswira ya uovu unaokera jamii na kuelezea mbinu zinazoweza kutumika kuumaliza uhalifu katika jamii. Aidha, tajriba yake ya kuandika magazeti huenda ilimpa nafasi nzuri ya kuyaelewa maovu yaliyotokea katika miji mikuu kama vile Dar es Salaam.

Ni dhahiri kwamba Ben R. Mtobwa anayaangazia maovu mengi katika jamii yakiwemo mauaji. Utafiti huu umebaini kuwa mwandishi wa riwaya teule

anayasawiri mazingira kama kichochezi kikuu cha tabia za binadamu. Mbali na mawazo hayo kuhusu kiini kikuu cha uovu, utafiti huu pia umebaini kwamba uovu upo na ni lazima upingwe kwa vyovyote vile. Waovu hao ni lazima waadhibiwe ili kuridhishia jamii ya mhasiriwa ihisi kwamba haki imetendeka Cohen (2012*).* Wapelelezi wa kujitolea, askari pamoja na wananchi wenye nia njema wanaupinga uovu huu na kudhihirisha wema. Sura inayofuata inahusu mikakati inayotumiwa na Ben R. Mtobwa kupigana na uovu.

# SURA YA TATU

# MAUAJI, ATHARI ZAKE NA MIKAKATI YA KUSHINDA UOVU KATIKA RIWAYA YA *SALAMU KUTOKA KUZIMU*

## 3.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu utafiti huu umezungumzia muhtasari wa hadithi, kiini cha maovu, athari ya uovu na mbinu za upelelezi anazotumia Mtobwa kukabiliana na uovu huo katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984). Haya yote yameshughulikiwa kwa kuzingatia mtazamo wa Ben R. Mtobwa ambaye ni mwandishi wa riwaya teule.

Kwa jumla utafiti huu umeainisha maovu yanayoangaziwa katika riwaya teule na mazingira kama kiini kikuu cha uovu katika jamii. Maovu yanayoangaziwa katika riwaya hii ni kama vile ukahaba, ulevi, ubakaji, unafiki na mauaji ya kikatili ambayo tumeangazia zaidi.

**Muhtasari wa riwaya ya Salamu Kutoka Kuzimu**

*Salamu Kutoka Kuzimu* (1984) ni riwaya yenye sura kumi na mbili. Riwaya hii ni ya kipelelezi na imezungumzia maudhui ya uovu. Anayepanga mauaji na kuua kwa njia ya kikatili ni mhusika ajulikanaye kama Jodor Proper. Mpelelezi mkuu anayewasaidia polisi kupigana na uhalifu mjini Dar es Salaam anajulikana kama Joram Kiango. Mauaji yanayotokea yanawaacha watu wengi vinywa wazi na kuhatarisha maisha ya mpelelezi.

Hadithi inaanza wajumbe wakiwa katika mkutano wao wa siri chini ya uwenyekiti wa Proper. Wajumbe hawa wanafanya mpango maalum wa kumuangamiza Joram ambaye wanamwona kuwa kizingiti katika mipango yao. Wahalifu hao wana nyadhifa

na heshima serikalini. Hivyo basi, wote wanaelewana kwa kauli moja kuwa ni lazima wamuue Joram Kiango. Mwenyekiti anapinga kauli kwamba Joram auawe kwa njia ya kisayansi, ndipo waendelee na mipango yao ya kuwaua watu.

Waridi anayeishi Mburahati kijiji kimoja cha mabanda jijini Dar es salaam alikuwa ameguria kijijini humo baada ya kifo cha rafikiye Bomba ambaye alimuua kwa mikono yake mwenyewe. Siku moja anampata mteja wa ajabu anayemlazimisha kwenda kumuua Joram la sivyo atambue siri yake kuhusu kifo cha Bomba. Sura hii inatuangazia kuhusu historia ya Proper na mazingira yalivyomuathiri. Hapa ndipo tunaelezwa kwamba Waridi mwenyewe alikuwa mtoto wa malaya na wanaume walianza kumtumia kwa njia hiyo tangu akiwa mtoto wa miaka kumi na miwili. Kwanza, Proper anamnajisi na kumpiga kinyama kabla ya kumpeleka mahali anapostahili kutimiza tendo la kumuua Joram.

Joram na msaidizi wake Neema wanapokuwa wanafanya mazungumzo katika baa fulani, kunatokea kilio cha kusikitisha nje ya baa hiyo na wanapotoka wanampata mwanamke ambaye alikuwa nusu uchi akilia kwa uchungu. Kando yake kuna kisu kirefu na damu iliyomwagika. Upelelezi unaanzia hapo huku Joram akishangazwa na hali kwamba msichana yule anamtaja kwa jina ili aweze kumhurumia. Badala ya Joram kumsaidia, yeye anawapigia polisi simu na kurudi ndani ya baa kuendelea na starehe zake. Mrembo huyo anachukuliwa na polisi ambao wanampeleka hadi hospitalini. Askari mmoja kwa jina Bob anapatikana akiwa amefariki kwa kuwa alikuwa amemguza Waridi bila kujua kwamba alipakwa sumu. Hapa ndipo Joram kutokana na maarifa yake anaanza kushuku kuwa kuna jambo la kuchunguzwa.

Kilele cha upelelezi huu ni pale Joram anapoambiwa kwamba maisha yake yalikuwa hatarini. Ukweli huu unamfanya Joram kuanza kupanga jinsi ya kumnasa mhalifu

huyu. Alipoondoka pale, Proper anaingia na kumuahidi Waridi kwamba atampeleka ahera. Waridi anachukua pombe na kuinywa akidhani ina sumu lakini kwa bahati mbaya, hafi. Anaamua kwenda Mburahati katika nyumba yake ambako baadaye anauawa kinyama na Proper kwa kukatwa vipande. Kifo cha msichana huyu kinamchochea mpelelezi kumtafuta Proper, kiasi cha kujisingizia kifo ili aweze kuchunguza zaidi kuhusu wahalifu wanaotaka kumuua.

Joram alilazimika kubadilisha sura na hulka yake ili kuendeleza uchunguzi huo. Alichukua umbo la mzee na kuchagua nyumba iliyozungukwa na kichaka cha miti. Hata hivyo, kifo kingine kilitokea kabla mhalifu hajanaswa. Ruta Bagambe ambaye alikuwa mmoja miongoni mwa mamia ya watoto wanaozurura mitaani aliuawa kwa bomu lililokusudiwa kumuua Joram. Kuna mtu aliyeelewa kwamba Joram alikuwa pale na alitega bomu hiyo kwa lengo la kumwangamiza. Bomu hilo lililipuka na kumwacha Bagambe akiwa maiti naye Joram akiwa katika hali mahututi. Kutokana na kisa hicho, Jodor Proper anapata tumaini la kuendelea na mipango yake bila wasiwasi kwani alidhani Joram amekufa.

Madai ya kifo cha Joram kinamuathiri sana Inspekta Kombora na Neema. Tunafafanuliwa kuhusu uhusiano wa Joram na Neema na jinsi walivyokutana kwa mara ya kwanza. Tunaelewa maisha ya Neema kabla ya kuwa mpelelezi na jinsi alivyolazimika kufanya lolote ili kupata habari. Tunamwona Joram alivyoyaokoa maisha ya Neema mikononi mwa majambazi waliokuwa wakitaka kumtupa baharini. Unono (mhusika aliyemuokota Joram akiwa katika hali ya mahututi) anamtembelea Neema kumpa picha ya Jodor Proper kwa maagizo yake Joram. Neema anaondoka na kwenda katika ofisi yake ya awali ambayo ilikuwa ya shirika la habari. Anagundua kutoka kwa mfanyikazi wa shirika hilo kuwa picha ile ilikuwa ya Chain Kimara au

Proper ambaye kwa wengi alieleweka kama profesa mwandishi wa vitabu. Neema alipopata anwani ya Kimara katika kitabu cha anwani anagundua kuwa anaishi mtaa wa India katika jengo lenye usajili wa namba 107. Badala ya kumngojea Unono, Neema aliamua kuchukua bastola kwenda kumtafuta Proper mwenyewe. Alipomuona alitulia roho na kudanganyika na wazo kwamba alikuwa mtu msomi, muungwana asiyeweza kutenda uovu. Baadaye anapoteza fahamu na alipogutuka, aligundua kuwa amedhulumiwa kimapenzi. Isitoshe, Proper alimpa sumu kali ambayo baadaye inasababisha kifo chake.

Mkutano wa siri ulifanywa tena chini ya uwenyekiti wa mhalifu ajulikanaye kama Proper. Mawasiliano yalifanyika kwa siri ambapo walijadili kuhusu mauaji. Yeyote aliyejaribu kupinga mauaji hayo alikuwa anatishwa kuuawa. Wakiwa na imani kuwa Joram amekufa, waliendelea kupanga jinsi ya kuwaangamiza viongozi wa nchi mbalimbali. Mwandishi anaeleza jinsi Proper alivyoweza kuwatia mtegoni watu hawa na kuwafanya washirika wake. Licha ya kuwa wahalifu wenzake walikuwa wamepinga hatua hiyo na hata kumtuma mtu mwingine amuue Proper ili asiendelee na mpango huo. Proper anamuua padre mmoja na kutorokea Dar es Salaam anakoendeleza mipango yake ya mauaji.

Inspekta Kombora akiwa ameshikwa na wasiwasi na hali ya taharuki anapata simu ya ajabu kutoka kwa Joram aliyekuwa amedaiwa kufa.  Kabla hajaondoka anaambiwa habari za padre, aliyetoweka na nguo zake za ukasisi kupatikana zikiwa na damu. Joram anasingizia kuwa ndiye mwenyekiti na kuita mkutano wa wajumbe. Anajitambulisha na kumualika Inspekta Kombora awashike wale wajumbe wahalifu. Inspekta Kombora aliwasiliana na katibu mkuu wa wizara yake mara moja baada ya kugundua kuwa swala hilo lilikuwa hatari kwa usalama wa kitaifa. Walizungumzia

umuhimu wa mkutano wa wajumbe ambao ulikuwa unafaa kutumika kujadili kuhusu utokomezaji wa ubaguzi wa rangi Afrika Kusini ili kusaidia Namibia kupata uhuru. Huko Arusha ,Proper anakutana na msichana mrembo kwa jina Sofia ambaye anaishi naye hadi wakati anapogundua siri yake kuwa ni mhalifu. Proper anamuua Sofia na kumteka nyara dereva wa teksi. Anampiga, kumjeruhi na kumuacha akidhani amekufa.

Katika mchakato wa Inspekta Kombora na kikundi chake cha askari kuchora mpango wa kumshika mhalifu naye mpelelezi akiandaa mikakati ya kumnasa, wanagundua kuwa picha walizoweka katika magazeti zilizaa matunda. Polisi wa Mwanza walipashwa habari na mwananchi mmoja kuhusu makazi ya mhalifu. Wanapoenda pale, Proper tayari alikuwa ametoweka na dereva wa teksi. Mwanamke mmoja alpatikana ameuawa na dereva mmoja akiwa hoi bin tiki. Hapo ndipo msichana kwa jina Nuru anajitokeza kwa mara ya kwanza anapokuwa anaandaa matayarisho ya wajumbe. Anakutana na watu wawili, mmoja akiwa mhalifu na mwingine akiwa mpenda wema anayemtafuta mhalifu.

Mwisho tunamuona Proper akiwa ameandaa mpango maalum wa kuwaangamiza wajumbe mbalimbali wa Kiafrika. Kama kawaida yake Proper anajaribu kumtumia Nuru kuwaua wajumbe kwa kutumia sumu kali. Kwa bahati nzuri, Joram anamtembelea Nuru kabla ya tukio hilo na kubadilisha sumu hiyo na poda ya kawaida. Proper anakasirika sana anapogundua kwamba mpango wake haujafanikiwa. Anaenda kumuua Nuru nyumbani kwake lakini anauawa kabla ya kutekeleza mauaji hayo.

### 3.1.0 Kiini cha uovu katika Riwaya

Katika sehemu hii mtafiti aliangazia kiini cha uovu katika riwaya za Ben Mtobwa. Tumezungumzia hasa mazingira kama kiini kikuu cha uovu kulingana na mtazamo wa mwandishi. Mbali na hayo mtafiti alitaja vijisababu vingine vidogo ambavyo vimejitokeza katika riwaya hii.

### 3.1.1 Mazingira kama kiini kikuu cha uovu

Kiini kikuu cha uovu hasa cha mauaji ya kikatili kulingana na Ben R. Mtobwa ni athari ya mazingira kwa wanadamu.Wazo hili linaungwa mkono na Cohen (2012) ambaye anataja sababu za kijamii na mazingira kama sababu kuu zinazomfanya mwanadamu kuwa muovu. Mazingira huchangia sana na huchukua nafasi kubwa katika kuchonga tabia za mwanadamu. Mauaji, hasa yale yanayojitokeza katika kazi za Mtobwa yanajaribu kutetea wazo kwamba mazingira huchochea tabia za mwanadamu kiasi cha kumfanya awe na tabia za kinyama. Kutoa mwanadamu uhai ni jambo ambalo ni kinyume na maadili Vaughn (2008). Anasema maadili hujibu maswali yaliyoulizwa na Socrates miaka ishirini na minne iliyopita. Kulingana na Vaughn (2008) Socrates alikuwa ameuliza swali kuhusu maisha ya wanadamu na hasa jinsi wanavyostahili kuishi katika jamii. Hakuna jamii yoyote ile, inayoweza kuunga mkono hali ya mwanadamu kuwatoa wenzao uhai.

Mtafiti amebaini kwamba mhusika mkuu katika riwaya hii na ambaye ndiye mhalifu amesawiriwa kama kiumbe anayepata raha anapotoa mwanadamu uhai. Mtu huyu ni mtaalamu wa kuua watu kwa kutumia mbinu zozote zile. Mwandishi anatoa ithibati inayoonyesha kwamba, tabia zake za kikatili zilitokana na mazingira yaliyomzunguka hasa alipokuwa mtoto. Matendo yale aliyoyapitia na kushuhudia yanamfanya kuwa mhalifu katika utu uzima wake. Mwandishi anatuambia kwamba Proper, Mswahili

aliyezaliwa mahali fulani katika pwani ya bahari ya Hindi. Akiwa na miaka kumi na miwili alidandia meli moja iliyotia nanga katika bandari ya Tanga. Meli hiyo ilikuwa na baharia wakatili kupita kiasi.Walimlaki kwa ukatili usiosemeka. Tunaambiwa ‘‘ Walimtendea mengi maovu, akitukanwa na kusimangwa. Aliishi kwa taabu mno, akistahamili yote hayo mwishowe akashika unyama wa mabaharia hao (uk.6).

Licha ya hayo, mtafiti alibaini kwamba Proper alishika tabia hizo za kinyama, akageuka kuwa na unyama zaidi ya wale mabaharia. Ndiposa akageuka kuwa muovu na kutekeleza mauaji mengi zaidi ya kikatili. Mazingira hayo yanamsugua akasugulika, naye akageuka kuwa baharia binadamu mwenye moyo wa unyama. Anamchukia kila mtu na hata kuichukia nafsi yake mwenyewe. Alitamani kutenda tendo fulani bovu ambalo lingeumiza jamii. Unyama aliokuwa nao Proper unawaacha wengi vinywa wazi. Mwandishi anasema kwamba ni vizuri Proper hakuwa mwanasayansi mwenye vipaji vya ugunduzi, ugunduzi ambao ungemwezesha kuiteketeza jamii. Tunaambiwa,‘‘Angekuwa na uwezo wa kujitengenezea bomu za kinuklia, angeifanya dunia itoweke kutoka uso wa ulimwengu’’(uk.6).

Hali ya kupenda kufanyia wanadamu wenzake maovu kunamfanya kuhitimu zaidi ya mabaharia wenzake kiasi kwamba, alitenda unyama zaidi yao. Kwa mfano tunaambiwa, “Hakusita kumtupa baharini mtu yeyote aliyegundulika kudandia meli kama alivyofanya yeye utotoni’’ (uk.6). Kauli hii inatudhihirishia jinsi alivyokuwa mtu ambaye hana utu. Anasahau kwamba yeye hakutupwa baharini alipodandia meli bali aliruhusiwa kuishi humo melini.

Mwandishi anamsawiri Proper kama mtu ambaye mazingira yalimfanya kuwa na hamu ya kutenda maovu zaidi. Haikuwa dhambi kufanya mapenzi na mwanamke na

kuondoka alfajiri baada ya kukata koo la mwanamke huyo (uk.7). Hii inaonyesha kwamba alikuwa na chuki maishani. Furaha yake ikawa ni kutoa wenzake uhai. Hakuwa na mapenzi ya dhati kwa mwanamke yeyote. Aliwaona wanawake kama viumbe vya kutumiwa na baadaye kuuawa. Isitoshe, anahitimu kutoka kwa maovu madogo madogo na kujiunga na waovu wenye nia ya kutenda unyama wa kustaajabisha. Mazingira hayo pia yalimfanya kuwa ni mtu mwenye kuvutiwa zaidi na mambo ya kikatili yasiyokuwa na mchango wowote chanya katika jamii. Alijiunga na kundi lenye waovu wa kiwango cha juu zaidi. Mtobwa anasema ingawa Proper alitenda maovu sirini, sifa zake zilifikia masikio mbalimbali. Mmoja kati ya waliosikia hayo alivutiwa sana na ukatili huo akaamua kukutana naye. Tunaambiwa : ‘‘Siku chache baadaye alikutana na Proper kwa siri katika meli hiyo. Wakaiacha meli hiyo kwa siri vile vile ’’ (uk.6).

Anapojiunga na kundi la wakatili, mazingira hayo yanamfanya kuwa mhuni zaidi ya wenzake. Mtobwa anasema kwamba baadaye Proper alipohitimu tayari alikuwa hodari wa wote. Akawa anaandaa mauaji, kusababisha mapinduzi, kuzorotesha uchumi. Tunambiwa, “Alikuwa mtu anayeipenda kazi yake, alifanya mengi yaliyotisha viongozi wake’’(uk.6-7). Hapa mtafiti amebaini kwamba, mara nyingi binadamu waovu husawiriwa kama watu wanaovutiwa zaidi na waovu wenzao.

Mtafiti amebainisha kuwa Proper ni kiumbe aliyeamini kwamba yeyote anayemuudhi anafaa kifo. Kwa mfano, anamuua kikatili padre mmoja ambaye naye kwa bahati mbaya ni mjumbe wa wahalifu. Alipohisi kwamba labda kuna mtu nyumbani mwake hachukui nafasi ya kumtafuta ili ajue lengo lake, anafyatua tu risasi. Mtobwa anasema kwamba hakujua mtu huyo alikuwa ametokea wapi, wala hakuwa na haja ya kutazama kuwa ni nani. Aliinua mkono wake wenye bastola na kafyatua risasi tatu za mfulilizo. Mwili wa mtu huyo ukamwangukia kitini huku akitapatapa. Proper

alipoinuka na kumtazama hakuweza kumtambua. Tunaambiwa kuwa, ‘‘Uso mzima ulikuwa umefumuliwa na risasi kiasi cha kuacha nyama nyama zenye damu ambazo hata mama yake aliyemzaa, asingemtambua’’ (uk.69).

Mtekelezaji mkuu wa mauaji haya ya kikatili anayazungumzia kimzaha tu kama anayezungumzia kifo cha mbwa. Anasawiriwa na mwandishi kama kiumbe asiyethamini maisha ya wanadamu wenzake. Proper anawaambia wajumbe kwamba serikali haitagundua kuwa ni wao wamehusika katika mauaji ya Joram. Kisha aliongezea kusema kuwa Joram hakufa kwa sumu kama ilivyotarajiwa. Tunaambiwa, ‘‘Walipanga hila watulaghai tu baada ya kunusurika kwake. Nililazimika kumuua kwa bomu’’ (uk.61). Inabainika wazi kwamba mhalifu huyu alikuwa ameamua kumuua Joram kwa vyovyote vile.

Anajaribu kumuua Nuru kwa sababu hakutimiza jukumu alilopewa la kuua wajumbe kwa kutumia sumu ya poda. Proper anakasirika na kumuahidi Nuru kwamba angemuua kinyama kuliko alivyowaua wale wengine. Anamwambia kwamba hakujua ni watu wangapi walikuwa wamekufa kupitia mkono wake. Isitoshe, anamtusi na kumwita malaya. Anamwambia, “Utakufa kifo cha kinyama kuliko vifo vyote vya kinyama ambavyo vimewahi kutokea katika historia ya dunia’’ (uk.116). Hapa mtafiti amebaini kwamba Proper ni mtu aliyetatua mambo kwa kuwaua wanadamu wenzake.

Waridi ni mhusika wa kike, mrembo ambaye naye pia tumeonelea kwamba alimuua mwenzake kwa njia ya kikatili. Mtafiti amebaini kuwa msichana huyu pia anasawiriwa kama mtu aliyepotoka kutokana na malezi katika mazingira yasiyofaa. Mazingira yale yalimfanya kuwa kiumbe asiyejali mapenzi bali aliyeweza kufanya lolote ili kutimiza lengo lake la kupata fedha. Uovu haujui jinsia au uana. Matendo ya Waridi yanatudhibitishia kuwa uovu unaweza kutekelezwa na yeyote. Mtafiti

amebaini kuwa mwandishi anatudhihirishia wazi kuwa Waridi alikuwa akimuiga mama hasa pale anaposema kuwa:

> Kwani mama yake pia alikuwa mtu wa nipe ni kupe. Alifanya biashara yake katika vitongoji vya Mwanza, katika moja wapo ya vibanda vibovu, akikaribisha yeyote mwenye "chochote"(uk.9).

Taarifa hii imetuonyesha wazi kwamba msichana huyu alidhani yale maisha aliyoishi mamake ndiyo njia ya pekee ya kujipatia riziki. Utafiti wetu umetudhihirishia kwamba Waridi naye alifanya kazi hiyo ya uasherati katika mabanda ya Mburahati alipokuwa mtu mzima.

Mtafiti amebaini kuwa Waridi anakuwa na imani kwamba wanaume ndio njia ya pekee ya kupata riziki. Anatumiwa na wanaume wengi ambao wanampatia pesa za kujikimu. Anapokutana na Bomba anaona kwamba maombi yake yamejibiwa. Bomba ni kijana aliyekuwa na pesa nyingi ambazo walizitumia na Waridi. Bomba anapotishia kumuacha baada ya kumtumia, Waridi anaamua kumuua kinyama.

Wazo lilimjia Waridi kwamba Bomba alikusudia kumtupa baada ya kupata pesa nyingi hizo ili aende zake Nairobi akatumie peke yake! Waridi anajishauri achote kidogo afiche lakini anashikwa na tamaa.Waridi alikuwa anamwona Bomba kama kitega uchumi na hivyo kumkosa ilikuwa hasara kubwa. Hapo ndipo alipanga njama ya kuangamiza Bomba ili apate pesa zote. Tunaambiwa, ''Akasita, alizihitaji zote. Akaamua kuzipata. Akazirudisha kama vilivyokuwa na kurudi zake nje'' (uk.11).

Mtafiti amebaini kwamba uovu haujui jinsia kwani hata kuna wanadamu wa kike ambao huweza kutenda matendo ya kinyama. Hata ingawa taji nyingi zadai kwamba matukio mengi ya kihalifu hutendwa na wanaume, Ben R. Mtobwa anawasawiri uovu kama tabia ambayo haijui uana, kwani hata Waridi anamuua Bomba bila kujali.

### 3.2.1 Mauaji katika misingi ya kisiasa

Mtafiti amebaini kwamba viongozi hasa wenye nyadhifa kuu serikalini hapa Afrika wakati mwingine hushiriki katika mauaji ili kuhifadhi nyadhifa zao serikalini. Inaaminika kwamba wao hushiriki katika unafiki ili kujitajirisha kwa njia zisizofaa. Hapo ndipo wahalifu hutumika kutekeleza kazi chafu kama vile kumwaga damu ya watu wasiokuwa na hatia. Binadamu yeyote anayejaribu kupigania haki anakomeshwa kwa kifo. Ndiposa tunaona wajumbe katika riwaya hii wakikutana ili kujadili jinsi ya kumuua Joram ambaye wanaamini kuwa ndiye pingamizi katika mipango yao. Mwandishi anatuambia kwamba, "Naam, lazima afe," sauti nyingine iliunga mkono. ''Afe, kabla hatujainua mkono kufanya lolote tulilokusudia '' (uk.1).

Wanatoa mfano kwamba Joram hapo mbeleni alikuwa amekorofisha mashujaa waliotaka kuiangusha utawala wa nchi ya Ngoko. Mtafiti amebaini jinsi mwandishi alivyoangazia wanasiasa na wafanyikazi wa serikali wanavyopanga kumuangamiza mpelelezi kwa njia ya kikatili ili asiwazuie kupata nafasi ya kufanya uhalifu. Mwandishi anasema kwamba watu hao waliokusanyika hawakuwa watu wenye njaa ya pesa wala kiu ya utajiri bali walikuwa watu mashuhuri walioshiba na kudhamiria kulinda shibe yao.Tunaambiwa, ''Wote walikuwa na hadhi mitaani, nyadhifa serikalini, na heshima katika chama. Wote walikuwa na matarajio ya kuvuna matamu'' (uk.2). Hivyo basi tunaona kwamba lengo lao kuu inakuwa ni kulinda nyadhifa zao za kisiasa.

### 3.2.2 Mauaji kusetiri ushahidi

Proper alimuua Sophia kikatili ili kuficha ushahidi. Anapong'amua kuwa amegundua siri yake, hakusita kumwangamiza. Alikuwa amemtumia kujificha wala hakuwa na mapenzi ya dhati kwake. Mtafiti alibaini kwamba Proper alidhani kwamba Sophia

ndiye kiumbe pekee aliyemshuku pale Mwanza. Aidha, alidhani asingetambuliwa na yeyote baada ya kifo cha Sophia. Mwandishi anasema, “Sophia alisongeza shingo. Hakutarajia radi iliyompiga ghafla. Lilikuwa pigo kali jepesi lililotua katika shingo hilo na kulivunja kabisa” (uk.92).

Mwandishi anasema kwamba, Sophia hakujua kapigwa na nini. Hili ni dhihirisho Anapotuambia, “Wala hakuona ugumu wa kufa. Alianguka chini na kupapatika kwa muda na kukata roho” (uk.92). Mtafiti aling’amua kwamba Proper alikuwa na tajriba kuu katika mauaji. Usemi huu unatudhihirishia kwamba Proper alielewa sehemu za mwili ambazo zikipigwa binadamu hufa bila kuhisi maumivu yoyote.

### 3.2.4 Tamaa ya mali na uongozi

Mtafiti alibaini kwamba tamaa ya pesa na uongozi pia imesawiriwa kama moja kati ya sababu zinazoweza kumfanya mtu awe muuaji. Katika riwaya hii kuna watu ambao mbali na kuchochewa na mazingira, waliwaua wenzao kwa sababu ya tamaa ya pesa. Mfano mzuri ni Waridi. Msichana huyu anamuua mpenzi wake kikatili kwa sababu ya fedha zake. Wanaponda raha lakini Bomba anapomwambia Waridi watengane, matamshi hayo yanamkasirisha sana Waridi. Tunaambiwa:

> Kijana huyu mwenye asili ya Kiarabu alikuwa mtu ambaye Maua alimhitaji. Siku zote alionekana amejaa. Fedha kwake hazikuwa na tatizo.Wala hakuona uchungu kutumia fedha hizo. Kadhalika fedha zake hazikukaa mfukoni kama wanaume wengine. Kitita cha elfu kumi au ishirini kikiwa kimefungwa kwa mpira kingekaaje mfukoni? Kwa hivyo Waridi alizoea kutimiza mahitaji yake kwa kutumia fedha hizo. Waridi anaona atakuwa na shida sana kuanza tena kujitafutia riziki. (uk.10).

Hili ni dhihirisho tosha kwamba hakuwa na mapenzi ya dhati kwa mwanaume huyu bali alikuwa anahitaji tu fedha zake. Waridi alirudi chumbani baada ya kumsikia Bomba akioga bafuni. Akafanya haraka na kuuendea ule mfuko ambao aliufunua.

Macho yake yalikutana na furushi kubwa la noti ambalo hakupata kuliona maishani. Kwa kukadiria zilikuwa laki nne. Mwandishi anasema: ‘‘Waridi akajishauri kuchota kidogo azifiche. Kisha akasita. Alizihitaji zote, akaamua kuzipata ’’(uk.11).

Ajabu ni kwamba anapomaliza kumuua Bomba, pesa zikawa zimetoweka. Waridi anakosa bwana na pesa. Tunaambiwa, “...wazo lake sasa lilikuwa moja tu, kuhesabu pesa zake kikamilifu. Lakini muujiza ulikuwa ukimsubiri. Mfuko ulikuwa umetoweka” (uk.11-12).

### 3.2.5 Mauaji ya kujiokoa

Mtafiti aligundua kwamba Proper mwenyewe anauliwa kinyama anapokuwa anajiandaa kumuua Nuru. Anapogundua kuwa amefeli katika jaribio lake la kuua wajumbe mbalimbali wa mataifa, anachukua hatua ya kumuua Nuru kwa kukosa kufuata maagizo yake. Hapo ndipo anapolipuliwa kwa bunduki. Joram anapotupa macho katika kiti alichokalia Proper, anashangaa kuona kitu kama uji uliochanganyika na damu nzito. Baada ya kutazama kwa makini, ndipo anapofahamu ni kipi alichokuwa akishuhudia. Tunaambiwa, “Ulikuwa ubongo wa binadamu uliotoka katika kichwa kilichofumuliwa na risasi” (uk.122).

Kuna wanadamu wanaoua ili kujinusuru. Muuaji wa kikatili anapogundua kwamba maovu yake yametambulika, huua wanadamu wanaomzunguka ili wasije wakamsaliti au kushtaki. Mfano mzuri ni pale Proper anapomuua Neema, anafanya hivyo kwa imani kwamba, ni yeye tu ndiye anayejua kwamba anahusika na vifo vya kikatili vya Waridi na Joram aliyedhaniwa kwamba amekufa.

### 3.3.0 Utekelezaji wa mauaji

Mtafiti aling'amua kwamba mambo yale Proper aliyoyapitia yalimfanya kiumbe huyu kutekeleza mauaji ya kinyama zaidi na kusababisha vifo vya watu wengi sana. Kwa mfano anamuua Waridi kinyama kwa kuufanyia mwili wake upasuaji wa kugawanya viungo vya mwili wake, huku Waridi akiona. Maelezo ya mauaji haya yalimtia hofu binadamu yeyote mwenye akili timamu. Haya ni mauaji yanayoonyesha kwamba aliyeyatimiza ana kikwazo moyoni, kikwazo ambacho kimemsumbua kwa muda mrefu. Kwanza, anamfunga mdomo kisha anachomoa kisu kikali kutoka ubavuni na kuanza kupita juu ya mwili wake. Maumivu yalikuwa makali lakini Waridi hakuwa na uwezo wa kulalamika. Anachoweza kufanya ni kuendelea kukodoa macho yenye dalili zote za hofu na maumivu. Macho hayo yanayashuhudia mikono yake ikikatwa mmoja baada ya mwingine na kuwekwa juu ya kitanda. Mtafiti alibaini kwamba mtu anayesumbuliwa na maisha, anachukia maisha na hajali kuyaharibu.Tunaambiwa:

> Kisha tumbo lilifumuliwa na utumbo kumiminiwa katika sinia lililokuwa mezani. Alikuwa amekwisha kata roho pindi kichwa chake kilipitwa na kuwekwa juu ya debe, kando ya kitanda (uk.31).

Taarifa hii inadhihirisha wazi kiwango cha uhayawani ambao Proper alikuwa nao. Proper anasawiriwa kama mwenye roho ya unyama asiyekuwa na chembe chochote cha utu katika mishipa ya damu yake. Tunaambiwa kwamba:

> Akiwa ameridhika na kazi yake, Proper alivua nguo zake zenye damu na kuzifutika katika mifuko ya koti lake ambalo alivaa na kutoka nje pole pole kama wateja wengine (uk.31).

Mtafiti alibaini kwamba kitendo cha kutoka polepole ni dhihirisho kuwa tendo la kuua ni jambo la kawaida kwa Proper. Jodor Proper ni muuaji wa kikatili ambaye amesawiriwa kama mwanadamu asiyejua njia nyingine yoyote ya kutatua shida ila kuua. Kwa mfano anapokosa kufaulu kumtumia Waridi katika mpango wake wa kuua

Joram, Proper anasema kwamba Joram alidhani anacheza na watoto wadogo kama alivyozoea. Anamwambia Waridi kuwa alikuwa amemfanyia Joram hisani kubwa ili afe kistaarabu kutokana na sumu, lakini akajitia ujanja. Proper anasema, "Sasa atakufa kifo cha kusikitisha zaidi" (uk.28).

Mbali na kuchinja watu kwa visu, muuaji huyu anatumia sumu kali kusababisha vifo vya kikatili. Anafanya kazi hiyo kwa njia ambayo madaktari wanashindwa kung'amua kiini hasa cha kifo. Mfano mzuri ni pale anapomlazimisha kumuua Joram kwa kutumia sumu kali. Kwa bahati mbaya polisi mmoja ajulikanaye kama Bob ndiye anayekumbana na kifo hicho. Hayo yanatokea pale Waridi anapomgusa Bob kwa mkono wenye sumu. Mwandishi anasema:

> Marehemu alipopelekwa hospitalini daktari hawakuchelewa kutoa taarifa yake. "Ugonjwa wa moyo" walidai. "Ulimshika ghafla wakati akivaa nguo zake" (uk.20).

Mauaji mengine ya kikatili yanayotekelezwa na Proper ni pale anapomuua Neema. Alidhani kwamba ndiye kiumbe pekee aliyeshuku kwamba amehusika na kifo kilichotuhumiwa cha Joram. Hivyo basi, tunaweza kusema kwamba anamuua ili kuficha ushahidi. Kwanza anampiga kwa njia inayomfanya kupoteza fahamu na baadaye kumnajisi.

Neema, anashikwa na hofu pindi anapokumbuka kwamba muuaji huyu alimnywesha kitu asichokifahamu. Isitoshe, anamhakikishia kwamba atamfuata mpenziwe Joram kule alikoenda. Mwandishi anasema kuwa hakuuona uwezekano wowote wa kuifanya hatia ya mtu huyu idhihirike. Lakini Neema anashikwa na hofu moyoni. Si hofu ya kufanya mapenzi bila kukusudia bali hofu ya kutofahamu kitu gani alichopewa hata akavuliwa nguo bila kufahamu. Ilikuwa kama ndoto ya kitambo

anayoikumbuka kwa shida. Alikumbuka kama kwamba aliyenusa harufu fulani inayomfanya atokwe na fahamu. Tunaambiwa:

> Pia alikumbuka kuwa alimsikia mtu huyu akimhoji juu ya kifo cha Joram Kiango, naye akiropoka kila kitu alichofahamu. Alimweleza juu ya yule mwanamke sura mbaya aliyoileta picha yake. Kisha akakumbuka alinyweshwa kitu fulani (uk.55).

Mtobwa anatuambia kwamba Unono anapofika anamkuta Neema akiwa katika kile anachodhani ni usingizi. Unono anapoteza dakika kadhaa kulihusudu kwa wivu umbo la Neema ambalo lililala kifudifudi juu ya kochi. Neema anauliwa kistadi kiasi kwamba inamchukua Unono muda kugundua kwamba alikuwa akitazama maiti. Kisha anapoteza dakika nyingine kadhaa, akijaribu kumwamsha kwa kumsukasuka. Tunaambiwa:

> Mara akaiona damu nzito ambayo ilikuwa ikimtoka mdomoni na puani, ulimi ulivyoponyoka kutoka kinywani na kuduwaa nje, akayaona macho yalitoka nje kila kitu kilitangaza mauti (uk.56).

Ukatili wa mhusika huyu unadhihirika wazi pale ambapo anakuja mwenyewe kuthibitisha kwamba kazi yake imekamilika. Tunaambiwa, "Marehemu alikuwa amekufa kwa namna aliyoitaka"(uk.58). Kauli hii inaonyesha kwamba Proper ni mtu ambaye anafurahia sana kuua kiasi kwamba hakuogopa maiti. Mwandishi anasema yeyote ambaye angeingia ndani kumtazama angedhani Neema yuko usingizini. Lengo kuu la Proper lilikuwa kuhakikisha kwamba hakuna ushahidi wowote wa kuonyesha kwamba Neema ameuawa.

Mauaji mengine yanayotekelezwa na Proper kinyama ni yale ya Father Peter Jamaa. Padre huyu anadai ndiye aliyekuwa sirini baina yake na makao makuu. Mwandishi anasema:

> Aliinua mkono wake wenye bastola na kufyatua risasi tatu za mfululizo bila kumuona mtu aliyekuwa kwake. Mwili wa mtu

> huyo ulimwangukia kitini huku ukitapatapa lakini binadamu huyo hashtuki. Proper alipoinuka na kumtazama hakuweza kumtambua Tunaambiwa: "Uso mzima ulikuwa umefumuliwa kwa risasi kiasi cha kuacha nyama nyama zenye damu ambazo hata mama yake aliyemzaa, asingemtambua" (uk.69).

Ingawa Waridi hakumuua Bomba kwa hiari, anatekeleza mauaji hayo kwa njia ya kinyama zaidi. Anamuua mwenzake waliokuwa wamejuana, kwa kumpasua kichwa kwa jiwe kubwa la ajabu. Bomba anapokuwa amelala kando ya anaanza kukoroma, hapo ndipo Waridi anaamka polepole na kunyata hadi uwani ambako alibeba kwa taabu lile jiwe kubwa alilokuwa ameliandaa mchana. Anaingia nalo hadi chumba ambako analenga barabara kwenye kichwa cha Bomba na kuliachilia jiwe lile. Anatekeleza mauaji haya kwa njia ya kikatili zaidi isiokisiwa. Bomba anakurupuka kwa kupaa angani na kutua tena kitandani. Alitoa mlio wa maumivu kwa sauti ndogo nyembamba ambayo inamwingia Waridi. Hata mbwa wako uliyemzoea huwezi ukamuua kwa njia hiyo.

Mtafiti alibaini kwamba kitendo hiki cha kuua kinyama kinaonyesha mauaji ya kikatili na kwamba Proper alikuwa na chuki moyoni kwa muda mrefu. Ni binadamu mwenye hasira moyoni ndiye anayeweza kumuumiza mwenzake kwa njia hii. Anapompiga kichwani kwa kutumia jiwe kichwa kinafumuka. Tunaambiwa, "Ubongo uliochanganyika na damu ulimiminika kitandani na kuchafua shuka. Lakini bado aliendelea kutapa huku na huku, akisema hili na lile" (uk.12).

Waridi anajuta baadaye, ingawa bado tunamuona kama mhalifu maanake hata baada ya tendo hilo, anarudi chumbani kutimiza lengo lake; yaani kuchukua pesa. Anamvuta hadi uani na kumtumbukiza chooni. Tendo linalodhihirisha ukatili wa hali ya juu. Waridi mwenyewe alijikaza kiume kwa kumfungafunga marehemu Bomba kwa blanketi kubwa kisha akajaribu kumwinua kumtoa nje. Kitendo hiki kinaonyesha

ukatili ambao ni jambo la kihalisia katika maisha ya sasa. Tamaa inayoambatana na chuki inamfanya Waridi kubeba maiti ya Bomba kwenda kutumbukiza chooni.

> Akamvuta hadi uwani huko, alijitahidi hadi akaifikisha maiti chooni ambako kulikuwa na tundu kubwa lililofunikwa na bati. Akaliinua bao hilo, na kumtumbukiza marehemu. Kisha akalifunika kama lilivyo hapo awali (uk.12).

Kinadharia mihimili ya nadharia ya uhalisia inatusaidia kutambua kwamba wahalifu huwa ni wanadamu wa kawaida wanaoishi miongoni mwetu.Wahusika kama vile Proper na Waridi ni watu wa kawaida wanaoishi katika jamii. Mhusika kama vile Bomba anawakilisha watu katika jamii wanauawa na rafiki zao.

Isitoshe, sehemu hii pia imefichua uovu unaopatikana katika jamii. Aidha, mtafiti ametumia mhimili wa nadharia ya maadili kuonyesha mahusiano kati ya jamii mbalimbali na mazingira yao. Utafiti umedhihirisha jinsi Ben R. Mtobwa anavyotumia riwaya zake teule kuweka wazi maovu na sababu zinazofanya mwanadamu kuwa muovu. Kwa kufanya hivyo, mwandishi huyu anajaribu kutimiza majukumu yake ya kurekebisha jamii kimaadili.

### 3.4.0 Athari ya mauaji ya kikatili

Mauaji ya kikatili ni aina ya uovu ambao huathiri sana jamii, polisi wanaochunguza kesi hizo na wapelelezi wenyewe. Athari hizo hutokea kwa njia zifuatazo:

### 3.4.1 Athari kwa wanajamii

Mtafiti aling’amua kwamba Proper anapokuwa katika harakati ya kutekeleza mauaji, wanajamii huathirika kwa njia mbalimbali. Wengine hupoteza maisha yao wakati mhalifu anapokuwa anajaribu kutekeleza mauaji. Proper hakuwa na habari kwamba kulikuwa na mtu mwingine mle ndani ya nyumba iliyokuwa maficho ya Joram.

Isitoshe, Joram naye hakujua kwamba makazi hayo ya siri aliyohamia yalikuwa na mtu mwingine. Tunaambiwa, “yalikuwa malazi ya Ruta Bagambe mmoja kati ya mamia wa vijana wazururao katika jiji la Dar es Salaam”(uk.35). Mtafiti amebaini kwamba mvulana huyu anakufa kifo asichokitarajia.

Analipuliwa na kufa kiasi cha kutotambulika na watu wengi. Polisi na wanajamii wote walidhani kwamba mwili huo ni wa Joram. Mwandishi anatumia mhusika huyu kupumbaza mhalifu ili mpelelezi apate nafasi ya kuendeleza kazi yake. Utafiti wetu ulituwezesha kung’amua jinsi mhusika Bagambe, anakatiziwa maisha kwa sababu ya mipango ya mauaji. Inabainika wazi kwamba, Bagambe alikuwa ndani ya nyumba alipoona mtu akificha kitu. Naye kwa tahadhari kama paka anayenyemelea panya, akaamua kwenda kuchukua kile alichoona kikifichwa. Anapofika anapekuapekua polepole na anapokiona, anatazama kwa mshangao.Tunaambiwa:

> Mshangao ambao ulikatizwa na mlipuko mkali uliofanya apae juu na kutua chini hali tayari katawanyika vipande vipande mfano wa nyama ya kopo inayoandaliwa kusindikwa (uk.36-37).

Mlipuko wa bomu unaposababisha kifo cha kusikitisha huwafanya wananchi kuwa na huzuni kubwa. Biwi la simanzi linatanda miongoni mwa wanajamii wanaolia machozi na wengine kuomboleza kwa sauti. Wananchi katika sehemu hiyo wanasononeka sana na wengine kushikwa na hofu kiasi cha kuogopa kutizama maiti. Watu wachache sana wanaotazama tukio hili kwa muda mrefu. Tunaambiwa:

> Wengi walitupia jicho kwa sekunde chache na kisha kugeuza nyuso zao upande mwingine wakiguna au kufuta machozi. Mama mmoja alisikika akilia kwa sauti (uk.37).

Aidha, mtafiti alibaini kwamba panapotokea mauaji, jamii huathirika sana kihisia. Majirani ambao mara nyingi ndiyo huwa wa kwanza Kukumbana na maiti hupata huzuni nyingi. Msichana ajulikanaye kama Waridi anapouawa katika nyumba yake,

wateja wake pamoja na majirani wanaona hofu na hata kuchanganyikiwa. Mteja wa tatu ndiye aliyewaambia majirani kilichotokea, kisha naye pia akatoweka. Hali hiyo ya kutoweka ina maana kwamba alikuwa katika hali ya uoga usiokuwa na kifani. Hakujua la kutarajia, kwani maisha yake yangekuwa hatarini. Mara nyingi watu hutoroka kunapotokea maafa kwa hofu ya kushukiwa au naye kuwa mhasiriwa, Tunaambiwa, “Majirani walichanganyikiwa kwa muda mrefu. Mmoja wao alitapika. Walilia kwa nguvu. Umati mkubwa ulifika, polisi pia hawakuchelewa” (uk.31). Mtafiti alibaini kwamba baada ya mauaji haya kulikuwa na hali ya taharuki na huzuni nyingi miongoni mwa wanajamii.

Wanajamii hasa wajumbe waliokuwa wakimuunga mkono muuaji, baadaye wanashikwa na hofu mauaji yanapokuwa mengi zaidi. Isitoshe, njia anazotumia kuua watu zinawatia hofu kiasi cha kutamani kujiondoa katika kundi hilo. Kulingana na mwandishi, Proper ambaye alikuwa mwenyekiti anawageukia wajumbe waliokuwa wameduwaa kwa maelezo yake na kuwatisha. Tunaambiwa:

> Hawa ni vibaraka wake. Lakini Proper anayeyafahamu madhambi yao mengine, amewatisha hata kuwafanya walazimike kumtii. Yeyote ambaye angeyadharau maagizo ya Proper angeteketezwa kinyama (uk.82).

### 3.4.2 Athari kwa polisi

Mauaji ya kikatili huzua hali ya uoga na taharuki miongoni mwa wananchi na askari. Inspekta Kombora anashikwa na uoga baada ya kifo cha Waridi. Anamwona mhalifu huyo kama mtu ambaye amekwepa mbinu zote za upelelezi. Kufikia sasa, hakukuwepo fununu yoyote. Wala hakuwa na uhakika kama alikuwa mtu mmoja au ni kikundi cha watu ambacho kilikuwa kikifanya hayo. Polisi wanaokosa mshukiwa wanalazimika kushirikiana na mpelelezi. Tunaambiwa, “Kifo cha yule malaya mzuri,

Waridi; kifo cha Joram, kifo cha Neema, kifo kipi kingefuata? Na ni vifo tu au ni pamoja na…nini? Aliendelea kutaabika kimawazo''  (uk.71).

Hali ya kusaka wahalifu, hufanya askari polisi kukosa usingizi. Siku ambayo hafanyi zamu ya usiku,  Kombora anakaa katika kituo cha polisi hadi usiku wa manane. Kombora hasinzii hata kidogo hasa pale anapowaza kuhusu njia za kumshika mhalifu. Wala hakudhani  kama angeweza kupitwa na lepe la usingizi usiku wowote hadi wakati mhalifu huyo angetiwa mbaroni  au  kufa. Zilikuwa zimesalia siku chache kabla ya mkutano maalum wa viongozi kufanyika mjini Arusha. Ilisemekana kuwa viongozi wa nchi nyingine huru za Afrika wangehudhuria. Wazo la wahalifu hawa kuwadhuru wageni linasononesha askari. Wanajaribu njia zote kumtia mikononi kabla ya wakati kuwadia. Inspekta  Kombora anasema:

> Na mtu huyu...lanakum anayekusudia kuwaangamiza vyongozi hawa kinyama yuko huru mahali fulani katika nchi hii. Vipi Kombora angeweza kulala  uk .83)?

Kaulu hii inaonyesha kwamba  Inspekta Kombora alikuwa akisononeshwa sana na hali ya kutomtia Proper nguvuni. Wasiwasi wake ilikuwa kwamba Proper angeuua mtu mwingine tena.

Mtafiti alibaini kwamba askari hufariki wakiwa katika harakati ya kuwasaka wahalifu. Mara nyingi hawana vifaa vya kujikinga, hivyo basi huathiriwa wakiwa kazini kama ilivyomfanyikia Bob. Polisi wengine hupoteza maisha wakiwa katika harakati ya kushughulikia uchunguzi wa vifo hivyo vya kikatili. Bob, polisi ambaye alienda kumchukua Waridi alipokuwa ameumia, anakufa kwa sababu ya kumguza Waridi bila kujua kwamba alikuwa amepakwa sumu na Proper. Askari mwenzake alipofika kwake asubuhi anamkuta akiwa amekufa kwa njia ya ajabu. Kwanza anashangaa moyoni akijiuliza ikiwa ni mzaha au mchezo ambao umeanza. Hii

inaonyesha kwamba aliuliwa kitaalamu kwa njia ambayo ilishangaza askari mwenzake. Anapoona povu lenye damu linamtoka mwenzake mdomoni na puani anaruka nyuma, kwani hakuwahi kuona kifo cha aina hiyo. Kisha kumsogelea kwa uangalifu kuchunguza vizuri zaidi. Tunaambiwa, ‘‘Akiyaona macho yake yalivyoduwaa, akauona ulimi ulivyotoka na kusahauliwa nje’’, (uk.20).

Athari zingine hutokea na baadaye isijulikane kilichosababisha ugonjwa au vifo vya askari hawa. Mwandishi anasema kwamba, ‘‘Hakuna aliyeshuku kuwa ni sumu ile ya aina yake, ambayo aliigusa kutoka kwa Waridi, na kufikisha sehemu iliyokusudiwa kufika mwilini mwake, bila yeye kijua” (uk.21). Hapa mtafiti alibaini kwamba wakati mwingine vifo vikitokea askari na madaktari wengine huchukulia vifo hivyo juujuu na kukosa kugundua ukweli.

Mauaji ya kikatili huwatia polisi wenyewe hofu nyingi. Kwa mfano Inspekta Kombora mwenyewe anashikwa na uoga. Watu wanakufa kwa njia ya ajabu na hakuna mshukiwa mmoja anayeshikwa kutokana na mauaji hayo. Inspekta Kombora anahofia maisha yake mwenyewe. Kifo kinachotokea kutokana na bomu kinamfanya awe na hofu zaidi kuliko wananchi waliokuwa wakitazama.Tunaambiwa:

> Macho yenye hofu na huzuni yalikuwa yakiwatazama askari ambao walikuwa wakiokota viungo vya marehemu kimoja baada ya kingine na kuvitia katika sanduku (uk.37).

### 3.4.3 Athari kwa mpelelezi na wasaiizi wake

Mpelelezi huhatarisha maisha yake anapokuwa katika harakati ya kumtafuta muuaji. Mpelelezi Joram anananusurika kifo mara tatu. Mtobwa anamsawiri Joram kama mmoja wa wale wapelelezi ambao hukumbana na hali za hatari wanapokuwa kazini. Kwanza mahasimu wake wanajaribu kumuua kwa kutumia sumu na baadaye bomu. Mfano mzuri ni pale anapotegewa bomu katika nyumba aliyokuwa akitumia kama

maficho yake. Bomu hilo nusura limwangamize Joram kwani mlipuko huo ulimkuta akiwa amesimama wima na fimbo mkononi. Joram anaduwaa anapoona ghafla mtu akizuka mbele yake na kupaa angani ambako anaumia kutokana na nguvu ya bomu. Anajikuta angani kisha anajibwaga chini akifuatwa na lundo kubwa la vitu ambavyo vinamfunika. Tunaambiwa:

> Hakuwa na muda wa kusikia maumivu pia. Alihisi kama aliyepoteza kichwa au ubongo. Fahamu zikamtoka na nafasi yake kuchukuliwa na kiza kinene kinachotisha (uk.37).

Isitoshe, wakati mwingine msaidizi wa mpelelezi huuawa. Mauaji kama haya ya kikatili hufanya wapendwa na wahasiriwa kuwa na hamu ya kulipiza kisasi. Kwa mfano, Joram ambaye ndiye mpelelezi mkuu katika riwaya hizi anaposikia kuwa msaidizi wake (Neema) ameuliwa, anakuwa na hamu ya kulipiza kisasi. Mwandishi anatuambia kwamba, "…Joram hakuwa na haja ya kuambiwa kuwa kifo hiki ni matokeo ya kazi ndogo aliyompa Neema kupeleleza juu ya mtu au watu hawa waliokusudia kumua" (uk.81). Tangu wakati huo Joram akaapa kuwa asingestarehe hadi amtie mtu huyu mikononi. Utafiti wetu ulibaini kwamba Joram hakuwa amewahi kuua mtu tangu aanze kazi ya upelelezi wala leseni yake haikumruhusu kuua isipokuwa katika kujitetea tu. Hata hivyo, aliamua kwamba lazima amuue Proper kwa mkono wake. Joram anasononeka kiasi cha kutamani kumuua Proper mwenyewe. Tunaambiwa, ''aliapa damu ya Neema na wote wasio na hatia waliouwawa na mtu huyu lazima ilipwe. Deni ya damu hulipwa kwa damu'' (uk.81).

Wakati mwingine wapelelezi hulazimika kujificha na kubadili hulka zao ili wasitambuliwe na mhalifu. Mfano mzuri ni pale Joram anapobadili sura ili akae kama mzee, kusudi asitambuliwe na wahalifu. Anabadilisha makao na kuhamia katika nyumba iliyozeeka, kuwafanya watu waamini kwamba alikuwa marehemu. Tunaambiwa:

> Ilikuwa nyumba ambayo kwa muda mrefu haikutumiwa kwa kutokamilika kwake. Joram alikuwa amechagua nyumba hii kujificha baada ya kuitazama mara kwa mara alipopita katika mtaa huu na kuona ilivyokaa vizuri kwa siri (uk 35).

Anapobadili hulka yake na sura, watu wanaomjua vyema kama Inspekta Kombora wanashindwa kumfahamu. Kwanza anajibadili ili wale wanaopanga kumuua wadhani amekufa. Hata ingawa Inspekta Kombora alimfahamu vyema Joram alishindwa kumtambua.. Joram anapojaribu kujitambulisha, Kombora anajiwazia kwamba si huyu mzee aliyesimama mbele yake katika vazi la Kiarabu, kanzu nyeupe, kupiga kilemba, mwenye ndevu ndefu, uso uliofunikwa na miwani na mkono kashika fimbo ambayo ilimsaidia katika mwendo wake wenye dalili zote za udhaifu wa kizee. Mtafiti alibaini kwamba maisha kama haya yanamuathiri mpelelezi kwa sababu yanamzuia kuishi maisha yake ya kawaida. Tunaambiwa:

> Joram akauliza tena. "Naona hujanifahamu Inspekta," ilisema sauti ambayo Kombora aliielekea kuifahamu kwa mbali. "Pengine niondoe miwani na haya madevu ya bandia ili uweze kunitambua (uk32).

Joram anabadili hulka na jina kwa mara ya pili ili kuonekana kama kijana mdogo aliyeziarani Arusha. Mabadiliko haya yanamfanya kukosa nafasi ya kuishi maisha yake ya kawaida kwa vile kila mara yuko njiani kutafuta wahalifu. Mtafiti alibaini kuwa anapumbaza mhalifu Proper ambaye anakosa kumjua. Mfano mzuri ni pale anapoenda Arusha kutafuta mhalifu ambaye alishuku angejaribu kuwaua wajumbe watakaohudhuria mkutano uliotarajiwa. Anaamua kufanya urafiki na Nuru, msichana mrembo anayefanya kazi katika hoteli ile. Alielewa vizuri kwamba Proper alikuwa na tabia ya kutumia wasichana warembo kutimiza wajibu. Wakati wote anapokuwa na Nuru anajitambulisha kama Duncan, anapotokea kumuokoa kutoka mkono wa kifo anakuja katika sura yake halisi ya Joram Kiango. Mtafiti aling'amua kwamba alifanya

hivyo ili atambuliwe na Proper. Proper anasema, "Haiwezekani. Huwezi kuwa Joram. Alikufa kitambo kwa mkono wangu" (uk.119).

Mpelelezi kama mwanadamu yeyote yule hujikuta katika hali ya kutamauka. Joram anatamauka kiasi cha kujaribu kujiua. Anashikwa na hasira sana anapokosa nafasi ya kulipiza kisasi kwa kumua Proper kwa mkono wake mwenyewe. Anapokosa kumuua mhalifu, mpelelezi anatamauka kiasi cha kutaka kutoa uhai wake mwenyewe. Mwandishi anasema, "Hasira mpya zikampanda Joram. Akainua bastola yake na kuielekeza katika kifua chake. Akafumba macho" (uk.122).

Unono anapotumwa na Joram kwa Neema kuchukua habari ambazo zingewafaa kumshika Proper anakutana na kifo chake;. Unono anakutana na mauti anapotoka mbio kwa Neema na kugongwa kwa gari. Tunaambiwa, ''Hakuenda mbali kabla haijatokea gari yenye haraka zake ambayo ilimgonga na kumuua palepale'' (uk.57). Hapa tulionelea kwamba mwanamke huyu alikufa akiwa katika harakati ya kumsaidia Joram kupata mhalifu.

Aidha, utafiti wetu pia ulitufanya tutambue kwamba, kabla hajauawa Neema alikuwa ameponea chupuchupu mara ya kwanza walipokuwa wanachunguza kuhusu vifo vya watu watatu waliodaiwa kuuawa na afisa mkubwa serikalini. Mtafiti alibaini kuwa uchunguzi huo ulifanya maisha ya Neema yawe hatarini, nusura atumbukizwe baharini kama siyo Joram kumuokoa, angalikufa kitambo. Mwandishi anasema:

> Lakini hakufika mbali kabla hajajikuta yuko kati ya watu wanne wenye bastola ambao walimnasa na kumpiga kichwani hadi alipopoteza fahamu. Zilipomrudia alijikuta yuko baharini, katika jahazi, mmoja wa majambazi hao kamshika kichwani mwingine miguuni wakijiandaa kumtumbukiza majini (uk.46).

### 3.4.4 Athari za kijinsia

Utafiti ulitufanya tubaini kwamba wahusika wa kike huumia zaidi katika mikono ya wahalifu. Kwanza kabisa hutumiwa kama chambo na wahalifu wanapotaka kutenda uovu. Wanatumiwa kuwafikia wale wanaofaa kuuawa. Mfano mzuri ni pale Proper anapomtumia Waridi ili kumfikia Joram. Anaumizwa na kumpeleka karibu na baa inayotumiwa na Joram kuburudika. Anatumwa kwa mara ya kwanza lakini mpango wa kuua Joram unakosa kutimia. Mara ya pili anakodishiwa chumba cha kulala, na kununuliwa nguo zinazoonyesha uchi wake ili amvutie Joram kimapenzi. Kazi yake kubwa ilikuwa ni kuhakikisha kwamba Joram amekunywa pombe yenye sumu. Proper anamwambia:

> Ondoa hiyo mikunjo ya hofu uvae sura yako nzuri kama ilivyo. Akija mpe tabasamu, mpe mapenzi, "kisha mkaribishe pombe. Usisahau chupa hiyo hapo ni yake, asipoinywa mpake hii kwa hila (uk.22).

Waridi anatukanwa vibaya sana na kubezwa. Proper anamuahidi kifo asipotimiza wajibu wa kumuua Joram. Anabakwa kwa njia ya kikatili kabla ya kulazimishwa kwenda kuua bila hiari yake. Pia anatishwa kwamba angemshtaki kwa mauaji aliyokuwa amefanya kitambo. Proper anasema: "Huendi hata nikisema kuwa Bomba ni ndugu yangu na ninafahamu alikozikwa?'' (uk.5). Maneno haya yalimmaliza nguvu na hivyo ikampa mhalifu nafasi ya kumdhulumu msichana huyu kimapenzi.

Msichana Waridi pia anabakwa na Proper kabla ya kuuawa. Proper anadharau wanawake na kuwaona kama vyombo vya kutumiwa na kuuliwa. Proper anajifanya mteja na kuingia ndani ya chumba cha Waridi. Anavua kofia ilioficha sura yake ili kuhakikisha Waridi anamtambua kabla ya kumchinja. Anambaka, anamchapa na kumuua kinyama. Anaongezea kuwa, "Unadhani nilikusudia ufe kistaarabu kwa ile

sumu? Ile ilikuwa maalum kwa Joram pekee. Wewe u mwovu mwenye dhambi nyingi unafaa ufe kishenzi” (uk.30).

Wanawake katika riwaya hii wanasawiriwa kama watu walioathirika zaidi kutokana na mauaji haya ya kikatili. Uafiti ulibaini kuwa wapelelezi wanapokuwa katika harakati za kufanya uchunguzi, wengine hulazimika kujisingizia umalaya ili waweze kuingia katika sehemu wasizoruhusiwa kukaribia. Neema wakati mwingine anajifanya malaya ili kugundua siri ya mauaji ya watu watatu. Tunaambiwa, “Ilibidi Neema ajifanye malaya ili aingie katika jumba la mkubwa huyo” (uk.46). Hapo ndipo akapata nafasi humo ndani ya kufanya kila mbinu hadi alipofanikiwa kumzubaisha mtumishi wa mkubwa huyo ambaye bila kufahamu alieleza habari za siri kuhusu mauaji hayo.

Isitoshe wanawake hunajisiwa na wahalifu hao. Proper anampa Neema dawa za kulevya na kumnajisi kabla ya kumuua. Neema baadaye anapoamka kutoka usingizi huo mzito, anaona akiwa uchi. Tunaambiwa, “Alijikuta kalala uchi kando ya Proper ambaye alikuwa kamkamata kwa mkono mmoja wa pili ukichezea chuchu zake” (uk.55).

Neema anasikitika sana na unyonge wake wa kuwa mwanamke, anashindwa nguvu za kujinasua kutoka kwa mkono wa jangili hili. Anajaribu kutoka kwa mkono wake lakini mwanaume huyo anamshinda nguvu na kukosa kuuelewa kilichokuwa kinatokea. Neema anapofoka na kumuuliza kinachotokea, Proper anamcheka tu na kumwambia wanafanya mapenzi. Utafiti wetu ulituwezesha kugundua kwamba, Proper anaona ni jambo la kawaida kufanyia mwanamke mapenzi bila idhini yake. Neema anapomuambia atamshtaki anacheka, kumaanisha kwamba anadharau polisi.

Neema anamwambia, “Umeninajisi.Umenitenda pasi ya hiari. Siwezi kuvumilia”(uk.55).

Proper anamuua Sophie baada ya kutumia nyumba yake kama maficho. Kwa sababu Sophie ana imani na biashara hiyo ya mapenzi, anapumbazwa na Proper anapomuambia kwamba Polisi wakiletwa pale wakimkuta watamshika rafikiye kwa kusema uongo. Mtafiti alibaini kwamba Sofia aliuuawa kwa kupigwa shingo na mhalifu huyo. Tunaambiwa: Sofia alisongeza shingo. Hakutarajia radi iliyompiga ghafla. Lilikuwa pigo kali jepesi ambalo lilitua katika shingo hilo na kulivunja’’ (uk.92).

Msichana mwingine anayeathirika na uhalifu huu ni Nuru. Proper anajaribu kwa mara ya mwisho kumdhulumu Nuru kwa kumnajisi na baadaye kumuua lakini anauawa kabla ya kutekeleza uovu huo. Sumu anayopewa kutumia kuua wajumbe inakosa kufanya kazi. Mtafiti anabainisha kwamba Proper ni kiumbe anayefurahia kutumia wanawake kimapenzi kabla ya kuwaua. Mfano mzuri ni pale Nuru anaokolewa na Joram aliyekuwa anaishi katika hoteli hiyo kwa kutumia jina Duncan. Tunaambiwa Proper alikuwa akimwambia Nuru, “Umekuwa msichana mzuri sana. Hufai kufa bila kuonjwa.” Hapo ndipo Joram alitokea na kuokoa maisha ya Nuru (uk.118). Inabainika wazi hapa kwamba mhalifu huyu alikuwa na mazoea ya kunajisi wanawake kabla ya kuwaua.

### 3.5 Mikakati ya kukabiliana na uovu

#### 3.5.0 Utangulizi

Kulingana na mtafiti, mikakati au mbinu nyingi anazotumia mwandishi kufanikisha upelelezi dhidi ya mhalifu ni mambo ya kawaida yanayoweza kutumiwa na mpelelezi wa kisasa kufanikisha upelelezi. Mtobwa anasawiri mpelelezi anayetumia mbinu za

kisasa kama vile: Vifaa, ishara, wasaidizi, kubadilisha hulka na jina, maarifa, ushirikiano kati ya mpelelezi na polisi kati ya mikakati mingine.

### 3.5.1 Mpelelezi kutumia vifaa

Katika riwaya hii, Ben Mtobwa anamsawiri Joram kama mpelelezi wa kisasa ambaye anatumia vifaa kama bunduki kujinusuru na kupambana na uhalifu. Maisha ya mpelelezi wakati mwingine huwa hatarini hivyo basi hulazimika kujikinga kutokana na mhalifu kwa kutumia silaha. Joram alichukua silaha kila mara alipoenda kufanya uchunguzi kuhusu uhalifu. Mfano mzuri ni pale Joram alipoenda kujificha katika nyumba mbovu baada ya kujisingizia kifo. Alihama usiku wa manane na mzigo wake pekee ulikuwa ni kijisanduku ambacho tunaambiwa, "alichukua vifaa vyake muhimu ikiwa pamoja na silaha" (uk.35).

Wakati Proper alipokuwa anajiandaa kumuua Nuru, Joram alikuwa amejificha bafuni na bastola. Anamkabili Proper na kumwambia kwamba hangemuua Nuru kama alivyotarajia. Proper anashangaa sana kumuona Joram akitokea. Tunaambiwa, "aliwasogelea taratibu sigara ikiwa mkono mmoja, bastola mkono wa pili " (uk.118).

### 3. 5. 2 Mpelelezi hulazimika kubadili sura na hulka

Mtafiti amebaini kwamba Ben Mtobwa anasawiri mpelelezi kama mtu ambaye hufanya lolote kupata habari za kumsaidia katika upelelezi ikiwemo kubadili sura na hulka. Joram analazimika kubadili hulka yake na kuguria katika nyumba mbovu. Imebainika kwamba hiyo ilikuwa siri yake binafsi ingawa Inspekta Kombora alimsihi sana amfahamishe ni wapi angejificha. Alikuwa amehamia hapo usiku wa manane ili kuhakikisha kuwa hafuatwi. Tunaambiwa, "Usiku huo alijiandaa kwa kuvua sura ya ujana na kuvaa uzee" (uk.35).

Anabadilisha jina lake ili kumnasa mhalifu Proper ambaye alikuwa amehamia Arusha. Anajitambulisha kwa Nuru kama Dancun Adolf. Mvulana aliyelelewa Uingereza na babake. Baadaye anaamua kuja kufanya biashara kwao nyumbani. Anajitambulisha kama mzaliwa wa Arusha ambako baba yake aliishi tangu ujana wake. Akaingiliana na watu hapo hotelini na kuwaambia ana mpango wa kuanzisha kiwanda cha utengenezaji wa vipuli vya magari. Mtafiti aligundua kwamba mbinu hii ya kubadili jina ni mbinu inayofanya watu wamuamini na kumpa habari anazotarajia. Proper mwenyewe anashindwa kumtambua kwa mara ya kwanza. Mbinu hii inamwezesha kumnasa Proper na kufanikiwa kuokoa maisha ya wajumbe aliokuwa amelenga kuua. Joram anamuambia Nuru, “Nililazimika kujigeuza sura na umbile kuwa Duncan ili kumdhihirishia huyo kuwa utaalamu wa binadamu kujibadilisha si jambo geni katika nchi hii” (uk.118).

Mpelelezi anatumia mbinu ya kubadili hulka yake na kujifanya ndiye mwenyekiti wa wahalifu, yaani Proper. Anawapumbaza wahalifu ambao wanaropoka bila kujua ni Joram. Baadaye alimwalika Inspekta Kombora ambaye naye pia anakosa kujua ni yeye. Ni pale anapojitambulisha na kusimulia uhalifu wote ambao ulikuwa umetokea ndipo Kombora anatambua kwamba ni Joram. Anapoiondoa nuru ambayo ilikuwa imewanyima nafasi ya kumuona vizuri, Inspekta anashangaa kumuona Joram Kiango ambaye watu walidhani kuwa amekufa. Tunaambiwa, “Joram! Kila mmoja aliropoka kwa mshangao. Hakuna aliyeamini macho yake” (uk.76). Hata Kombora mwenyewe hakuamini macho yake, alibaki ameduwaa hadi Joram anapomwelezea hatua kwa hatua mauaji yaliyokuwa yametokea na jinsi yalivyotekelezwa. Alimpa mwanga Inspekta na kufanikisha kutiwa nguvuni kwa wahalifu hao.

Mtafiti alibaini kwamba mbinu hii ni ya kihalisia katika karne hii inaweza kutumika na wapelelezi chipukizi wa karne hii ya ishirini na moja kuwanasa wahalifu wanaowaua watu ghafla bila kugunduliwa.

### 3.5.3 Ushirikiano kati ya mpelelezi na watu wengine

Kutokana na utafiti wetu, tumegundua kwamba Ben Mtobwa anasawiri mpelelezi Joram Kiango kama mtu asiyetumia miujiza bali ushirikiano na watu wengine kama vile: wasaidizi wake, polisi na wanajamii.

#### 3.5.3.1 Ushirikiano kati ya mpelelezi na wasaidizi wake

Mtafiti amegundua kwamba ushirikiano kati ya mpelelezi na watu wengine ilitumika kama moja ya mikakati ya upelelezi katika riwaya hii. Mtobwa anasawiri mpelelezi Joram kama mtu aliyeshirikiana na mwenzake katika mambo yake yote. Mfano mzuri ni pale anapoamua kumjulisha Neema kuwa atajifanya amekufa ili aweze kufanya utafiti wa kutosha. Neema na Inspekta Kombora walijadiliana kuhusu mipango ya Joram wakati Kombora anapoenda kumjulisha Neema Joram amekufa kweli, haamini. Kombora anapojaribu kumshawishi lakini Neema anacheka. Neema anajibu akitabasamu kwamba: "Hata wewe unajua. Imebidi ajifanye hivyo kwa ajili ya watu hawa ambao wanamtafuta. Muda mfupi atafufuka na jambo ambalo litakusisimua Inspekta" (uk.44).

Mfano mwingine ni pale Joram anapoenda kumtembelea Waridi aliyemwalika hotelini. Alikuwa amemuarifu msaidizi wake (Neema) kwa kusema kuwa, "Yaonekana kuwa hata jana alikuwa na haja nami, hakuwa na majeruhi wala ugonjwa"(uk.22) Mawasiliano hayo yanatudhihirishia kwamba Joram na Neema walishirikiana sana katika mambo ya upelelezi.  Joram alimuelezea Neema hofu yake

kuhusu Waridi hasa alipompigia simu. Anashangazwa na jinsi Waridi alivyotaja jina lake na hata kujipa taabu ya kutafuta nambari yake ya simu. Anamweleza Neema shaka anayotilia Waridi pale anaposema: “Jana alikuwa hoi. Leo anaongea kwa uchangamfu na yuko loji badala ya hospitali! Huoni kama kuna jambo hapo (uk.22)?”Mazungumzo hayo yanatudhihirishia kwamba Joram alipoenda kukutana na Waridi, tayari alikuwa ameanza kumshuku.

Mtafiti alibaini kwamba wakati walipokosa kushirikiana, ndipo Neema alikosea na kumkabili Proper na picha. Unono anatumwa na Joram kumpelekea Neema picha lakini hakumuambia kwamba Joram yu hai. Unono alikuwa amempatia picha tu bila kumfahamisha ukweli kwamba alikuwa ametumwa na Joram. Ukosefu wa ushirikiano huo ulisababishia kifo cha Neema. Unono alipoulizwa na Neema alikotoa picha ya Joram, alisema:

> Inahusiana…Nilipata katika mfuko wa maiti yake dakika chache baada ya kifo chake. Naamini inahusika. Pata maelezo kamili ya picha hiyo. Nikija nitakuelezea lipi zaidi la kufanya (uk.49).

Kulingana na utafiti wasaidizi wa mpelelezi wanapaswa kushirikiana na mpelelezi ili kuepuka hatari ya kuuawa na mhalifu.

### 3.5.3.2 Mpelelezi hushirikiana na polisi

Joram anashiirikiana na Inspekta Kombora kujisingizia kifo baada ya kugundua kwamba Proper anapanga kumuua. Kwanza Kombora anakataa lakini baada ya kusikia jinsi Waridi alivyouliwa kinyama, akaamua kushirikiana na Joram.Wanajadiliana kwa muda, Kombora akawa ameafikiana, japo kwa taabu sana na Joram. Nia yake ilikuwa Joram awaachie polisi kufanya kazi yao. Lakini maelezo ya Joram yanamshawishi hata akakubali ingawa shingo upande. Ushirikiano huo unamlazimisha Kombora kuvunja sheria zingine ili mhalifu ashikwe. Kombora

anamkumbusha Joram kuwa alikuwa akivunja sheria zote na kushiriki katika uongo mkubwa kuhusu kifo chake, ili wapate mhalifu, Kombora anasema: "Hivyo, nakutegemea hutaniangusha kwa kushindwa kuitimiza ahadi yako ya kuwatia watu hawa mikononi mwa sheria" Kombora alisema baadaye (uk.34).

Mtafiti alibaini kwamba Waridia anapodai ameumia na kuita jina la Joram, anaenda nje kuangalia kilichokuwa kimesibu. Kwa maarifa yake anaamua kuwaita polisi waje kumpeleka hospitalini. Tunaambiwa :

> Aliporudi ndani ya baa alienda kibanda cha simu na kuzungusha 999. Sauti ilipomjibu alisema "*Hapa ni Forest of Flowers Bar*…ndiyo Kinondoni. Njooni, kuna mtu wenu anayevuja damu…" (uk.18).

Hapa mtafiti alidhihirishia wazi kwamba Joram aliwasiliana na polisi waje kumchukua msichana huyo. Kwani kwa hekima yake alijua kwamba haikuwa kawaida msichana aliyeumia kuita jina lake amsaidie ilhali kulikuwa na watu wengi pale. Hivyo basi anaamua kushirikisha polisi ili asiingilie mambo asiyoyaelewa vizuri.

Joram anashirikiana na polisi pale anapomuita Inspekta Kombora kuwashika wahalifu wakiwa mkutanoni. Anamuarifu habari zote alizokuwa amepata kuhusu Proper, ikiwemo mpango wa kuwaaua wajumbe watakaohudhuria mkutano kule Arusha. Isitoshe anampa stakabadhi alizokuwa amepata katika hifadhi ya Proper. Joram anasema:

> "Nadhani Inspekta Hujafahamu kiini hasa cha unyama huu.Taarifa kamili imo katika karatasi hizo ambazo nimezipata katika hifadhi zake. Yapitie uone."(uk.82)

Aidha**,** kuna wakati Inspekta na Mkuu wa polisi wanapongeza juhudi za Joram kiasi cha kutamani kumshirikisha katika kikosi chao cha polisi. Katibu Mkuu huyo anamlimbikizia sifa anaposema: "Naona njia zake za upelelezi zimo katika tapo la

kipekee." (86) Wanakubaliana kwa kauli moja kwamba Joram atawafaa sana katika uchunguzi na kuwasaidia kushika Proper. Mkuu wa polisi anapomuuliza Kombora sababu zake za kutomuingiza Joram katika kikosi cha polisi, Kombora anamjibu kwamba: " Joram tumemwambia mara nyingi. Hataki ni mtu apendaye uhuru wake"(uk.86) Utafiti ulibaini kwamba mazungumzo hayo yalidhihirisha ushirikiano baina ya mpelelezi huyo na polisi.

### 3.5.3.3 Ahadi ya tuzo kwa wanajamii

Mtafiti pia alibaini kwamba mwandishi ametumia ahadi ya tuzo inayotolewa na polisi kama mbinu ya kupigana na wahalifu. Wanapoahidiwa tuzo wanajamii wanapewa ari au motisha ya kuangalia kwa makini zaidi binadamu wanaokaa kutiliwa shaka. Aidha, tuzo pia imetumika kama mojawapo ya mbinu za kuwafanya wanajamii kusaidia serikali kuchunguza wahalifu. Mfano mzuri ni pale polisi wanapotangaza kuwa atakaye mtambua Proper atatuzwa. Rafikiye Sofia pamoja naye, wanaanza kumshuku Proper. Huyo rafiki anakimbia kwenda kuwajulisha polisi ili aweze kupata zawadi. Mtafiti alibaini kuwa Sofia ambaye alikuwa mpenziwe Proper, anaanza kumshuku kuwa ndiye mhalifu anayesakwa na polisi. Jioni ya siku ya tatu, mambo yanaanza kwenda mrama pale Sofia anaporejea kutoka mjini na gazeti mkononi. Anamfuata Proper aliyelala chali kitandani na kumfunulia ukurasa wa tatu uliokuwa na picha sita chini ya kichwa cha habari kilichosoma:

> TANGAZO ZA POLISI JIHADHARI NA MTU HUYU-MARA UMWONAPO IARIFU POLISI. ANATAFUTWA KWA MAUAJI YA WATU WENGI.(uk.91).

Matangazo ya aina hii yalimfanya mhalifu ababaike na pia ni njia bora zaidi ya kuwafanya wanajamii kujitahadharisha. Sofia anaposema, "Kweli hata yule rafiki aliyekuja jana amesema hivyo'' (uk.92). Proper anaamua kumuua Sofia. Hii ina

tudhihirishia kuwa alijua atanaswa na hivyo mipango yake haitafaulu. Baadaye Proper anababaika na kutoroka mbio kuepuka mkono wa sheria.

### 3.5.3.4 Wanajamii walishirikiana na wapelelezi

Utafiti wetu uligundua kwamba wanajamii kama Unono walikuwa msitari wa mbele kujaribu kusaidia mpelelezi kupigana na uhalifu. Unono anashirikiana na Joram anapokubali kumpelekea Neema picha ya Proper. Unono anamwambia Neema atafute makazi ya mhalifu huyo. Unono alistahili kurudia habari hizo siku iliyofuata, lakini anaporudi anakutana na mauti.

Mfanyikazi katika kampuni ya habari anamsaidia Neema kutambua picha na makazi ya Proper. Neema anaamua kwenda mjini katika kampuni moja ya habari aliyokuwa ameifanyia kazi hapo awali baada ya kupewa picha na Unono, Huko alipata kijana mmoja aliyetambua picha hiyo kama ya Profesa Chain. Huyo mwenzake alimtazama kwa mshangao na kumuuliza Neema:

> Umeipata wapi picha hii Neema?" "Unamfahamu?" Neema aliuliza kwa matumaini." Wewe, humfahamu huyu? "Alijibiwa kwa swali lingine "Huyu si Profesa Kimara, Kila mtu anamfahamu" (uk.50).

Waridi ambaye ni mwanajamii anampa Joram fununu kuhusu Proper. Msichana anamsaidia kupanga njama ya kujisingizia kunywa pombe yenye sumu iliyokusudiwa kumua. Msichana huyu anapomuona Joram anashikwa na huruma. Anayejua kwamba kijana huyu mtanashati anayepigania haki hakufaa kufa. Hivyo anafungua roho na kumuambia ukweli wote. Mtobwa amesawiri sura ya mpelelezi kama yenye kuaminika na watu. Ndiposa Waridi anapomuona, badala ya kumuumiza kama ilivyokusudiwa, anamwambia ukweli kwa matumaini kwamba

atamnusuru.Waridi anachangia sana upelelezi anaposhirikiana na Joram. Joram anamwambia:

> Najua kinachotokea. Sinywi pombe hiyo. Acha nijifanye nina kunywa ili nimpumbaze huyu anayetaka kuniua. Nitakuomba uwe msiri wangu. Mwache aamini kuwa ameniua, mwache kila mtu adhani kuwa nimekufa.(uk.27)

Sofia kama mwanajamii anachangia sana kutoa fununu kwa polisi kuhusu aliko Proper. Wanaposoma gazeti na kumtambua Proper, rafiki yake anakimbia kumuarifu polisi. Hasa pale wanapoona matangazo kuhusu kutolewa kwa tuzo. Matangazo hayo yanamfanya Sofia atake kuwa na uhakika kuwa ndiye mhalifu. Sofia anasema, “Nina mashaka yule rafiki yangu amekwenda polisi. Laki nne sio pesa kidogo”(uk.92).

Mwanajamii kama vile mwendesha teksi baada ya kujeruhiwa na mhalifu, bado anashirikiana na polisi kuwapa habari kuhusu Proper. Hivyo basi, mtafiti alibaini kwamba, mwandishi anatumia wanajamii kama chombo muhimu cha kupeana habari kwa polisi ili kuwawezesha kupigana na uhalifu. Kwa vile mpelelezi alishirikiana kwa karibu na polisi, wanatumia habari hizo kumfikia Proper.

### 3.5.4 Mpelelezi kujisingizia kifo

Utafiti wetu ulionyesha kwamba baada ya kifo cha Waridi, Joram aliamua kujisingizia kifo ili kufanya uchunguzi wake. Kwa vile alijua kwamba wataendelea na mipango bila hofu, anaamua ni vyema kufanya upelelezi wake kwa siri zaidi, bila kukusudiwa ili kuelewa lengo la mauaji hayo ya kikatili. Anashirikiana na Inspekta Mkwaju Kombora ili kumjulisha mipango ya kumtia Proper mikononi. Joram anaingia afisini kwa Inspekta akiwa amevalia kama mzee ili asijulikane na wengi. Anamuambia Inspekta kiini cha kufanya hivyo, ni wakati huo anapogundua kuhusu kifo cha

Waridi: “Sio mchezo Inspekta. Niko kazini. Unionavyo hapa mimi ni marehemu. Wako watu wameniua. Nataka niendelee kuwa marehemu …” (uk.32).

### 3.5.5 Matumizi ya Ishara

Ben Mtobwa anatumia Ishara kama mkakati wa kunasa wahalifu katika riwaya zake. Moja kati ya ishara anazotumia ni stakabadhi za Proper alizoacha katika nyumba yake alipotorokea Mwanza. Joram alipata taarifa hizo katika karatasi alizotoa katika hifadhi ya Proper. Karatasi hizo zilimpa Kombora ukweli wa mambo kwamba wahalifu hawa walikuwa tayari kufanya lolote. Stakabadhi hizi zinampa mwangaza Kombora na jamii nzima ya polisi. Hapo ndipo askari polisi wakiwemo makachero walipoanza kufanya uchunguzi na kutumia njia zote ikiwemo kujifanya mwoga.

Mtafiti alibaini kwamba ishara nyingine iliyotumika katika *Salamu Kutoka Kuzimu* ni mkufu uliopewa Nuru kama zawadi. Joram anagundua kwamba mkufu huo ulikuwa na kinasa sauti ambacho kilikusudiwa kunasa mazungumzo kati ya Nuru na watu wengine. Proper anajifanya mtu mzuri na kuanza kuwa rafiki ya Nuru. Proper anapomletea mkufu kama zawadi, Joram anagundua kwamba mkufu ule si wa kawaida na kumwonya kwa hekima asiwe mtu mwenye kuchukua zawadi kutoka kwa watu asiowajua vizuri. Joram anamhoji Nuru kwa kumuuliza maswali mengi sana kuhusu mtu aliyempatia mkufu huo. Baada ya kutafakari majibu ya Nuru anagundua kwamba yule ndiye mshukiwa wa mauaji. Joram anasema, “Yule wa jana? Mtu akufuate ghafla. Akuambie kuwa wewe ni mzuri sana, hii hapa zawadi yako” (uk.104).

Nadharia ya uhalisia imetufaa kuangazia wahusika wa kawaida wanaopatikana katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu.* Wahusika hawa ni kama mpelelezi, mhalifu, Waridi na hata kijana Bagambe aliyekufa katika mlipuko wa bomu. Athari

zinazoangaziwa ni mambo ya kawaida yanayokumba jamii. Mihimili ya nadharia hii pia imetusaidia kubaini kwamba athari ya uovu unaozungumziwa na Ben R, Mtobwa na mikakati inayotumika ni ya kisasa na inatumika katika karne hii.

### 3.6 Hitimisho

Sura hii ilitoa maelezo ya jumla kuhusu riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984). Matukio muhimu kutoka mwanzo hadi mwisho yalishughulikiwa. Sura hii pia ilishughulikia sababu mbalimbali zilizosababisha uhalifu wa aina hiyo kutokea katika jamii. Mtafiti alibaini kwamba mazingira yalichukua nafasi kubwa mno katika kuchonga tabia za kikatili za muuaji katika riwaya hii. Utafiti ulidhihirisha kuwa mauaji ya kikatili huwa na athari kubwa siyo tu kwa wanajamii, bali kwa wapelelezi na hata polisi walioshughulikia kesi hiyo. Kwa kusawiri mhalifu akishindwa kufaulu katika malengo yake, mwandishi anadhihirisha kwamba mbinu zilizotumika zinaweza kufaa jamii yoyote ile kupigana na uhalifu. Isisahaulike kwamba, maswala haya yalijadiliwa kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia. Kwa vile matukio mengi yaliyozungumziwa na mwandishi hutokea katika mazingira yetu kwa mfano tukio la mauaji la wachimba migodi Kaskazini Mashariki mwa Kenya 2/11/2014. Uovu ni changamoto inayokumba jamii ya sasa. Kwa kuzungumzia sababu za mwanadamu kugeuka kuwa muuaji hutupa nafasi ya kutafakari na kuepukana na mambo yanayofanya maovu hayo kushamiri katika jamii. Wale wasiojitahidi kupinga uovu, huchangia katika kuleta hali ya taharuki katika jamii zetu. Katika sura ifuatayo tulionyesha namna uovu hasa mauaji ya kikatili yalivyosawiriwa katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu (1987).* Mtafiti alibaini kwamba riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu* inaendeleza hadithi ya uhalifu inayopatikana katika *Salamu Kutoka Kuzimu*. Tutaona anavyosawiri tatizo hili na mikakati iliyotumika kukabiliana na uovu.

# SURA YA NNE

# MAUAJI, ATHARI ZAKE NA MIKAKATI YA KUANGAMIZA UOVU KATIKA RIWAYA YA *TUTARUDI NA ROHO ZETU*.

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu* (1987). Mtazamo wa Mtobwa kuhusu kiini, athari ya mauaji ya kikatili na mikakati ya upelelezi iliyotumika katika riwaya hii. *Tutarudi* na *Roho Zetu* ni mojawapo ya harakati za Joram Kiango. Yeye ndiye mpelelezi mkuu wa kujitolea kwa ajili ya kukomesha uovu na ufidhuli nchini Tanzania. Joram anatumia mbinu zote za upelelezi ili kuokoa nchi ya Tanzania na nafsi yake mwenyewe. Riwaya hii ni mwendelezo wa *Salamu Kutoka Kuzimu* ambapo baada ya kifo cha Neema, Joram anaamini kwamba mhalifu hakufa mikononi mwake kama alivyotarajia. Hapa tunamwona Joram akitamauka kiasi cha kuanza kukata tamaa kuhusu kazi ya upelelezi. Anapogundua kwamba uhalifu uliomkabili ulikuwa unahatarisha maisha yake na ya watu wengi wasiokuwa na hatia, anaamua kuyakabili kwa kutumia mbinu zote.

### Muhtasari wa hadithi katika *Tutarudi na Roho Zetu*

Riwaya hii inaanza wakati ambapo Joram Kiango na Nuru wameamua kuwa watumiaji wazuri wa fedha. Wanatembea kutoka jiji hadi jiji wakiponda mali. Inspekta Kombora anamsihi Joram arudi kazini lakini Joram anakataa. Anaamua kuishi maisha ya kivivu na mpenziwe Nuru. Joram anahisi amenyimwa nafasi ya kutia risasi katika kichwa cha Proper. Wanatembelea miji ya Zanzibar, Dodoma na Mwanza. Anasa hii yote haimpi raha. Baadaye Nuru anajaribu kumshawishi arudi kazini lakini Joram anakataa. Anaposikia habari kwamba Samora ameuliwa katika

ajali ya Lagos na Benki Kuu ya Tanzania ikachomwa Joram hatishiki. Walishuku kwamba ni nchi ya Afrika Kusini ndiyo iliyohusika lakini hawakuwa na njia ya kuthibitisha jambo hilo. Vifo hivyo vyote vinawaacha katika hali ya taharuki.

Kilele cha hadithi ni pale Joram anapokutana na Chonde; ambaye tunagundua ni jasusi na mmoja kati ya wauwaji waliotumwa na Von Iron kutekeleza uhalifu. Joram anashangazwa na maswali ya Chonde hasa pale anapomwita kwa jina. Joram anaamua kufanya utafiti zaidi kuhusu Chonde ambaye alimshuku kuwa jasusi. Utafiti wake unamwezesha kupata habari kutoka kwa msichana anayepokea wageni hotelini. Anaambiwa kwamba Chonde anaishi 'Hotel Africa' chumba nambari 104. Anaamua kufulilizа hadi kule 'Hotel Africa' ambapo upekuzi wake unamfanya kugundua kwamba yule jamaa anaitwa Chonde na alikuwa amesafiri katika nchi nyingi duniani. Anafumaniwa na Chonde akiwa anajaribu kufungua sanduku lake. Anapotoka pale anatambua kwamba maisha yake yamo hatarini. Ugunduzi huu unamfanya Joram kuamua kwamba ni lazima awatafute adui hawa ili ajue lengo lao kuu.

Joram anakutana na Chonde kwa mara ya pili ambapo wanahojiana hapa na pale. Joram anamtuma msaidizi wake kwenda kupekua vitu vya Chonde. Msaidizi huyo analipuliwa kwa bomu wakati akijaribu kufungua sanduku la Chonde. Hapo ndipo Joram anaamua kwenda kumkabili Chonde. Chonde anamwelezea ukweli wote kwamba ni adui wake na kujaribu kumuua kwa bunduki. Joram ananusurika kifo baada ya kuokolewa na Nuru dakika chache kabla Chonde hajafyatua risasi. Joram anachukua kijisanduku cha Chonde na kutoroka nacho. Baada ya kusoma taarifa inayomdhihirishia hofu yake yote, anaamua kutoroka kutoka Tanzania kwa kujisingizia uhalifu.

Joram na Nuru wanatorokea Jijini Nairobi. Wanabadilisha majina na hata hulka zao. Hapo ndipo Joram anaanza mipango maalum ya kijasusi kuhusu ukombozi wa

Tanzania kutokana na uhalifu. Mpelelezi huyu anapoelewa kuwa Tanzania imekuwa na maadui hatari kutoka nje ya Tanzania, anaamua kutoamini mtu yeyote. Anachukua nafasi kusoma na kufanyia utafiti taarifa na vifaa alivyopata katika kijisanduku cha Chonde. Joram na Nuru wanatoroka kutoka Tanzania ili kupata nafasi nzuri ya kufanya uchunguzi zaidi.

Aidha Joram anatembelea maktaba za London na kulazimika kumshirikisha Nuru amsaidie katika upekuzi wa habari. Wakati huo huo, kuna mamluki kwa jina Kweza anayeshikwa Tanzania na polisi akiwaameficha silaha na vyombo vya mawasiliano. Anamwambia Inspekta Kombora wazi kwamba Tanzania itawaka moto na kwamba mwenye akili anafaa kutoroka.

Joram na Nuru wanafanya utafiti katika miji mbalimbali duniani. Wakati huo Joram anajifanya mhalifu kiasi cha kufanya watu waamini kuwa ameacha kazi ya upelelezI. Dunia nzima ikiwa inamtafuta, anajaribu kumshawishi Nuru arudi Tanzania ili asidhurike maanake kazi iliyokuwa mbele yake ilikuwa hatari. Nuru anakataa uamuzi huo na kuapa kumsaidia Joram hadi mwisho.

Wanapoenda Afrika kusini wanakutana na Makaburu wanne wakiwa wanasikiliza habari za kijasusi. Kwa mara ya kwanza, Joram wanakutana na kiongozi wa wahalifu ajulikanaye kama Von Iron. Yeye ndiye mkurugenzi mkuu wa shirika la kijasusi Afrika Kusini. Mtafiti amebaini kuwa Von Iron ndiye aliyebuni uwezekano wa kutumia nguvu za kinuklia kuangamiza Waafrika. Anabuni mpango wa kuwepo majasusi Makaburu waliovikwa ngozi nyeusi ili kupenya Tanzania kufanikisha mipango yake potovu ya mauaji. Tunapata taswira kuhusu hali ilivyo Afrika Kusini na mipango ya kuangamiza Tanzania ambayo waliamini ni chimbuko la msukosuko wote dhidi ya utawala wa Makaburu.

Mtafiti amebaini kuwa Von Iron ndiye mhalifu mkuu aliyemtuma Chonde na hata Kweza nchini Tanzania. Falsafa ya Von Iron ni kwamba mtu mweusi anafaa kuangamizwa kwani yeye ni chombo cha mtu mweupe ambacho hakina thamani. Ni wakati huu ndipo Joram anawasili Afrika Kusini kwa kisingizio kwamba ni mhalifu na mtoro wa Tanzania. Joram anathibitisha kwamba mauaji yote yaliyokuwa yakitokea katika nchi ya Tanzania yalipangiwa Afrika Kusini. Inspekta Kombora na kundi lake la askari wanamshika Clay ambaye alikuwa ametumwa Tanzania kutega mabomu katika majengo kadhaa nchini humo ikiwemo Ikulu.

Wanapoenda Afrika Kusini Joram na mpelelezi mwenzake walikuwa wamejiandaa vya kutosha. Baada ya kusoma taarifa waliopata katika kijisanduku cha Chonde, waliamua kujitolea kwa hali na mali kwenda Afrika Kusini. Joram alikuwa amemuandaa Nuru kwa kila hali ikiwemo kufyatua bunduki hadi kupiga judo. Ingawa Joram na Nuru wanajifanya watoro kutoka Tanzania, wanawekwa katika chumba kilichotengwa. Hapo wanawekewa ulinzi mkali ili wachunguzwe zaidi. Joram na Nuru wanatoroka kutoka nyumba hiyo na kutega mabomu katika majengo muhimu jijini Johanesburg. Baadaye askari wa Von Iron wanamshika Joram na kumfungia katika chumba cha kuua watu. Von Iron anamchukua Nuru na kumweka afisini mwake kwa lengo la kumwonyesha jinsi nchi yake inavyoangamia wakati ukifika.Von Iron anaamua kumnajisi Nuru kabla ya kumuua. Hapo ndipo Nuru kwa ujanja wake anapata nafasi ya kumpumbaza na kumuua Von Iron kwa bunduki. Msichana huyu anakimbilia katika chumba cha mauaji na kumuokoa Joram. Wanatoroka baada ya kumuua mhalifu Von Iron na kuharibu mtambo uliotegwa na Makaburu kuangamiza Watanzania. Joram na msaidizi wake Nuru wanarudi Tanzania na roho zao. Hapa tunaona jinsi mwandishi anamsawiri mwanamke kama msaidizi anayeweza kuokoa nchi anaposhirikishwa.

### 4.1.0 Kiini cha uovu

Mtafiti amebaini kwamba Ben R. Mtobwa anatuangazia mambo kadha wa kadha ambayo yanasababisha uovu katika jamii. Kwa mujibu wa mtazamo wake mtafiti alikuwa mwenye maoni kwamba mazingira yamepewa nafasi kubwa sana ikifuatwa na siasa na ubaguzi wa rangi.

### 4.1.1 Mazingira kama kiini kikuu cha maovu

Mtafiti amebaini kwamba kulingana na mtazamo wa Ben R. Mtobwa, wahusika wakatili wanaoshiriki sana mauaji wamesawiriwa kama watu wanaochochewa na mazingira anamoishi mwanadamu. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu*, kuna wauaji wa aina tatu. Kwanza, kuna Von Iron mhusika aliyechochewa na mazingira, pili kuna muuaji mtaalamu mwenye uhayawani au kichaa cha kuua na tatu kuna wauaji wanaoua ili kujinusuru. Mtazamo huu wa Ben R.Mtobwa unaafikiana mawazo ya Bandura (1977) kuhusu athari ya tajriba za maisha ya utotoni katika maisha ya utu uzima.

Mhusika Von Iron anayesawiriwa kama binadamu aliyechochewa na mazingira kuwa mtu mwenye roho mbaya na roho ya unyama kiasi cha kuwa muuaji mkuu wa kupanga mauaji na kutekeleza mengine kivyake. Anajiona kama kiumbe aliyenyimwa haki ya malezi akiwa mtoto. Anashuhudia babake mzazi akimuua mamake. Baadaye babake anajitoa uhai na kumuacha akiwa yatima. Mateso ya kiakili aliyokuwa nayo kutokana na tukio hilo hayakumtoka hata katika utu uzima. Anaishi kuwa mtu asiyethamini maisha ya binadamu. Mipango yote ya mauaji yanayotokea kwa sababu ya mikakati inayopangwa na Von Iron. Furaha yake kuu inakuwa ni kuona watu wakifa, hasa anapowatoa uhai watu weusi.

Mtafiti amebaini kwamba, mwandishi anasawiri Von Iron kama binadamu anayejisikia kusheherekea kila chozi linalotoka katika uso wa mtu mweusi. Kifo cha wazazi wake hasa mamake kinamfanya kuchukia binadamu wa Kiafrika. Ni ndoto na tamaa yake kuu kuweza kuwaangamiza Waafrika wote. Anakuwa muovu kiasi cha kutamani kumbaka msichana wa Kiafrika. Anapomuona Nuru, anaona nafasi nzuri ya kufanya ukatili huo. Mwandishi anasema:

> Alihitaji kuijua siri iliyomo katika ngozi hii nyeusi. Siri iliyomfanya kukosa baba na mama milele. Baada ya hapa ndipo Nuru atamfuata Joram ahera ( uk.125).

Mawazo yake ni potovu na yanayokosa utu kabisa. Anakuwa na shida ya akili, akili iliyojaa uozo. Anapomuona Joram anafurahia sana kwani anajua amepata nafasi ya kumfanya ashuhudie nchi yake ikiteketea na baadaye amuue. Mwandishi anasema kuwa wakati huu wote alikuwa akiwaza jinsi atakavyomchinja na ashindwe la kufanya. Von Iron anaona ikiwa imebaki saa chache sana amlete Joram katika chumba kilicho na televisheni ili atazame nchi yake inavyoteketea. Tunaambiwa anawaza kwamba : ‘‘Baada ya haya tutamchinja kwa urahisi kama kondoo’’ (uk.124). Von Iron anazungumzia kitendo hicho kama jambo jepesi lisilokuwa na uzito wowote. Matamshi hayo yanadhihirisha kwamba swala la kuchinja mtu halikuwa jambo geni kwake Von Iron.

Ben R. Mtobwa anamsawiri Von Iron kama mtu mwenye ukatili kiasi kwamba ukatili wake unawatia uwoga wakubwa wake. Anapopanga kuweka mtambo uliofaa kuwaangamiza Waafrika katika nchi kadhaa, wanajaribu kuupinga. Mpango huo uliotokana na ubunifu wake Von Iron na ulipita kwa taabu sana. Wakubwa wake walikuwa wamelalamika kwamba, mpango huo ulikuwa wa kikatili mno. Mwandishi anasema kwamba, ‘‘Lakini yeye Von Iron na wenzake wachache walijaribu kuwashawishi. Von Iron anakuwa mbaguzi wa rangi namba moja’’ (uk 125).

Siku inapokaribia ya mtambo uliokusudiwa kuwaua Waafrika kulipuka, tunaambiwa kuwa Von Iron anacheka kwa furaha. Chuki yake dhidi ya watu weusi inamfanya awatendee maovu bila kusita. Anapokuwa akimrai Nuru afanye mapenzi naye, anamtafadhalisha na baadaye anajishutumu sana kwa tukio hilo. Tunaambiwa, ‘‘Von alijilaumu kwa kutamka neno hilo. Vipi amtafadhalishe mtu mweusi’’ (uk.143).

Makaburu wenzake wanajaribu kumshawishi kuwa Joram auwawe mapema lakini anakataa kuwasikiliza. Kulingana na Makaburu hao, kumwacha mpelelezi hodari kama Joram akiwa hai ilikuwa sawa na kujifungia na nyoka chumba kimoja. Lakini Von Iron hakudhamini maoni yao lengo lake ilikuwa ni kumfanya Joram na Nuru wahisi uchungu wanapoona nchi ya Tanzania ikiangamia.

Isitoshe, Von Iron anamuua mtu yeyote anayejaribu kuharibu mipango yake ya mauaji. Mwandishi anasema kuwa kuna mmoja kati ya wahandisi wake aliyewahi kupoteza maisha baada ya kushukiwa kuwa alikuwa na dhamira mbaya kwa mtambo wake. Anafanya kifo cha mhandisi huyo kuonekana kama ajali iliyosababishwa na dereva mlevi kugonga mtu anayetembea kando ya barabara. Hapa inabainika kwamba Von Iron ni mtu aliyechukulia maisha ya binadamu kuwa kitu kidogo sana. Angeweza kutoa mwenzake uhai na kutupa maiti yake barabarani kama mzoga wa mbwa (uk.147).

Mipango yote potovu ya kuua watu wanaopinga uongozi wa Makaburu ilifanywa na Von Iron. Von Iron anajenga chumba cha kuwaua watu, hasa wengi wanaotupwa mle wanakufa kwa njaa. Mtafiti amebaini kwamba maiti zilikuwa zimejaa mle ndani zingine zikiwa zimeoza. Aidha, maiti hao hawakuzikwa. Miili hiyo inaliwa na panya ambao tunaambiwa, walikuwa wamenona ungedhani ni paka. Joram anatupwa mle ndani ili afe lakini kwa bahati nzuri anaokolewa na Nuru.

#### 4.2.2 Mauaji katika misingi ya kisiasa

Afrika Mashariki inaongoza mashambulizi katika miji kadha barani Afrika ili kuwaogofya dhidi ya kutetea wenzao wa Afrika Kusini. Chonde anamtania Joram na kumuambia kwamba Afrika iko katika mashaka makubwa. Anamsisitizia kwamba watu wanakufa ovyo, majumba yanalipuka ovyo na bara zima liko mashakani. Anajifanya mwananchi anayejali sana maslahi ya Tanzania. Anamuuliza Joram sababu za kunyamaza wakati watu wanaumia. Chonde anasema : "Joram ninayemfahamu mimi angeitoa roho yake kujaribu kupambana na hali hii" (uk 23). Mtafiti amebaini kwamba ni Chonde aliyekuwa ametega bomu katika sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki.

Aidha, imebainika kwamba Chonde alikuwa mmoja wa majasusi wa Von Iron waliotumwa kuharibu na kuwatia uoga wananchi katika nchi kama Tanzania. Utafiti wetu umebainisha kuwa Chonde alikuwa anaelewa siri kubwa iliyokuwa inafanya vifo vya watu wengi vishuhudiwe nchini. Anaelezea kuwa ni siri kubwa inayohusu Afrika na dunia nzima.

Baadaye mtafiti amebaini kwamba siri hii ilikuwa mtambo uliokusudiwa kulipua Tanzania. Kulingana na Chonde ilikuwa siri nzito kuliko bara nzima la Afrika. Kwa maneno mengine ni siri ambayo dunia nzima ilikuwa ikipigania kujua. Chonde anamwambia Joram kwamba siri hiyo ilikuwa inafahamika na watu wachache sana. Chonde anasema kwamba: ''Watu ambao walishona midomo, hawangeweza kusimulia hata maiti siri hiyo'' (uk.46). Mtafiti amebaini kuwa Chonde alikuwa akizungumzia mambo ya kisiasa kwani, yalikusudiwa kuhifadhi uongozi wa Makaburu.

Isitoshe, mtafiti amebaini kuwa Ben R. Mtobwa amesawiri mauaji yanayosababishwa na mvutano wa kisiasa na kutekelezwa na wauwaji wakatili. Imebainika kwamba wahalifu hawa walichochewa na mazingira ya malezi yao. Wahalifu hawa wanajihusisha na uhalifu kama vile kutega mabomu na kulipua wenzao kwa risasi. Wengine wanajitekelezea ilhali binadamu kama Von Iron anakodi watu wakatili kutimiza malengo yake ya kuua. Kwa mfano Clay ni muuaji anayemfanyia Von Iron kazi ya kuua, wanatumwa nchini Tanzania kutega mabomu na kuua watu wasiokuwa na hatia. Haya yote ni kuwalazimisha Watanzania wabadili msimamo wao wa kutetea Waafrika wa Afrika Kusini. Mtafiti ameng'amua kwamba Tanzania kuacha kusaidia nchi zinazopigania haki na uhuru wake ilikuwa ndoto ambayo kamwe isingetokea. Tunaambiwa:

> Lakini kuendelea kusaidia nchi hizo huku ukisubiri maafa ya hatari sana, kwa nchi yake na rafiki zake hali huna uwezo wa kufanya lolote ilikuwa ndoto ya kusikitisha sana. Ndoto ambayo ingeweza kutokea (uk 80).

### 4.2.3 Mauaji ya kujinusuru

Nuru anamuua Chonde kumuokoa Joram ambaye ndiye mpelelezi mkuu. Ben R. Mtobwa anasawiri Nuru kama msichana jasiri. Mfano mzuri ni pale anapomuua Chonde ambaye alikuwa tayari kumfiatulia Joram risasi. Anafika kwa wakati na kumuua Chonde ambaye kifo chake kinamwezesha Joram kupata fununu kuhusu hatari iliokuwa ikiikabili nchi ya Tanzania. Tunaambiwa, ''Joram alipojiinua na kuchungulia ikamshangaza kumuona Chonde kalala chini kifudifudi damu ikivuja anasema, Nuru! Nawezaje kukushukuru Nuru?" (uk.47). Kulingana na mtafiti, Nuru anasawiriwa kama mwokozi mkuu wa Tanzania na malaika anayejitokeza hasa anapohitajika. Aidha, mtafiti amebaini kwamba katika jamii ya Waafrika mwanamke huchukuliwa kama kiumbe dhaifu asiyeweza kuhusishwa na majukumu mazito.

Hivyo basi, mwandishi amempandisha cheo mwanamke kwa kumsawiri kama jasiri anayemsaidia mpelelezi kufanikisha vita dhidi ya uhalifu.

Nuru anamuua Von Iron kwa kutumia bunduki ili kuokoa maisha yake na ya Joram. Von Iron anajikuta akiwa amelengwa na bastola yake mwenyewe, Nuru anamwambia Von Iron, "Pokea chako muuaji mkubwa," Nuru alionekana akifyatua bastola (uk 159). Anapomaliza kumuua Von Iron, anachukua funguo kwenda kumuokoa Joram. Kitendo cha Nuru kinamwezesha kuokoa maisha yake na Joram. Wanapata nafasi ya kuharibu mtambo uliokusudiwa kuangamiza Tanzania.

### 4.2.4 Ubaguzi wa Rangi

Ubaguzi wa rangi unasawiriwa kama sababu nyingine kuu ya mauaji katika riwaya hii. Mhalifu Von Iron anawachukia sana watu weusi. Joram mwenyewe anajua kwamba weusi walikuwa wamebaguliwa kiasi kwamba Makaburu walikuwa na kiu ya kuwaua. Anamwambia Nuru kwamba watu hao walikuwa kiuu ya kuwaondoa uhai. Anamwelezea hayo yote anapokuwa anajaribu kumshauri asimfuate kule Afrika Kusini. Anasema, ‘‘Ni nchi ambayo kuna watu wenye kiu kubwa ya damu ya mtu mweusi’’ (uk.88).

Von Iron ndiye aliyekuwa msitari wa mbele kuandika mpango wa kuwaangamiza Waafrika. Ukatili wake ulifanya apewe cheo hicho cha kupanga mipango ya kuwaangamiza Waafrika. Hii ni kwa sababu alijulikana kuwa anawachukia Waafrika zaidi kuliko mtu yeyote. Mtafiti amebaini kwamba, taarifa ya kijasusi iliyopatikana katika kijisanduku cha Chonde, ilikuwa imeandikwa na Von Iron. Anawatuma Chonde, Kweza na Clay kwenda kutega mabomu katika sehemu tofauti za jiji la Dar es Salaam ili kuwaua Waafrika. Hisia zake za chuki zinamfanya atamani kuangamiza

Waafrika wote. Tunaambiwa, ‘‘Ni yeye aliyebuni uwezekano wa kutumia nguvu za kiniuklia kuangamiza mwafrika’’ (uk.98).

Mtangazaji mmoja wa televisheni anawabeza sana Waafrika na kuwakashifu wakati Joram na Nuru wanapowasili Afrika Kusini. Maneno yote anayoyesema ni kumdunisha mtu mweusi. Joram na Nuru wanapowasili, Von Iron anawaona kama viumbe weusi wanaopenda tu kufa.

Von Iron anajilaumu kwa kumtafadhalisha Nuru, kwa kuwa ni mtu mweusi. Von Iron anajilaumu sana kwa kutamka neno hilo. Anashangaa sana vipi angemtafadhalisha mtu mweusi (uk.143)? Kulingana na habari hii, mtafiti amebaini kuwa Von Iron anachukia sana Mwafrika. Mtafiti amedhirisha kuwa Von Iron ni mwenye imani kwamba watu weusi ndio waliomfanya kuwa yatima.

**4.3 Utekelezaji wa mauaji**

Katika riwaya hii ya *Tutarudi na Roho Zetu*, Ben R. Mtobwa anatupa taswira ya mauaji ambayo ni ya kikatili zaidi katika ulimwengu wa sasa. Mifano ni mauaji ya kutumia bomu kama yale yaliyotekelezwa na Chonde na Clay. Chonde anatumia bomu kumuua Edward (uk.44). Kuna watu wanaoliwa kwa hila kama askari wa benki aliyepatikana akielea baharini pwani ya Magomeni (uk.15). Wengine wanaouliwa kwa kuchomwa na moto ambao haukueleweka chanzo chake. Watu mia nne wanafariki na mia tisa kujeruhiwa uwanjani Lagos Naijeria bila yeyote kushikwa. Tunaambiwa, “Uchunguzi unaonyesha kuwa utawala wa Afrika Kusini unahusika” (uk.8-9).

Isitoshe, watu wengine walikufa kutokana na ajali zisizoeleweka jijini Dar es Salaam. Mwandishi anasema kwamba viongozi wanane wa vyama kadhaa vya wapigania

uhuru wa Afrika Kusini na mwakilishi wa PLO nchini Tanzania ambao walikuwa wakikutana kwa faragha katika jengo moja walifariki ghafla katika moja ya ajali hizo zisizoeleweka. Tunaambiwa, "Alikufa kwa moto ambao ulilipuka ghafla katika chumba chao cha mkutano" (uk.13). Hakuna aliyefahamu kikamilifu kilichosababisha moto huo. Vifo hivi vyote vilikuwa vimeandaliwa na Von Iron ambaye anatuma mawakala wake kuyatekeleza.

Kuna watu ambao wanaachwa kufa kwa njaa kwa amri yake Von Iron. Wale waliopinga mipango yake au hata kujaribu kwenda Afrika kusini kufanya ujasusi kuhusu hasa mipango yao, wakawa wanateseka hadi kufa kutokana na majeraha na njaa. Tunaambiwa, ''Mrusi huyo alikuwa mmoja kati ya watu wengi ambao walikuwa wakiuawa baada ya kushukiwa kuwa walikuwa wakifanya upelelezi'' (uk 162).

Utafiti wetu ulibaini kwamba kuna watu wanaouliwa kwa bunduki kama vile mhandisi aliyeuliwa na Von Iron (uk.147). Baadaye anamkanyaga kwa gari ili kuwafanya watu wadhani kwamba ni mlevi aliyekanyagwa na gari tu. Chonde alipokuwa ameshika bunduki tayari kumuua Joram, ilidhihirisha kwamba alikuwa mtaalam wa kuitumia kutoa watu uhai. Tunaambiwa, "Chonde kaielekeza bastola katika kifua cha Joram, kidole chake kiligusa kiwamo cha kufiatulia risasi" (uk.47). Wahandisi waliouliwa kwa bunduki wakati wapelelezi wakitafuta mwanya wa kutoroka, walikuwa wameduwaa walipofiatuliwa risasi.

Nadharia ya maadili imetusaidia sana kuangazia uovu unavyojitokeza katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa na hasa sababu kuu zilizochochea tabia hii. Mtafiti amebaini kwamba Ben Mtobwa anatumia riwaya zake teule kuweka wazi uovu huu ili kuukemea usipotoshe jamii. Anapotuangazia jinsi mpelelezi na polisi wanavyopigana na uovu huo, anatudhihirishia kwamba uovu huo unafaa kuepukwa au kumalizwa.

### 4.3.0 Athari za mauaji ya kikatili

Mauaji ya kikatili huathiri mpelelezi, jamii kwa jumla na hata polisi ambao kazi yao kuu ni kulinda usalama. Tumeelewa kwamba kunapotokea mauaji ya kikatili, watu mbalimbali huathirika kwa njia moja au nyingine. Aidha tumeangalia kwa kina jinsi ambavyo kila mmoja huathirika.

Maisha ya mpelelezi huwa hatarini. Joram ananusurika kifo mara tatu katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu.* Kwanza anapokabiliana na mhalifu ajulikanaye kama Afith Chonde, nusura amuue alipomfumania akipekua vitu vyake chumbani. Ananusurika kifo tena pale msichana mfanyikazi wa hotelini anapobisha mlango wa Chonde. Joram anapoenda kumwangalia Edward katika chumba cha Chonde, anamkuta kauawa kwa bomu. Baadaye Chonde anamwelezea Joram kwamba ni lazima afe kwa kuwa alikuwa amegundua siri nyingi. Wakati Chonde anapokuwa karibu kumpiga risasi Joram, Nuru anatokea na kumuua Chonde. Tunaambiwa Joram anamshukuru sana Nuru kwa kuokoa maisha yake. Joram anasema: "Nuru! Nawezaje kukushukuru Nuru" (uk.47)? Matamshi haya ni dhihirisho tosha kwamba Joram alikuwa mwingi wa shukrani.

Mara ya tatu Joram ananusurika kifo akiwa Afrika Kusini. Mwandishi anamsawiri mpelelezi kama mtu anayenusurika kifo mara kadhaa. Mfano mzuri ni pale Joram anapotupwa katika chumba cha mauaji. Watu wengi walikuwa marehemu chumbani humo isipokuwa Mrusi mmoja. Mrusi huyo kabla hajafa, anamshawishi Joram ajikaze apigane hadi awanusuru wananchi wasiokuwa na hatia. Joram anajaribu kufungua mlango huo kwa kutumia bastola lakini risasi inaanguka ardhini kama gololi. Hapo ndipo anaambiwa na Mrusi jinsi watu hufia humo kinyama baada ya kushukiwa kwa kujaribu kupeleleza dhidi uongozi wa Makaburu. Joram anagundua kwamba pango

hilo lilikuwa limechimbwa maalum kwa kuwaangamiza watu kwa siri (uk.162). Wenzake wote wanakufa ila Joram anayeokolewa na Nuru.

Aidha mtafiti alibaini kwamba, wapelelezi hulazimika kuingia sehemu ambazo ni hatari ili kupata habari. Mpelelezi Joram anasawiriwa na Mtobwa kama mtu anayejitolea kuokoa nchi yake bila kujali maisha yake. Anasema, "Matumaini yake ya kurudi ilikuwa ndoto isiyo na hakika'' (uk.133). Mwishowe Joram alipogundua kwamba anafuatwa, anamuomba Nuru abaki nyuma. Anamwambia Nuru kwamba anataka kuulipua mtambo huo kabla madhara waliyoyandaa katika jiji la Johannesburg kutokea.

Isitoshe, mpelelezi wakati mwingine hulazimika kubadilisha hulka, sura na jina lake ili kufanya uchunguzi wake. Mtafiti alibaini kwamba mabadiliko kama haya yanaathiri maisha ya kawaida ya mpelelezi. Kwa mfano Joram anapokuwa anasafiri kwenda nchi za nje kama Nairobi Kenya na Afrika Kusini, anabadili jina na sura. Ben Mtobwa anasawiri wawili hawa kama watu waliokuwa tayari kufanya lolote kufikia malengo yao ikiwemo kubadili sura. Mwandishi Mtobwa anasema mtangazaji mmoja alisafiri hadi Nairobi ambako utafiti wake ulimfikisha katika chumba alimokuwa Joram na Nuru kwa majina bandia. Anaandika katika gazeti kwamba, Joram alikuweko London wakati huo. Gazeti hilo lilieleza kuwa, "Dunia haiwezi kupumbaza na hila zake za kubadilika sura na umbile '' (uk 74)? Mtafiti alibaini kwamba mpelelezi huyu alilazimika kubadili sura na hulka ili aweze kupenya sehemu ambazo hangeruhusiwa kuingia.

Tuliona jinsi ambavyo mpelelezi Joram anatamauka kiasi cha kuamua kuishi kivivu. Kula, kunywa na kuburudika ilikuwa ndiyo kazi kubwa waliofanya kwa wiki mbili. Mfano mzuri ni pale Joram anapokosa nafasi ya kumuua Proper, anapoteza matumaini

kiasi cha kutamani kujiondoa uhai. Maovu yanatokea mengi lakini hali hii inamfanya Kombora kumshawishi arudi kazini lakini anakataa. Joram anakasirika na Kombora anapomshauri kuhusu ulevi. Ndipo Kombora akamwambia:

> Hapana. Wewe si mlevi na wala huwezi kuwa mlevi. Ni mnywaji tu. Mnywaji ambaye hanywi kwa ajili ya kupenda kunywa, isipokuwa hasira baada ya kunyang'anywa fursa ya kuitia risasi kwa mkono wako katika kichwa cha yule mshenzi. Sivyo Joram ? (uk.18)

Taarifa hii inaonyesha kwamba alikuwa ametamauka sana baada ya kutolipisha kifo cha Neema. Maneno hayo ni majibu yanayotolewa na Joram anapojaribu kushawishiwa arudi kazini. Mtafiti alibaini kwamba maneno ya Kombora yanatufanya tuelewe kiini hasa cha unywaji huo wa Joram.

Mpelelezi huumizwa kutokana na vichapo vya mhalifu. Joram anapokea kichapo cha mbwa anapoenda katika chumba cha Chonde. Lakini jinsi hivyo vipigo vilivyopigwa kwa hasira, havikuwa na madhara makubwa. Mara ya kwanza anapigwa sana alipojipeleka katika chumba cha Chonde kuchunguza ili aweze kujua ni mtu wa aina gani. Anapigwa tena kwa mara ya pili pale anaporudi katika chumba cha Chonde akiwa na matumaini ya kumuokoa Edward. Anafumaniwa na Chonde ambaye anampiga nusura amuue. Kwa dakika chache baadaye Joram alijikuta chali sakafuni kasalimu amri. Chonde anaendelea kutabasamu, naye Joram akawa anamtazama kwa mtazamo wa hasira zaidi. Mwandishi anasema: "Joram alishangaa na kujiuliza, " ni mtu wa aina gani anayeweza kumwadhibu kama mwanawe'' (uk. 29).

Mtafiti amebaini kuwa wapelelezi kama Joram wakati mwingine hushikwa na hofu. Joram anashikwa na hofu anapogundua kwamba Chonde ana habari nyingi sana kuhusu juhudi za serikali kushika mhalifu. Joram anaamua kujiamini katika kazi yake. Anajifanya mhalifu ili kupata wahalifu ambao walikuwa hatari zaidi kwa nchi yake.

Mtafiti alibaini kwamba, mpelelezi huyu alishuku kuwa wahalifu hawa walikuwa na masikio hata katika idara ya polisi. Hivyo basi, Joram akaamua kujifanya mhalifu ili atorokee nchi za nje ambapo angefanya uchunguzi zaidi. Nuru anamwambia kwamba, "Sasa nimekuelewa. Nimeelewa kwa nini ulifanya vile. Ulikuwa ukijiandaa kwenda Afrika kusini. Ulichofanya ilikuwa kuilaghai dunia ili uonekane mhalifu". Uoga huo unadhihirika pale anapojaribu kumshawishi Nuru asiende, Joram anasema: "Tatizo ni kurudi. Unaonaje, tutarudi na roho zetu?"(uk.91) Mazungumzo haya yanatufanya tuelewe kwamba ile hali ya Joram kuibia Benki ilikuwa ni mbinu yake ya kuwafanya wahalifu wamuone kama mmoja wao.

Kuna wakati mpelelezi  analazimika kuua ili kuokoa maisha yake na ya watu wengine. Mfano mzuri ni pale Joram na Nuru wanapotoroka kutoka katika chumba walimokuwa wamefungiwa na Makaburu Afrika Kusini. Joram analazimika kumuua mlinzi ili wapate nafasi ya kutoroka. Jambo ambalo baadaye linamhuzunisha sana, lakini jukumu lililomkabili lilikuwa kubwa zaidi. Hivyo basi alilazimika kuchukua hatua hiyo ili kupata nafasi ya kuepuka vifo vya wengi. Tunaambiwa:

> Bila shaka, alijibu mwanamume akiutia mkono wake mfukoni. ulitoka na kisu ambacho kilididimia katika kifua cha mlinzi huyo. Maumivu makali yaliyochanganyika na mshangao vilimfanya aifyatue bunduki yake bila shabaha yoyote (uk.127).

Aidha, Nuru analazimika  kumuua Chonde ili kumuokoa Joram. Anapokuwa ametembelea hotel Afrika kumsaidia Edward kazi ya kuchunguza Chonde, anafika wakati Chonde anajiandaa kumuua Joram. Nuru anafyatua risasi ambayo inamuua Chonde mara moja.  Ingawa Nuru anasikitika hasa pale anaposema, "Unajua jana nimemuua mtu'' (uk.52). Maneno haya yanaashiria kuwa Nuru anasumbuliwa kisaikolojia na tukio hilo kwa kuwa hakuzoea kuua. Mtafiti amebaini kwamba, hii

ndiyo tofauti kati ya waovu wanaotafutwa na wanaoua kujinusuru. Wahalifu walio na utaalamu katika mauaji hawajuti hata mara moja.

Nuru anauua kwa mara ya pili kumuokoa Joram anapokuwa amefungiwa katika chumba cha mauaji Afrika Kusini. Msichana huyu analazimika kumwuua Von Iron kumwezesha achukue fungua za chumba hicho.Von Iron anapokuwa anajiandaa kumuua Nuru baada ya kulipua jiji la Dar es Salaam. Anamwambia Nuru asubiri kidogo ajionee jinsi ambavyo watu wa Dar es Salaam watakavyokuwa wakichomeka. Hakujua kwamba Nuru alikuwa anampumbaza ili apate nafasi ya kujinusuru. Hatua hiyo ya Nuru kumuua Von Iron inamwezesha kuchukua funguo kwenda kumuokoa Joram. Joram anapookolewa na Nuru, anatumia fursa hiyo kuharibu mtambo uliokusudiwa kuwaua wananchi. Aidha, hatua hiyo inawawezesha Joram na Nuru kujinusuru na kuinusuru nchi yao (uk 166-167).

Wasaidizi wa mpelelezi kama vile Nuru huhisi uoga mno wanapokumbana na changamoto za kazi ya upelelezi. Mfano mzuri ni pale Nuru anapomuua Chonde, analia na kujuta kwa hofu ya kushikwa na polisi. Pia, anaposoma taarifa waliopata katika mfuko wa Chonde, anashikwa na hofu, hasira na hamaki hasa anapogundua mipango ya wahalifu hao. Mipango ya kufanya nchi za Kiafrika kutoa machozi ilimshtua si haba. Joram anapomfunulia siri hii, analenga kumtia woga ili asithubutu kwenda Afrika Kusini. Mwandishi anatuambia kwamba wanaposoma maneno hayo, “Nuru anainua macho ghafla kumtazama Joram.Tayari uso wake ulikuwa umelowa jasho ya hofu na mshangao” (uk.90). Joram anapomuambia kuwa hawatarudi na roho zao, Nuru anamjibu, “Sasa sikia, tutakwenda pamoja Afrika Kusini” (uk.91). Mtafiti amebaini kwamba msichana huyu alikuwa mkakamavu na mzalendo aliyekuwa tayari kufanya lolote kuokoa nchi yake ya Tanzania.

Joram anajichafulia jina katika harakati ya kuokoa nchi yake ya Tanzania. Mtobwa anasema kijana huyu alikuwa amegundua kwamba hangemwamini yeyote. Hii ni baada ya kujua adui mwenyewe ni nani, ndipo Joram anafanya uamuzi kutoroka Tanzania. Hakukuwa na njia bora zaidi ya kufanya hivyo. Mtafiti alidhihirisha kwamba Joram anaamua kujifanya mhalifu na mtoro ili kuwafanya wahalifu wafikirie kwamba ni mmoja wao. Anaingia benki na kuiba pesa, jambo ambalo linasikitisha polisi. Kulingana na Inspekta Kombora Joram anapaka jina lake matope. Anasema, "Sijui amepatwa na nini mtoto huyu. Alifoka Inspekta Kombora huku akitupa gazeti hilo mezani"(uk.79). Isitoshe, Mwanahabari mmoja anamharibia sifa sana katika magazeti kwa kusema kwamba Uingereza inawakaribisha na kuishi nao kama binadamu wenzao ilhali ni wahalifu. Anasema, "Miongoni mwa watu hawa kuna Joram Kiango" (uk.74). Mtafiti amebaini kwamba hatua hiyo ilikuwa ni njia moja ya kufanya wahalifu wadhani kwamba, alikuwa ameachana na mambo ya upelelezi.

### 4.3.1 Athari ya uovu kwa wanajamii

Wakati kunapotokea mauaji ya kikatili hasa yanayosababishwa na bomu, wanajamii huathirika sana. Athari hizi huwa za kisaikolojia na kimwili. Wanajamii wanasawiriwa kama watu ambao hujikuta wamefariki bila kuwa na hatia. Mpelelezi na mhalifu wanapopambana, wananchi wengine wasiotarajia huumia. Mfano mzuri ni pale Joram anapouliza kuhusu mabomu waliyokuwa wametega. Nuru anamwambia asikilize kwa mbali mjini kulikuwa na kelele nyingi za hofu. Tunaambiwa:

> Vilio na milipuko ya kutisha unaosikika kutoka kila upande. Wanasikiliza kwa nusu dakika, kisha Joram anatabasamu na kusema polepole: "nilidhani inatosha. Wanakufa wenye hatia na wasio na hatia" (uk. 166).

Aidha, kutoroka kwa Joram na Nuru kutoka mahali walipokuwa wamefungiwa Afrika kusini kunawatia Makaburu wasiwasi. Wananchi Makaburu baada ya kusikia jinsi

ambavyo Joram alikuwa ametoroka, wakawa na uoga kiasi cha kuogopa kwenda kazini. Wengine walikuwa na uoga kiasi cha kutofungua milango yao inapogongwa na yeyote. Joram na  Nuru ambao walikuwa wamebadili sura zao kukaa kama wazungu, wanashuhudia hofu hiyo kila walipopita karibu na Makaburu.Tunaambiwa, ‘‘Macho yao yaliwatazama raia hao Makaburu waliojaa wasiwasi kwa dhihaka’’ (uk.131).

Wananchi wa Tanzania baada ya kupokea habari kuhusu mipango ya wahalifu kulipua miji mikuu, wanatamauka sana. Mwandishi anasema, “Kwa wananchi wa Tanzania na nchi nyingine ambazo zilikuwa mashakani zikisubiri maafa kwa hofu na mashaka makubwa…” (uk 169). Mtafiti amebaini kwamba woga uliwafanya wananchi wenye imani kuweka matumaini yao yote kwa Mungu Mwenye Enzi walipokuwa wanasubiri kifo hicho cha ajabu.  Wananchi wenye imani ya dini wakawa wanasubiri katika makanisa na misikiti. Mwandishi anasema wakristo walichubuka magoti kwa sala ndefu zilizoambatana na vilio. Kwa upande mwingine Waislamu  wakawa wanavunja migongo kwa kwenda rakaa huku wakimlilia Mola.Wasiomjua Mola walisubiri kwa namna mbalimbali. Inabainika kuwa wananchi hawa walikuwa wamejawa na hofu na hali ya kuchanganyikiwa.

Kuna wananchi waliopoteza maisha wakiwa katika harakati ya kusaidia mpelelezi ashike mhalifu. Mfano kijana Edward anayetumwa na Joram katika hoteli kwenda kupekua vitu vya Chonde. Anapoenda pale chumbani analipuliwa kwa bomu. Hapo ndipo Joram anagundua uzito wa kazi iliyokuwa mbele yake. Tunambiwa, “Hakupata kushindwa hata moja isipokuwa leo ambapo amepoteza maisha yake” (uk.45). Haya ndiyo yalikuwa maoni ya Joram alipopata Edward amefariki.

Wananchi wanaofanya kazi katika afisi na majengo makuu ya serikali hupoteza maisha yao wakati wa mikasa hii ya mauaji hasa pale bomu inapotegwa. Kwa mfano, askari mlinzi wa benki kuu anauliwa kwa njia ya kutatanisha. Yeye pekee ndiye mtu aliyemwona mshukiwa wa ulipuaji huo wa benki kuu. Mlinzi huyu alikuwa ndiye tumaini la serikali, kifo chake kina waacha askari bila fununu kwani ni yeye tu aliyekuwa shahidi. Tunaambiwa, "Harakati pekee za kupeleleza ni nani aliyehusika katika kumuua hazikuwa zimezaa matunda yoyote" (uk.16). Mtafiti amebaini kwamba wananchi wasio na hatia huangamia wahalifu wanapokuwa katika harakati ya kutekeleza mipango ya mauaji. Anuawa kwa njia inayowashinda hata polisi kung'amua kwamba ni kazi ya mhalifu. Hapa mtafiti alibaini jinsi Ben R. Mtobwa anavyosawiri polisi wa Afrika Mashariki kama askari wasiochunguza kwa kina kesi za mauaji. Hii ina maana kwamba, wahalifu wengi wanaotekeleza mauaji hukosa kutiwa nguvuni.

### 4.3.4 Athari ya uovu kwa polisi

Askari hukosa usingizi wakati maovu yanapochacha nchini. Haya hutokea pale ambapo wanashindwa kupata mhalifu aliyetenda maovu hayo. Mfano mzuri ni Inspekta Kombora. Ilikuwa dhahiri kwa yeyote amtazamaye Kombora machoni kwamba alikuwa hajapata usingizi wa kutosha kwa muda mrefu. Mambo mengi yalikuwa yamemkabili Kombora kichwani kiasi cha kumpokonya hamu ya kula. Wakati huu wote hawakuwa wamepata lolote la haja katika kukomesha tishio linalokabili nchi. Tunaambiwa, "adui hao walitaka serikali iache msimamo wa kimapinduzi, la sivyo ajali zingeendelea kutokea" (uk. 80).

Askari polisi nao hukumbana na hali ya kuhatarisha maisha yao. Wakati Inspekta Kombora anapofanya uamuzi wa kuchunguzwa kwa Clay ambaye nusura amuue

Inspekta Kombora na askari wengine. Clay anajaribu kumlaghai Kombora kwa kumuambia achukue kifurushi kimoja katika mfuko wake aone kama ungewasaidia kuokoa nchi yao. Kumbe ilikuwa ni akiba ya vigololi alivyotega katika majengo muhimu na kubakisha chache. Clay alikuwa na imani kwamba Kombora angevibeba hadi Makao makuu ya polisi ambapo vingelipuka na kusababisha maafa kwa polisi kadhaa akiwemo Kombora. Alipoona kwamba mpango wake umeshindikana, Clay anachomoa kisu kwa wepesi usiokadirika na kumdunga askari mmoja ambaye tunaambiwa baadaye aliaga dunia. Tunaambiwa, ‘‘Kisu cha pili kilimgwaruza Kombora mkononi’’ (uk.120). Hapo ndipo Kombora anaamua kumuua Clay kwa risasi. Mtafiti amebaini kwamba askari wengi hupoteza maisha yao wanapokuwa wanachunguza uhalifu. Inabainika kwamba Inspekta Kombora anamuua Clay kujinusuru ili asiangamizwe na mhalifu huyo. Hapa ndipo nadharia ya uhalisia inatusaidia kuangazia changamoto zinazokumba polisi.

### 4.3.5 Athari ya kiuana

Mtafiti anagundua kwamba mwandishi Ben Mtobwa anawasawiri wapelelezi wa kike kama watu walioathirika sana kiuana. Sababu kuu ikiwa ni mielekeo ya wahalifu ambao wengi huwaona kama viumbe vya kutumiwa tu Wanawake wapelelezi wanabakwa kuuawa na wahalifu hawa. Von Iron anapomwona Nuru, anaapa kwamba lazima amtumie kimapenzi ndipo amuue. Anapompata anamsihi alale naye ili ajinusuru, lakini Nuru anakataa ombi hilo. Von Iron anaamua kumpiga, kumrarulia nguo na kumbaka Nuru. Von Iron alimchapa akapoteza fahamu na alipoamka, tunaambiwa,“Alikuwa kama alivyozaliwa. Mavazi yake yaliyochakaa yalikuwa yametupwa kando’’ (uk.154).

Aidha, mtafiti amebaini kwamba mwandishi anaonyesha changamoto ambazo wapelelezi wa kike hupitia. Wauaji kama Von Iron hudhulumu na kuwatumia wanawake kama wahasiriwa wa matendo yao maovu. Nuru anapowasili Afrika Kusini Von Iron anawaza tu, jinsi anavyoweza kumtumia kumaliza uchu wake. Baadaye Nuru anabakwa na Von Iron katika afisi yake. Tunaambiwa:

> Von sigara mdomoni alikuwa kaketi pale pale alipokuwa macho yake yakimtazama Nuru kwa namna ya mtu aliyekuwa amekata kiu yake ya muda mrefu (uk. 154).

Hapa mtafiti amebaini kwamba, Von Iron baada ya kumbaka Nuru, Von Iron anajaribu kumbaka tena kwa mara ya pili, na wakati huo ndipo Nuru kwa ukakamavu anatumia udhaifu huo kumuua. Binti huyu anaelewa kwamba maisha yake na ya Joram yalikuwa hatarini. Hivyo basi anatumia nafasi hiyo ya mwisho kujiokoa na kuokoa nchi yake.

### 4.4.0 Mikakati kushika wahalifu inayotumika

Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu* (1987) utafiti wetu umetudhihirishia kwamba Ben Mtobwa anatumia mbinu changamano za upelelezi kinyume na watangulizi wake. Kwa mfano Mohamed Said Abdalla aliyetumia maarifa na uajabu katika riwaya zake. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu* mbinu za upelelezi zinazotumika ni kama vile: ishara, vifaa, maarifa, kubadilisha sura na hulka, sadfa na msaada wa watu wengine. Mbinu hizi zote zinatumika na mpelelezi ili kumaliza uovu nchini Tanzania.

### 4.4.1 Kubadilisha hulka, jina na sura

Mtafiti amebaini kwamba mwandishi alitumia ubadilishaji wa hulka kama njia moja ya kushika wahalifu. Kwa mfano katika riwaya ya *Tutarudi Na Roho Zetu*, Nuru na

Joram ambao ni wapelelezi wanalazimika kubadilisha majina yao ili kupenya katika nchi za kimagharibi. Inakuwa ni lazima waende London na nchi zingine ili kufanya utafiti. Habari walizopata katika mfuko wa Chonde hazingeeleweka hivi hivi. Kwa mfano walipoenda London wakajitambulisha kama Bwana na Bi Godwin wananchi wa Naijeria, mwandishi anasema:

> " sijui dada anaitwa nani?"
> "Mrs Prosy Godwin,"
> " kutoka?"
> " Naijeria."
> " Yuko wapi bwana Godwin ?"
> "Ametoka, ninadhani atarudi baada ya dakika chache" (uk.77).

Anapoenda Nairobi kwa mara ya kwanza anatumia majina ya bandia ili kupata nafasi nzuri ya kujificha. Yeye na Nuru walijiita Bw. na Bi. Charles Morris. Tunaambiwa kwamba walipofika huko waliandika majina katika kitabu cha wageni. Joram anasema, "Mr and Mrs Charles Morris," Joram alijitambulisha (uk.57). Wanapokuwa Nairobi, wanashukiwa kuwa wahalifu, nusura washikwe lakini Joram anatumia ujanja kutoroka. Joram anajifanya mzee mwenye mvi na ndevu ili kujinusuru. Akajiokoa na kutorokea nchi ya mbali. Joram alivalia kama mzee naye Nuru kama kijana wa kiume. Hivyo basi, wawili hawa wanapumbaza watu na kufanikiwa kutoroka. Mwandishi anasema:

> Kijana wa kiume mwenye sura nzuri ambaye alikifunika kichwa chake kwa kofia pana na macho kwa miwani ya jua. Dakika mbili tatu baadaye mzee mmoja wa kiume, mwenye mvi na ndevu za kutosha alionekana akitoka katika hoteli hiyo" ( uk. 67).

Isitoshe msaidizi wake Joram analazimika kubadilisha sura ili kujiokoa. Kutokana na tendo la kubadili sura na jinsia, watu hawa wawili wanawezewa kukwepa askari na kwenda nchi nyingine ili kuendeleza mipango yao ya kutafuta wahalifu. Mwandishi anasawiri wapelelezi kama watu ambao wanafaa kujitolea kwa vyovyote vile.

Kujitolea huku kunajumuisha kubadili sura ili kupenya sehemu wasipohitajika. Joram na Nuru wanabadili sura zao ili kutoroka Afrika Kusini. Walilazimika kufanya hivyo kwa sababu hawangeruhusiwa kutembea au kuingia sehemu zingine wakiwa na sura za Kiafrika. Wakajipatia sura za kizungu. Hii inakuwa moja kati ya shughuli anazofanya, tena kwa gharama kubwa kabla ya kuzuru nchi ya Afrika Kusini. Mwandishi anasema, "Alikuwa amepata mtaalamu ambaye aliwatengenezea ngozi za bandia za kuvaliwa" (uk. 131).

### 4.4.2 Kutumia siri

Mtafiti amebaini kwamba Ben R. Mtobwa alimtumia mpelelezi kama suluhisho katika kumaliza uhalifu. Mpelelezi anasawiriwa kama mtu msiri ambaye wakati mwingine hafai kuamini yeyote hata polisi. Joram Kiango anatupa taswira ya mtu anayejitolea kwa hali na mali. Ana imani kwamba yeye ndiye suluhisho. Tunaambiwa: "Anajiamini na kutotoa siri hiyo hata kwa dunia" (uk. 90). Mara ya kwanza alikuwa amemficha Nuru siri hiyo. Mtafiti amebaini kwamba hakutaka kumuamini yeyote na siri hiyo. Hiyo ni kutokana na utambuzi wa Joram kwamba, hasimu wake kama vile Chonde alielewa mambo ambayo alidhani ni siri kati yake na polisi.

### 4.4.3 Mpelelezi anatumia usaidizi wa watu wengine

Mwandishi anatumia wasaidizi wa mpelelezi kumaliza uovu. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu* anatumia msichana. Mwanamke ambaye labda wahalifu hudharau na kujaribu kutesa, ndiye anayetumikia zaidi katika riwaya hii. Nuru anakuwa msitari wa mbele kumshurutisha Joram aisaidie nchi wakati mabomu yanaanza kutegwa kiholela nchini Tanzania.

Nuru analazimika kumdanganya Joram kwamba ametekwa nyara ili Joram aone hali ya usalama ilivyozoroteka nchini. Mwandishi anasema kuwa Joram alielewa kwamba Nuru alikuwa ameandika barua kumlaghai ili adhani ametekwa nyara. Anamwelezea Nuru kwamba alisalitiwa na mwandiko wake pamoja na kitendo chake cha kuvuruga nyumba. Joram anasema, “Usinichekeshe Nuru. Waweza kuwa ulifanikiwa kuwalaghai watu wote pamoja na polisi, lakini mimi hukunidanganya”(uk.49).

Nuru, msaidizi huyo wa kike alikuwa na ujasiri uliomshangaza Joram. Wanaposoma taarifa iliyopatikana katika mfuko wa Chonde, hapo ndipo wanagundua kwamba Chonde alikuwa amehusika katika ulipuaji wa benki kuu Tanzania. Ugunduzi huo unamfanya Nuru kukata kauli kwamba ni lazima aandamane na Joram kwenda Afrika Kusini. Anaona ugumu wa kazi hiyo na kumhimiza Joram amruhusu kupitia taarifa ya Chonde. Yale wanayoyasoma yanampa ari kutaka kwenda na Joram Afrika kusini. Joram alitarajia kwamba Nuru ataogopa kwandamana naye hasa pale anaposema kwamba, “Huyu alikuwa na jukumu la kusubiri amri yetu ili aachie vipigo vingine ambavyo vitafanya Afrika itokwe na machozi na dunia kulalamika” (uk 90). Lakini kinyume na matarajio hayo, Nuru anavutiwa zaidi na kazi hii.

Mwandishi anamsawiri Nuru kama msaidizi mwenye bidii na roho ya kujitolea. Anamshurutisha Joram waende kusaidia serikali kusaka wahalifu, Nuru anamwambia, “tunawezaje kustarehe hivi huku nchi ikiwa mashakani” (uk.90). Anamshawishi Joram aende naye, kwani atamfaa katika uchunguzi. Anamhimiza waende wapiganie nchi yao. Anadhihirisha uzalendo mkubwa anapokata kauli kuwa anaenda kupigania nchi yake. Joram anamwambia, “Mpenzi wewe ni shujaa kuliko mashujaa wengine niliopata kuwasikia. Sasa sikia, tutakwenda pamoja Afrika Kusini’’ (uk.91).

Joram anapokuwa amefungiwa kule Afrika Kusini asitoke, wanalazimika kutumia mbinu nyingi sana kuokoa nafsi zao. Nuru anachukua nafasi hiyo kuwapumbaza askari ili kumsaidia Joram atoroke. Nuru anatumia uana wake kwa mara ya pili kujiokoa wakati Von Iron anapokuwa akijiandaa kulipua Tanzania na kisha kumua Nuru na Joram. Kama ilivyo kawaida ya wahalifu katika riwaya za Mtobwa, wao huwabaka wasichana kabla ya kuwaua. Hapo ndipo Nuru alidaka nafasi hiyo kumpiga risasi kwa kutumia bunduki ya Von Iron. Kwa kweli baadaye tunamwona akimuokoa Joram kutoka katika chumba cha mauaji Afrika Kusini.

Mtafiti amebaini kwamba baada ya Nuru kubakwa na Von Iron, aliona maisha yake na Joram yakiwa hatarini. Anapogundua kwamba ameduwaa kwa kumwangalia, Nuru anachukua bunduki yake na kulipua kichwa cha Von Iron. Anatumia uke wake kama silaha ya kumuangamiza Von Iron. Nuru na elimu yake juu ya mwanaume alijua kuwa dakika chache baadaye roho ya mwanaume hurudiwa na tamaa ile ile. Hivyo basi anamchokoza ili kumpubaza. Nuru anasema, “wewe ni mshenzi …” alimchokoza tena ili atazamwe.Wakati huo huo akilegeza macho yake na kujiweka kochini …( uk. 156).

Msichana huyu msaidizi wa Joram anaibuka kuwa mkakamavu sana. Anamuokoa Joram kutoka chumba cha mauaji alimokuwa ametupwa na Von Iron. Wakati huo Joram alikuwa ametamauka. Kitendo cha kumuokoa Joram kilikuwa ni hatua kubwa katika vita hivyo vya uhalifu. Baadaye wanaharibu mtambo uliokuwa umetegwa na Von Iron kuangamiza Dar es Salaam. Hivyo basi uovu uliofaa kutendeka unakomeshwa kwa ushirikiano wa Joram na Nuru.

Mtafiti amebaini kwamba mpelelezi alitumia watu fulani mtaani kumsaidia katika kazi hiyo. Mfano mzuri ni pale anapotuma kijana ajulikanaye kama Edward katika

hoteli ya ‘New Afrika’ kutafuta habari kuhusu Chonde. Baadaye kijana huyo anauawa kinyama kwa bomu lililotegwa na Chonde.

Mpelelezi anatumia msichana anayefanya hotelini kupata habari kuhusu makaazi ya Chonde. Joram anamuuliza kwa kutumia maarifa kujua kuhusu Chonde hasa maisha yake kwa jumla. Anampa habari nyingi ikiwemo nambari ya chumba anamoishi Chonde na jina la hoteli. Mhusika huyu wa kike ambaye jina lake halijatambuliwa anamwambia Joram,“Nimekwambia leo hana mtu, ananiambia nikimaliza kazi nimkute hoteli ya ‘New Afrika’ chumba cha 104”. Kwa maoni ya mtafiti, matamshi haya kutoka kwa msichana mhudumu wa hoteli yanampa mpelelezi fununu kuhusu makao ya Proper. Habari hizi zinampa Joram nafasi ya kupiga hatua ya kwanza katika upelelezi wake.

### 4.4.4 Ishara

Ben Mtobwa katika *Tutarudi na Roho Zetu* anamsawiri mpelelezi katika riwaya zake kama mtu anayetumia mbinu changamano za upelelezi kumnasa mhalifu. Mojawapo ya mbinu hizo ni matumizi ya ishara. Matumizi ya mbinu hii inampa mwanga halisi kuhusu fumbo la mauaji yaliyokuwa yakitokea mjini Dar es Salaam na miji mingine katika bara la Afrika.Mara ya kwanza Joram anapogundua kule Chonde anakoishi, anaenda hadi katika hoteli hiyo na kuanza kupekuapekua vitu vyake. Pale ndani anavutiwa na karatasi zilizoonyesha kwamba mtu huyu husafiri sana. Hati za usafiri alizopata ndani ya begi lake zilionyesha kwamba kokote alikoenda alitumia kipindi kifupi mno. Tunaambiwa, “Hapo akawa na maoni kwamba biashara alizofanya mtu huyu hazikuwa za kawaida” (uk.26).

Mbali na hayo, anagundua mifuko ya siri katika begi lake. Mifuko hiyo ilikuwa imejifichwa kiasi kwamba hata maafisa wa forodha hawangeipata. Ugunduzi huo

unahitaji ujuzi maalum, lakini Joram anafanikiwa kuzipata. Katika mifuko hiyo Joram anapata bastola moja. Tunaambiwa, “Aina ya revolver” (uk.27). Aidha, alipata maandishi mbalimbali ambayo alijaribu kusoma bila kufanikiwa kwa sababu yalikuwa yameandikwa kimafumbo.

Isitoshe, anapata kijaluba ambacho kilikuwa kimefungwa kwa ufunguo. Kijaluba hicho kinamvutia sana. Aliona ni kama kijaluba hicho kilikuwa kimeficha mambo mengi. Joram alikuwa na hamu ya kutaka kujua kilichokuwa ndani ya kijisanduku cha Chonde. Ari hiyo inamfanya kutuma mvulana mmoja msaidizi wake kwenda kufanya upekuzi zaidi, lakini mvulana huyo anauwawa. Kijisanduku hiki kinamsaidia kugundua siri nyingi sana ya majasusi hao. Pale anapochukua sanduku la Chonde na kutoroka nayo. Joram anafanya uamuzi kutorokea nchi za nje ili kufanya utafiti zaidi kuhusu habari za siri zilizokuwa mle ndani. Mtafiti alibaini kwamba kijisanduku hicho ndicho kilikuwa ishara kuu katika upelelezi wa mauaji nchini Tanzania. Upekuzi wa Joram unampa nuru kuhusu yale anayostahili kufanya kukabiliana na uhalifu. Anapata ramani inayoonyesha makao makuu ya mipango yote potovu na mahali walipoficha mtambo.

Ishara nyingine inayojitokeza katika riwaya hii ni saa. Joram anapokuwa ameketi na Chonde, saa inatoa mlio wa sauti nyembamba usio wa kawaida. Mlio huo unamfanya Chonde kumwangalia Joram kwa makini na kisha kuondoka kwa kisingizio kwamba anaenda msalani. Joram anasubiri kwa dakika chache na kumfuata nje ambako anagundua kwamba alikuwa amedanganywa. Wakati huo ndipo anajaribu kumpigia Edward simu ili kumuonya dhidi ya kufumaniwa na Chonde. Anapoamua kumfuata kule hotelini, anampata Edward akiwa tayari ameuawa na Chonde. Mtafiti amebaini kwamba ishara inatumika sana na mtafiti katika riwaya hii kuangamiza uhalifu katika jamii.

### 4.4.5 Vifaa .

Mwandishi anasema mpelelezi anatumia ufunguo wenye uwezo wa kufungua kufuli yoyote, kutafuta ushahidi. Joram anatumia funguo hizo kufungua chumba cha Chonde. Mwandishi anatuambia kwamba, uamuzi wake wa kutotembea na bastola unamfanya kuhatarisha maisha yake. Lakini Tunaambiwa:

> Kuacha kwake tabia ya kutembea na bastola hakukuwa kumemfanya aache kutembea na vifaa vyake vidogo vidogo kama funguo malaya ambazo hazishindwi kufungua funguo yoyote ya kawaida (uk. 26).

Joram anatumia bomu kuwafanya Makaburu wawe na wasiwasi. Baada ya Joram na Nuru kuzunguka katika nchi za ng'ambo wakifanya uchunguzi kuhusu vifaa, walivyopata katika kijisanduku cha Chonde, wanaamua kwenda Afrika Kusini kumwangamiza mkubwa wa wahalifu. Kujaribu kuwategea mitego waliokuwa wamepanga kutega Dar es Salaam. Wanapoenda wanakuwa na wasiwasi kiasi kwamba hawakujua kama watarudi na roho zao. Wanapotoroka kutoka mahali wanapohifadhiwa, wanatega mabomu katika majengo muhimu mjini Johannesburg. Von Iron ambaye ndiye mhalifu mkuu, haamini macho yake anapoona jiji hilo likichomeka. Tunaambiwa, "Alikuwa kama ambaye hakuweza kuyaamini macho yake kuona dude hilo likizidi kusongea. Mara jiji la Johannesburg likijitokeza katika kioo hicho" (uk.157). Mtafiti alibaini kwamba walipofanya hivyo waliwafanya Makaburu wale kuwa katika hali ya kutoelewa kilichokuwa kinatokea. Hivyo basi, Nuru na Joram wanapata nafasi nzuri ya kuharibu mtambo wao.

Hii ina maana kwamba Joram alitumia bomu kujaribu kukomesha uhalifu. Vigololi alivyopata kutoka kwa marehemu Chonde, viliwafaidi pakubwa kupigana vita hivi. Nuru alipoona majumba yanalipuka, anakumbuka kwamba walitega mabomu. Nuru

anasawiriwa akiwaza kuwa, “Ni yale ambayo yeye na Joram wamefaidi kisha kutega vile vigololi ambavyo walipata kutoka kwa hayati Chonde” (uk 158).

Msaidizi wa mpelelezi katika riwaya hii anatumia bunduki kumwangamiza mhalifu. Tunaambiwa Nuru alichukua bunduki ya Joram. Wakati Joram akiwa katika chumba cha Chonde, Nuru anatokea na kuokoa maisha yake. Anafanya hivyo kwa kumuua Chonde kwa bunduki. Nuru anatumia bunduki kwa mara ya pili kuokoa maisha ya Joram. Anamwangamiza mhalifu Von Iron kwa kutumia bunduki yake mwenyewe. Tunaambiwa, “Bastola ilikuwa mikononi mwa Nuru macho yake yasiyo na mzaha yakitangaza shari”(uk.159).

Kwa maoni ya mtafiti, sentensi hii inaonyesha jinsi uzalendo unavyoweza kumfanya mtu kuwa na ukakamavu. Isitoshe, ujasiri unaosawiriwa na Nuru ni dhihirisho tosha kwamba kupigana na uhalifu haujali uana.

### 4.4.6 Maarifa

Joram anapotoka nje ya Tanzania ndipo anaanza kutumia maarifa kusoma na kuchunguza habari zilizokuwa katika kijisanduku cha Chonde. Anatumia makini na ujuzi mwingi kujaribu kuelewa habari alizopata katika kijisanduku hicho. Mwandishi anasema, “Yale maandishi ya kijasusi ni jambo jingine ambalo lilihitaji muda na utulivu mkubwa ili kueleweka” (uk.51).

Joram aliamini kuwa yale aliyoyapata katika kile kijisanduku yalimtosha kujua ukweli na kupambana na uhalifu. Anakusanya nyaraka zote muhimu na kuziweka katika begi lake. Mpelelezi huyu alijuwa vizuri kwamba kukaa kwake Tanzania hakungemruhusu kufanya uchunguzi wa kutosha. Hakuwa na imani na mtu yeyote pale. Hakuwa na

uhakika kama Chonde mwingine angejitokeza na labda aibe habari za pekee ambazo zingemsaidia kugundua ukweli wa mambo.

Aidha, Joram anatumia maarifa kuelewa ramani aliyoipata kwenye kijisanduku cha Chonde. Tunaambiwa, "Ramani hiyo ilimwonyesha majengo maarufu kama ikulu, vituo vya jeshi, mabenki, na kadhalika." Mpelelezi anatumia umakini wake kuelewa nambari za kirumi zilizokuwa kwenye majengo hayo zilikuwa na maana fulani. Anagundua kwamba jengo la benki kuu lilikuwa na alama ya X kwa wino nyekundu. Akakumbuka kuwa jengo hilo tayari lilikuwa limechomwa. Akang'amua kuwa Chonde alikuwa amehusika kuteketeza benki kuu. Joram anatia juhudi kuelewa maandiko ya vitu alivyopata katika kijisanduku hicho. Anachukua muda kujifunza mbinu za kuyasoma maandishi katika nyaraka alizopata. mwandishi anasema:

> Kisha alifunga sanduku hilo kikamilifu na kuandika meza ambayo aliinamia na kuanza kujifunza tena mbinu za kuyasoma maandishi hayo kwa makini zaidi"(uk.62).

Joram anatumia maarifa kama mbinu ya kumnasa mhalifu. Kwanza kabisa alikuwa ametamauka baada ya kifo cha Neema. Anapokosa nafasi ya kumuua mhalifu aliyetenda kitendo hicho. Joram anaamua kuburudika tu na kuachana kabisa na mambo ya upelelezi. Anapojaribu kushawishiwa na Nuru kurudi kazini, anakataa katakata. Maafa yanayotokea ya mauaji katika benki hayamshtui hata kidogo. Anapokutana na Chonde anamshuku kuwa jasusi hasa pale wanapojadiliana naye. Joram anatumia maarifa yake kufanya uamuzi wa kumchunguza Chonde. Anamfuata hadi chumbani kwake, ambapo upekuzi wake unadhihirisha ukweli huo. Anapata kijisanduku katika vitu vya chonde ambacho anashuku kina mambo mengi ya siri. Anatumia maarifa yake kugundua mifuko ya siri katika kijisanduku hicho. Hapo ndipo anang'amua kwamba maisha yake yako hatarini. Joram anatumia msaidizi wake kwenda kupekua zaidi. Upekuzi huo unasababisha kifo cha Edward.

Isitoshe, anatumia maarifa kuchukua kijisanduku cha Chonde kwa upekuzi zaidi. Aidha, anatumia maarifa kufungua kijisanduku hicho kupata habari zaidi. Tunaambiwa, “Joram aliliendea sanduku la marehemu Chonde na kutazama uwezekano wa kukifungua” (uk.51).

Anatumia maarifa anapokabiliwa na mtu asiyemjua. Mwanamme huyu anaanza kumhoji na kumkejeli kwa kupoteza uzalendo wake. Wanapoendelea kunywa na kuongea anatumia maarifa kugundua kuwa Chonde hakuwa mtu wa kawaida. Hivyo basi anaamua kumchunguza zaidi Chonde. kwa mfano anashangaa Chonde anapomwambia, “Mwanamapinduzi aliyekata tamaa,” Chonde alikuwa akisema . “Aibu iliyoje kukata tamaa hali nchi yako iko mashakani” (uk 42)? Aidha, ilibainika kwamba matamshi hayo yanamfanya Joram kuwa makini zaidi. Joram anatia shaka zaidi pale anapogundua kwamba Chonde anajua mambo mengi kuhusu maisha yake. Hasa pale anaposema:

> Ninasikia msichana wako ametekwa nyara .
> umesikia wapi?
> kwani ulidhani siri? (uk 42)

Kwa maoni ya mtafiti, matamshi hayo ya Chonde yanamfanya Joram kuwa na wasiwasi. Anasema jambo hilo linamshtua Joram, hivyo basi anatumia maarifa yake kumshuku Chonde zaidi. Anakuwa na imani kwamba mtu huyu alikuwa amezidokoa habari hizo kwa polisi. Jambo hilo linamfanya azidi kufikiria kwamba hakuwa mtu mwenye mkono mrefu tu, bali alikuwa na masikio mapana. Kukosa imani kwa polisi ndiko kunamfanya Joram kuchukua hatua ya kuufanya upelelezi bila kuhusisha polisi wala serikali kwa njia yoyote. Ndiyo maana baadaye anafanya uchunguzi mwenyewe hadi anapofaulu kuangamiza uhalifu.

### 4.4.7 Sadfa

Mwandishi Ben R. Mtobwa anatumia sadfa kama mbinu ya upelelezi. Joram anapofumaniwa na Chonde, anachapwa kama mbwa na kuambiwa kwamba atauawa na maiti yake kuokotwa siku inayofuata. Mwandishi anatumia sadfa kuonyesha jinsi ambavyo maisha ya Joram yalivyookolewa. Anajiona akiwa na vita vikubwa zaidi vya kuokoa roho yake. Kabla hajafiatuliwa, mlango unabishwa na kufunguliwa kwa utaratibu. Wakati huo tunaambiwa, "Wote walimtazama msichana, Chonde akimlaani Joram akimshukuru" (uk.30). Joram anadaka nafasi hiyo kutoroka.

Sadfa inatumika na mwandishi Mtobwa pale Chonde anapokuwa amemwelekezea Joram bunduki na kusema, "Ningependa kukuua kwa mkono mitupu. Hata hivyo sina muda wa kutosha" (uk.46). Mara Chonde akielekeza bastola katika kifua cha Joram, kidole chake kikigusa kiwambo cha kufyatulia risasi, lakini akasita kufyatua. Mara hiyo, Nuru anaingia na kumuua Chonde. Joram anagundua kwamba yuko hai. Anaamua kuchunguza ili ajionee kilichokuwa kimejiri. Anapochungulia, anamuona Chonde kalala chini kifudifudi, damu ikimvuja katika tundu la risasi. Aidha, anagundua kuwa Nuru alikuwa ametokea na kuokoa maisha yake.

Aidha, sadfa inatokea wakati Joram anapokuwa aking'ang'ana kujiokoa au kutafuta mwanya wa kutoka katika lile pango la kifo. Katika mawazo yake, Joram anaamua kwamba yeyote ambaye angeingia angemuua au kumlazimisha kumtoa mle ndani. Wakati akiwaza hilo ndipo naye Nuru anatokea kama malaika kuja kumuokoa. Joram anasema, "Wewe Nuru kweli au malaika (uk.166)?" Mtafiti alibaini kwamba, Mtobwa anatumia mbinu hii kuokoa maisha ya mpelelezi ili kumwezesha kutimiza lengo lake.

Kwa mujibu wa mihimili ya nadharia ya maadili, mtafiti ameweza kuchunguza aina za uovu . Isitoshe, tumebaini jinsi ambavyo mazingira yanavyoweza kuchonga tabia ya mwanadamu. Aidha, tumeona kuwa mwanasanaa kama vileBen R. Mtobwa anavyotimiza jukumu la kuangazia kiini cha uovu na kuelekeza jamii katika wema.

Kinadharia kupitia mihimili ya nadharia ya uhalisia, mtafiti amebaini kwamba mwandishi anazungumzia mandhari ya kawaida. Mandhari anayotaja ni yale yanayoeleweka kwa mfano anazungumzia mazingira ya mijini kama vile Dar es Salaam na Johanesburg. Aidha, athari ya mauaji pamoja na mikakati ya kushika mhalifu ni mambo ya kawaida yanayoweza kudhihirika katika maisha ya kawaida.

**Hitimisho**

Katika sura hii mtafiti ameshughulikia muhtasari wa riwaya ya *Tutarudi* na *Roho* zetu. Aidha sura hii imeshughulikia kiini hasa cha uovu katika riwaya hii, utekelezaji wa mauaji, athari ya mauaji hayo na mbinu zilizotumika kuwanasa wahalifu. Aidha mtafiti amezungumzia athari ya uovu kwa mpelelezi mwenyewe, kwa jamii na hata kwa polisi. Isitoshe, mtafiti alibaini kwamba siasa pia huchangia kueneza maovu nchini. Watu waovu wenye tamaa ya uongozi hupanga njama kuwaua wapinzani wao hapa barani Afrika. Binadamu wenye akili mbovu na wenye uchu wa kumwaga damu kama akina Von Iron na Chonde hutumika kutekeleza mauaji hayo. Mtafiti amekuwa mwenye maoni kwamba wapelelezi huhatarisha maisha yao, hivyo basi wanafaa kuwa na ujuzi mwingi kupigana na uhalifu. Hata hivyo mtafiti amebaini kwamba mbinu za upelelezi zilizotumika ni za kihalisia.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuonyesha jinsi uovu unavyosawiriwa katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa yaani: *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984) na *Tutarudi na Roho Zetu* (1987). Utafiti huu ulilenga kubainisha mtazamo wa Ben R. Mtobwa kuhusu uovu. Hata hivyo, utafiti ulifanywa kutokana na utambuzi kuwa kulikuwa na haja ya kuelewa dhana ya uovu athari zake na jinsi Ben R. Mtobwa anavyotumia riwaya zake kuweka wazi maovu hayo. Aidha, ukosefu wa utafiti wa kina kuhusu usawiri wa uovu katika riwaya za Ben R. Mtobwa na mbinu zinazotumika kuwanasa wahalifu hao ulichangia katika kufanywa kwa utafiti huu. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Maadili na Nadharia ya Uhalisia. Mihimili mitatu kutoka kila nadharia ilitumika ili kutambua uovu na kuushughulikia kimaadili.

Katika sura ya kwanza, masuala ya kimsingi katika utafiti ambayo ni usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti zilizohusisha eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data yalishughulikiwa.

Sura ya pili imeshughulikia historia na tajriba ya mwandishi Ben R. Mtobwa, maana ya uovu, dhana ya uovu kulingana na wataalamu mbalimbali, aina za uovu na mawazo ya Mtobwa kuhusu kiini cha uovu katika riwaya zake. Maelezo hayo yalinuiwa kuweka wazi tajriba ya msanii pamoja na kurahisisha hali ya kueleza na kufahamu kazi zake. Ilikuwa bora kwa utafiti huu kuelezea maana mbalimbali ya uovu pamoja na dhana ya uovu ili kulinganisha maoni ya wataalamu mbalimbali. Isitoshe suala la maadili lilijadiliwa kwani ili kuelewa uovu, ni lazima kuwe na

ufahamu wa wema. Wema na uovu ni kama pande mbili za shilingi. Aidha, uainishaji huu ulifanywa kwa kuzingatia riwaya teule za mwandishi.

Sura ya tatu imeshughulikia kiini cha uovu, athari ya uovu na mbinu za upelelezi zilizizotumika katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984). Sura hii ilitoa maelezo ya jumla kuhusu riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984). Matukio muhimu kutoka mwanzo hadi mwisho yalishughulikiwa. Sura hii pia ilishughulikia viini mbalimbali vilivyosababisha uhalifu wa aina hiyo kutokea katika jamii. Utafiti ulidhihirisha kuwa mauaji ya kikatili huwa na athari kubwa siyo tu kwa wanajamii, bali kwa wapelelezi na hata polisi wanaoshughulikia kesi hiyo. Kwa kumsawiri mhalifu akishindwa kufaulu katika malengo yake, mwandishi anaonyesha mikakati inayoweza kuifaa jamii yoyote ile kupigana na uhalifu. Matukio mengi yaliyozungumziwa na mwandishi hutokea katika mazingira yetu. Kwa mfano, kuna tukio la mauaji la wachimba migodi Kaskazini Mashariki mwa Kenya tarehe 2/11/2014. Hii ina maana kuwa uovu ni changamoto inayoikumba jamii ya sasa. Kwa kuangazia mambo haya, mwandishi anawazindua wajamii na kuwataka wajikakamue katika kutafuta njia za kuyaepuka matatizo hayo katika maisha yao ya usoni. Suala la mwanadamu kugeuka na kuwa muuaji linatupa nafasi ya kutafakari na kuepukana na mambo yanayofanya maovu hayo kushamiri katika jamii. Inabainika kuwa wale wasiojitahidi kupinga uovu, huchangia katika kuleta hali ya taharuki katika jamii zetu.

Sura ya nne katika riwaya hii imeshughulikia kiini cha uovu, athari ya uovu na mbinu za upelelezi katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu* (1987). Aidha sura hii imeshughulikia jinsi mazingira kama kiini kikuu yalivyowaathiri wahusika mbalimbali katika riwaya teule. Matendo ya wahusika hawa wauaji, yanawaathiri wanajamii wengine, polisi na mpelelezi. Katika harakati za kuiokoa nchi yake,

mpelelezi anaponyoka kifo mara tatu mfululizo. Aidha, utafiti huu umejadili mbinu anazotumia mpelelezi katika kupigana na uovu hadi anapomuua mhalifu. Imedhihirika kuwa mbinu anazotumia Mtobwa ni za kisasa na zinatofautiana na waandishi wa awali kama vile Mohamed Said Abdalla waliotumia tu maarifa na uajabu.

Sura ya tano na ya mwisho imeshughulikia muhtasari, matokeo, mapendekezo na hitimisho la utafiti.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umebainishia kuwa riwaya za upelelezi zina umuhimu siyo tu katika fasihi bali katika jamii. Imethibitishwa kwamba mbali na kuburudisha, riwaya hizi zimetumika kama gurudumu la kufichua na kuweka wazi maovu yanayopatikana katika jamii. Ben R. Mtobwa amezungumzia aina nyingi za maovu yakiwemo ulevi, unafiki, ubakaji mauaji ya kikatili na ubaguzi wa rangi. Mauaji ya kikatili ni aina ya uovu ambao umeshughulikiwa zaidi na Ben R. Mtobwa katika riwaya zake. Utafiti huu ulibaini kwamba, maovu yapo na ni suala linalotishia amani na linajitokeza zaidi katika jamii ya sasa. Pia, uchunguzi huu ulipata kuwa uhalifu upo ila unaweza kukomeshwa kwa ushirikiano wa polisi, wapelelezi na hata jamii. Hivyo basi Ben R. Mtobwa anatumia fasihi kuweka wazi maovu katika jamii na kubainishia njia mwafaka za kupigana nayo. Taswira anayotupa Ben R. Mtobwa katika riwaya zake teule ni kwamba uovu unaweza kushindwa ukikabiliwa vilivyo na washikadau wote.

Aidha imebainika kwamba mwanadamu anaweza kuwa mwema au muovu. Walimwengu mara nyingi hutarajia wenzao watende wema au uovu. Haya yameonekana wazi hasa pale ambapo watu wema kama Joram wamelimbikiziwa sifa ilhali waovu kama akina Proper na Von Iron wanakashifiwa. Maudhui haya husaidia

kutimiza lengo hasa la fasihi ambalo kulingana na Gardener (2005), ni kusisitiza maadili yanayotufaa na kutufanya kuhisi vibaya kuhusu upungufu wetu na matendo yetu mabaya.

Isitoshe, Ben R. Mtobwa katika riwaya zake teule za upelelezi anaonyesha kuwa wahalifu hasa wauaji huenda wakawa walichochewa na mazingira yao ya utotoni. Ingawa kuna viini vingine vinavyotajwa kama siasa na tamaa. Uchunguzi huu uliangazia swala la siasa ambalo ni changamoto kubwa hapa barani Afrika. Kwa kuwa Mtobwa alikuwa akifanya kazi ya kuandika magazeti, alikuwa na habari kuhusu tamaa ya uongozi na sababu zingine zilizosababisha uovu. Pia aliwataja watu wenye tamaa ya mali na ubaguzi wa rangi.

Malezi anayopewa mtoto katika familia huijenga tabia yake ya baadaye. Hivyo basi mtoto akishuhudia maisha ya uovu au kulelewa katika mazingira ya uovu, huenda akaathirika katika maisha yake ya utu uzima. Tunaona kwamba mhalifu mkuu Proper katika Riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu( 1984)* aliteseka kiasi cha kutoroka nyumbani. Anapotoroka akiwa na miaka kumi na miwili, Proper anajikuta miongoni mwa mabaharia wenye nyoyo za kinyama. Mateso anayopata pamoja na ukatili anaoshuhudia kutoka kwa mabaharia wale inamfanya kuwa mhalifu sugu asiyekuwa na utu hata kidogo. Anakuwa muuaji anayewachinja watu na anayeua kwa njia za kikatili. Von Iron ni mhusika anayepanga mauaji mengi sana ya Waafrika katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu.* (1987) Anasawiriwa kama mtu aliyechochewa na mazingira. Wahusika makahaba katika riwaya hizi wanasawiriwa kama watoto waliolelewa katika madanguro, kubakwa wakiwa watoto na kurithishwa uovu huo. Uchungu walio nao unawafanya kuwa wauaji. Kwa sababu ya uchungu huo,

wahusika hawa wanakosa upendo wa dhati na wanakuwa na tabia za kinafiki. Mfano mzuri ni Waridi katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984).

Utafiti huu pia umedhihirishia kwamba mtazamo au falsafa ya Ben R. Mtobwa yanaafikiana na mawazo ya Jacques Rousseau katika kazi yake '*Confessions of Rousseau*. Rousseau anasema ukatili aliotendewa na mwajiri wake ulimfanya awe na tabia mbaya kama udanganyifu, wizi na kadhalika. Utafiti huu umedhihirishia kwamba watu waovu zaidi duniani kama vile Shaka Zulu wa Afrika Kusini, General Idi Amin wa Uganda, Adolf Hitler wa Ujerumani ni miongoni mwa watu waliolelewa katika mazingira magumu au potovu. Hitler alikuwa akichukiwa na babake ambaye alimchapa hadi akazoea uchungu. Siku moja, babake alimchapa viboko thelethini na viwili lakini hakulia. Mbali na hayo, alisononeshwa sana na dhuluma ambazo babake alimtendea mamake. Kulingana na historia, katika utu uzima wake Hitler anajulikana kama binadamu aliyewaua watu wengi zaidi. Machungu aliyohisi akiwa mtoto yalimfanya kuwa muuaji katili zaidi katika utu uzima. Haya yanadhihirishia kwamba fasihi ni kioo cha jamii na huweza kutumika kuuangazia masuala nyeti katika jamii. Isitoshe, fasihi haitoki katika ombwe tupu bali huangazia mawazo yanayoweza kutetewa na matendo ya wanajamii.

Uchunguzi huu umetambua kuwa mauaji ya kikatili ni aina ya uovu ambao huonyesha kiwango cha uovu unaomshtua binadamu yeyote. Imebainika kuwa uovu wa aina hii umekuwa jambo la kawaida katika karne ya ishirini na moja. Nchini Kenya kwa mfano, kumekuwa na mauaji mengi yaliyotekelezwa na watu binafsi. Mfano mzuri ni Onyancha kule mjini Naivasha (12/ June /2013), Mukhobero wa Kakamega (alimkatakata mke na watoto wake wote) na Naivasha Vampire aliyewaua mabinti wengi tu bila sababu maalum. Aidha, kuna waovu fulani wenye kufurahia kumwaga

damu ya watu ili kutekeleza maovu hayo. Kwa mfano wahalifu kama vile Osama bin Laden aliyeanzisha kundi la wahalifu la kuwaua watu. Isitoshe, kuna Alshabaab, ambao wametekeleza mauaji mengi sana nchini Kenya. Mifano ya matukio haya ni kama mkasa wa Westgate (21/9/2013), mauaji ya Mpeketoni (2014), mauaji ya walimu katika basi Marsabit (22/11/2014) na uvamizi wa Chuo kikuu cha Garissa. Binadamu kuwauua wenzao bila kuhisi uchungu wowote kunadhihirisha kwamba, mauaji ya kikatili ni uovu unaoikumba jamii kihalisia. Haya yamedhihirika kwa kuwa ni masuala nyeti na ibuka katika karne hii ya ishirini na moja. Mtafiti amebaini kwamba Ben R. Mtobwa alitumia riwaya zake za upelelezi kutupa mwanga kuhusu maovu yanayoikumba jamii.

Utafiti huu pia umeangazia athari za mauaji ya kikatili. Mpelelezi, wanajamii na polisi wanaathirika sana na uovu huu. Mpelelezi ambaye katika riwaya za Ben R. Mtobwa anajulikana kama Joram aliathirika kwa njia mbalimbali. Kwanza mhalifu anapanga kumuua ndiposa aweze kuendelea na mipango yake ya mauaji. Mhusika Proper katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* anajaribu kumuua Joram. Kwanza anamtuma Waridi na sumu kali ili amwangamize Joram. Mara ya pili anatega bomu katika nyumba alimokuwa anaishi kwa imani kwamba atamwangamiza. Hivyo basi kunakuwa na majaribio mawili ya kumuua Joram. Mpelelezi msaidizi wa Joram, msichana kwa jina la Neema ananajisiwa na kuuawa kinyama na mhalifu Proper anapomshuku kuwa amegundua siri yake. Athari hizi ni za kihalisia hata katika nchi za Afrika Mashariki. Kwa mfano mpelelezi mwanahabari kama vile Muhammed Ali nchini Kenya huhatarisha maisha yake kila mara anapokuwa katika harakati za kufanya udadisi kuhusu maswala tata ili kuyapeperusha katika kipindi kijulikanacho kama ‘Jicho pevu’ kwenye runinga ya ‘KTN’. Wananchi huwaamini wapelelezi na hivyo basi kuwapa habari muhimu zinazoweza kuwasaidia polisi kuwanasa wahalifu.

Mara nyingi maisha ya wapelelezi hawa huwa hatarini hasa wahalifu wanaposhuku kuwa watatoboa siri zao.

Bomu linapotegwa, mhalifu anawaangamiza waliomo na wasiokuwemo. Kuna wananchi wasiokuwa na hatia kama vile Bagambe, Sofia na Waridi katika *Salamu kutoka Kuzimu* (1984) ambao wanapoteza maisha yao. Tukio hili linaonyesha namna Ben R. Mtobwa anavyoyaangazia mambo ya kihalisia yanayokumba nchi nyingi za Kiafrika katika karne hii. Kwa mfano wanafunzi walipovamiwa katika Chuo Kikuu cha Garrisa, wazazi waliathirika sana kisaikolojia huku wanafunzi wengine wakiachwa wakiwa viwete. Isitoshe, kuna wale waliokufa kutokana na kisa hicho.

Polisi wengine huathirika kwa kufutwa kazi na wengine kuuawa wanapokuwa wanapigana na uhalifu. Askari mmoja ajulikanaye kama Bob anafariki kwa njia ya kikatili anapokuwa katika harakati ya kuchunguza kesi ya mauaji. Inspekta Kombora mwenyewe anakuwa na wasiwasi kwani vifo visivyoeleweka vinatokea kila kukicha. Katika *Tutarudi na Roho Zetu (1987)*, Kombora anadungwa kwa kisu mkononi huku askari mmoja akiuawa na mhalifu Clay. Hivyo basi, maisha ya polisi hawa huwa hatarini kila mara hasa wanapofanya uchunguzi kuhusu mauaji. Athari za uovu zinazojitokeza katika riwaya za Ben R. Mtobwa ni mambo ya kihalisia.

Kazi hii imetambua kwamba mbinu za upelelezi zinazotumika katika riwaya hizi zinaweza kufaa katika jamii yoyote ya kisasa. Aidha, imedhihirisha kuwa uovu unaweza kumalizwa ikiwa washikadau watashirikiana na kutumia mbinu changamano za upelelezi. Mpelelezi anatakiwa kuwa mwerevu, mwenye hekima na ujuzi wa kupigana na mtu anayefanya maamuzi ya haraka. Pia anafaa kuwa mwigizaji anayeweza kuiga mienendo na hulka za watu mbalimbali ili kumwezesha kupenya sehemu ambazo ni hatari kuingia. Imetambuliwa kwamba, haya yote yakifanywa kwa

uangalifu, mipango ya wahalifu inaweza kuzuiwa na kumalizwa kabla hawajatenda uovu.

Imebaini kwamba mbali na polisi kupigana na uhalifu, kunafaa kuwe na mpelelezi wa kibinafsi. Kuwe na watu wanaoweza kufanya ujasusi kwa vyovyote vile bila kutambulika. Mpelelezi afanye lolote hata kama ni kujifanya mhalifu ili aweze kuteka imani ya wahalifu. Ni kwa kujifanya mhalifu ndiko kunamfanya mpelelezi katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu* (1987) anagundua mpango halisi wa wahalifu hao na kuharibu mipango yao kwa wepesi. Mtu huyo anafaa kuwa mzalendo ambaye yuko tayari kuifia nchi yake na kushirikiana na polisi na wanajamii kama anavyofanya Joram katika riwaya zake teule. Hivyo basi, upelelezi umedhihirika kama mkakati maalum wa kukabililiana na uovu.

Kutokana na utafiti uliofanywa, imedhihirika kwamba Ben R. Mtobwa alikuwa mtu mwenye maadili mema kinyume na hadithi alizoziandika. Watu wengi hasa wale waliosoma '*Dar es Salaam Usiku'* walimuelewa vibaya. Hii ni kutokana na jinsi Ben R. Mtobwa anayoyaweka wazi mambo ya mapenzi. Kwa kuelezea kinagaubaga hatua za kufanya mapenzi katika *Tutarudi na Roho Zetu* (1987). Mtafiti amebaini kwamba marehemu Ben Mtobwa alitaka kutoa taswira ambayo ingemfanya mtu yeyote aelewe ni kwa nini Von Iron hangestahamili kuangalia kamera iliyokuwa chumbani mwa Joram na Nuru. Mtafiti aling'amua kwamba, mwandishi alitaka kutuonyesha umbali ambao wapelelezi huenda ili kufanikisha uchunguzi wao.

Mbali na hayo, utafiti huu umebaini kwamba riwaya za upelelezi husomwa sana na vijana nchini Tanzania. Riwaya hizi basi zinaweza kutumika kutoa mafunzo kwa vijana iwapi watazingatia wanayosoma. Hili litawawezesha kuelewa uovu na wema. Kwa kuelewa uovu na wema, vijana hawa wataweza kufanya uamuzi wa busara kwa

vile wanaelewa tofauti iliyopo katika ya dhana hizi mbili. Aidha, vijana hawa wataelewa kiini cha uovu na athari zake. Wale walioathiriwa utotoni wanaweza kupewa ushauri nasaha wa kutosha ili uchungu au mazingira mabaya ya utotoni yasiwaathiri katika maisha yao ya usoni. Kuna makala bunilizi ya fasihi, hasa katika riwaya za upelelezi ambayo huweza kufunzwa. Kwa maoni ya Price- Anisman (1982), kuna vitabu vya upelelezi vyenye manufaa kwa mwanafunzi. Yeye ni moja miongoni mwa watetezi wa riwaya hizi ambazo anaamini huweza kufaidi wanafunzi kupata ustadi. Anasema wanafunzi hao huishi katika mazingira yenye fujo na ukosefu wa matumaini, hivyo basi huwa na uelewa kuhusu wema na uovu, uhalifu na wahalifu, haki na uovu. Anaamini kuwa athari ya hadithi hii inatosha kumsaidia mwanafunzi kuwa na uhuru wa kujiamulia mambo. Washiriki hawa basi mwishowe huonyesha uadilifu na ukosefu wa maadili. Suala la mauaji huondoa ubunifu na kudhihiri uhalisia ambao wanafunzi wanaelewa. Hii inaonyesha kwamba riwaya za upelelezi zina dhima katika jamii kwani zinapendwa na vijana na hivyo wakizoea kuzisoma huenda wakajifunza kupigana na uhalifu.

Zaidi ya yote, utafiti huu umebainisha kwamba mikakati changamano inatumika katika riwaya hizi kumaliza uhalifu. Mbali na mpelelezi kuwa na maarifa, pia anatumia mbinu za kisasa kama vile ishara, vifaa, kubadili sura na hulka, kushirikiana na watu wengine na sadfa kumaliza uovu katika jamii. Katika kufanya hivyo, utafiti huu umeonyesha jinsi Ben R. Mtobwa anavyotofautiana na watangulizi wake kama vile Muhamed Said Abdalla na wengine katika kutatua suala la uovu. Mbinu hizi hutumika katika enzi ya kisasa na hivyo kudhihirishia kwamba riwaya za upelelezi zinaweza kutumika siyo tu kutahadharisha jamii kuhusu uovu bali pia inaweza kutumika katika kutuelimisha kuhusu njia za kisasa zinazoweza kutumika kupigana na uovu.

## 5.3 Changamoto za Utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto si haba. Mojawapo wa matatizo hayo ilikuwa ni tafsiri. Ili kuweza kupata maana ya dhana mbalimbali zilizotumiwa, mtafiti alilazimika kusoma vitabu vya kiingereza na baadaye kuvitafsiri. Isitoshe taarifa zilizotolewa mtandaoni pia zilikuwa zimeandikwa kwa Kiingereza na hivyo zilihitaji kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Maelezo mengi yalikuwa kuhusu nadharia na yalikuwa yameandikwa katika lugha ya Kiingereza. Halikuwa jambo rahisi kutafsiri dhana zilizotumiwa na kuweka wazi ujumbe kwa kuzingatia maana halisi iliyotarajiwa.

Mtafiti hakuweza kusafiri hadi Dar es Salaam kuihoji jamii ya Ben R. Mtobwa. Uhaba wa fedha haungeturuhusu kuwafikia watu hawa huko Tanzania. Badala yake, mawasiliano kwa njia ya simu na pia barua pepe kwa wahadhiri wa chuo kikuu cha Dar es Salaam yalifanywa. Muda mwingi ulipotezwa kuwatafuta watu ambao wangehiari kuzungumza na baadhi ya jamaa za Mtobwa. Bwana Ogalo aliyemfikia mhariri wa kampuni ya *Heko* pamoja na kumjulisha mtafiti kwa Reystuta Mtobwa ambaye ni bintiye Ben Mtobwa. Binti huyo aliufaa utafiti huu pakubwa kwa kutoa habari kumhusu babake.

Licha ya changamoto, utafiti ulifaulu kwa kiasi kikubwa na unalenga kuchangia katika kufanikisha usomaji na ufundishaji wa somo la fasihi kwa mazingatio ya riwaya za upelelezi kama zenye dhima kuu ya kuikosoa jamii.

## 5.4 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umedhamiria kuwaandaa binadamu kuelewa maana ya uovu, kiini na athari ya uovu katika jamii. Uelewa huo utasaidia wanajamii kujihadhari na hata kuudhibiti uovu kabla ya hatari. Aidha, umeonyesha kuwa uovu unajitokeza zaidi

katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa. Mtazamo wa mwandishi umetuonyesha wazi kuwa uovu lazima upingwe kwa njia yoyote ile ili kuelekeza jamii katika wema. Kwa kutumia Nadharia ya Uhalisia, utafiti umedhihirisha aina za uovu na jinsi maovu haya yanavyopotosha maadili katika jamii.

Imebainika kwamba uovu upo na ni changamoto inayoikabili jamii ya sasa, lakini wanajamii wanaweza kubadili mikakati ya kupigana na uovu huo. Binadamu wanafaa kutumia mbinu za kisasa zinazotofautiana na zile za waandishi wa jadi ambao walitumia tu mbinu moja, yaani maarifa kutatua shida za uhalifu. Ben R. Mtobwa anashughulikia msururo wa mauaji, mauaji ya kinyama na mauaji ya halaiki ya watu ambapo mtu anatumia bomu. Haya ni kinyume na mauaji ya mtu mmoja yaliyodhihirishwa na watangulizi wake.

Kwa hivyo, utafiti umeweza kubainisha jinsi uovu unavyosawiriwa katika riwaya za upelelezi (kama riwaya teule za Ben Mtobwa) miongoni mwa riwaya zingine. Aidha utafiti huu umefungua ukurasa mpya wa kuchunguza, kutathmini na kujadili kwa makini matumizi ya riwaya za Kiswahili. Utafiti huu uliongezea kwa kuelezea zaidi kuhusu dhana ya uovu. Isitoshe, utafiti umedhihirisha kwamba huwezi kuelewa wema bila kuelewa uovu. Ni pale unapoelewa uovu ndipo utajaribu kuwa mwadilifu, na kumakinika kuhusu swala hilo. Imebainisha kwamba kazi ya sanaa ni njia bora zaidi ya kuelimisha jamii kuhusu suala la uovu na mikakati ya kupambana nao. Fauka ya hayo, utafiti huu umeweka wazi uovu unavyodhihirika katika jamii ili kuitahadharisha jamii mbali na kuwapa moyo waandishi wa riwaya hizi waendelee kuziandika. Hivyo basi, riwaya hizi teule zimedhihirika kuwa gurudumu la kuburudisha, kutahadharisha jamii na hivyo kuongezea dhima ya fasihi andishi kwa jumla hapa barani Afrika.

**Mapendekezo ya Utafiti zaidi**

Utafiti huu ulichunguza kipengele cha uovu pekee katika riwaya teule za Ben R. Mtobwa. Aidha, ulishughulikia kiini cha uovu, athari zake na mbinu za upelelezi zinazotumika kuwanasa wahalifu katika riwaya hizo.

Hatahivyo, ningependekeza kwamba watafiti wengine washughulikie vipengele vingine ambavyo vinahitaji utafiti kama vile:, maudhui mengine yanayopatikana katika riwaya za Ben R. Mtobwa, wahusika na usawiri wa wanawake katika riwaya za Ben R. Mtobwa. Mbali na hayo, wanaweza pia kutafiti mtindo na lugha katika riwaya za Ben R. Mtobwa.

**MAREJELEO**


Anderson, C.A and Carnagey, N.L (2005). *Violent Evil and The General Aggression model.* Chapter in A. Miller (Ed.) Social psychology of good and Evil. (pp168-192) New York :Guilford publications.

Anja Oed and Christine Matzke (2012). *Life's a thriller: Investigating African crime fiction* (crimebeat.bookslive.co.za) Accesed on 24/4/2014 http://d-nb,info/1018060049

Arnold, H.A.(1974). "*Popular Literature In Tanzania.*" Toleo La Kiswahili: Juzuu 51/1 n 51/2. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Dar es salaam

Ashley, B. (1989). *The Study Of Popular Fiction*. London: Printers Publishers Ltd.

Attack on Garrisa University on 4 April 2015 (www.cnn.com/.../ Africa/Kenya-university (www.bbc,co.uk/.../world-africa-3216908 Accessed on (2pm-27/6/2015)

Auden, H. W. (1948 rev 1962). *The Guilty Vicarage. Notes on The Detective Story, by an Addict* New York ; Random House

Augustin (1955). '*Essays in philosophical theology'* Reff.in Enccyclopedia of philosophy vol.3:138 www.str.org/articles

Awdhesh, S. (2014) *Good And Evil.* Allahabad: Aatmic Science publication( A Division of Aaatmic Scienc Publication)

Baclay, W. (1972). *Introducing The Bible*. Nashville: Abington

Bandura, A (1977). *Social Learning Theory*. Englewood Cliffs. Nj Prentice-Hall

Bertoncini, E. Z (1989). *Outline of Swahili Literature: Prose Fiction & Drama*. Leiden:E.J.Brill

Cohen,B. S (2011). *Science of Evil*. UK: Penguin Publishers. Columbia University Press.(http://mobile.nytimes.com/2011/06/14/science/14scribds/html?referenc 8r=0)

Cohen, B, S (2012) *Zero Degrees on Empathy: A New Theory of Human Cruelity*.London Allen Lane

Ervin, S. (2003). *The Psychology of Good and Evil*: New York : Cambridge University Press.

Falk, G. and Falk, C. (1990) *Murder an Analysis of its Forms and Conditions and Causes*.North Carolina: Mefarland and Company, Inc.Publishers

Francis, M. (1992). *Contemporary Marxist Literary Criticism*. New York: Longman Group Limited. gadetection.pbworks.com/w/page/7930447/detective fiction . Accesed on 2/6/2013

Gromov and Primorac (2008). Kumbukumbu za Ben R. Mtobwa (http://jcl.sagepub.com/content/44/3/163). Citation accessed 25th april 2014

Gromov, D. M (2008) 'Mahojiano na Ben R. Mtobwa' katika Kiswahili Forum 15: Kongamano la Tisa la Janheinz Jahn: Mainz.Group Limited.

Hant, C (2010). *Young Hitler*. London: Quantet Books Publishing.

Hirsch, D.E Jr. (1960). *Objective Interpretation* , Source PMLA.Vol 75 No.4 Modern

Language Association. http:www.jstor.org/Stable/460609. Accessed 26/6/2016

Haycraft, H. (1992) *The Art of Mystery Story*: *Acollection of Critical essays*. Carrol & Graf Publishers.

Haycraft, H. (1946) *The Art of Mystery Story*. New York: Gosset & Dunlop.

Hirsch, D. E (1967). *Validity in Interpretation*. London: Yale University.

Hough, G. (1966). *An Essay On Criticism*. Britain: Redwood Press Limited.

http://gutenberg.net.au or www.Feedbooks.com. Accesed July 11 2013

http://jcl.sagepub.com/content/44/3/163. Accesed on July 11 2013

http://jcl.sagepub.com/content/44/3/163.citation accessed 25th April 2014

http://www.Sagepublications.com accesed July 11 2013

http:harpers.org/print/.accessed on May 20 2013

Idi Amin-Facts & History www.history.com/topic/idi amin.( Accessed 20 October 2015)

Jamaadar, A. (1978) *Muwi Huwa Mwema* Nairobi.Longman publishers.

Jenkins, P. (1994). *The Social Construction of Serial Homicide*. New Brunswick: Transaction Publishers.

Kalas, J. E. (2009). *Detective Stories From The Bible*. Nashville: Abingdon Press .

Kamau, M. (1992). *Ufundi Katika Riwaya Za Mohamed Said Abdulla*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Keesey, D.  (1997). *Context For Criticism.*New York City:Mcgraw-Hill

Kersaw, I.(1999). *Hitler 1889-1936*. New York: W.W.Norton &company

Kettle, A. (1960*). An Introduction To The English Novel (*voli) Henry James to present London: Harper & Row

Kezilahabi, .E. (1975*).* "*Riwaya za Upelelezi Katika Fasihi ya Kiswahili*" katika Kiswahili Toleo 45/21. Dar es Salaam: TUKI

Kibet, P. R. (2005). 'Uchanganuzi wa Namna Burhani anavyotatua Matatizo Yanayokabili Jamii katika Riwaya Zake.' Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Egerton (Haijachapishwa).

Kimani, C. (2003)*. "Swala La Dhuluma Dhidi ya Wanawake Katika Fasihi ya Kiswahili."* Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Knoll, J. L. (January 01, 2008). The recurrence of an illusion: the concept of "evil" in forensic psychiatry. *The Journal of the American Academy of Psychiatry and the Law, 36*, 1, 105-16

Lara, M.P (2007). *Narrating evil Postmetaphysical Theory of Reflective Judgement*. NewYork: Columbia University Press.

Larkin , M. (1977). *Man And Society In The Nineteenth Century Realism*. London: Mackmilllan.

Lewis, C. S. (1978*). The abolition of man*. 1943. *New York: Collins*.

Leroy, L. P. (1979). *Novels in Britain WateusShepherd*: *The Detective*. Britain: Bowling.Green University Popular press

Vaughn, L. (2008). *Doing Ethics Moral Reasoning and Contemporary issues.* NewYork: W.W Norton & Company.

Lukacs, G. (1972). *Studies In European Realism*: *A Sociological Survey Of Writings Of Balzac, Stendhal, Zola, Tolstoy Gorki &Others*. London: Marlin Press.

Lukacs, G. (1963). *The Meaning of Contemporary realism*. London: Merlin Press. Macmillan Press.

Mcleod, S. A (2016). *Bandura Social Learning Theory*. Retreaved from-www simplypsychology org/bandura.html Acced on 27/7/201

Madumulla, J.S (2009). *Riwaya za Kiswahil.* Dar es Salaam: Mture Educational publishers Ltd.

Madumulla, J. S. (1988). '*Riwaya za Kiswahili (Tanzania) katika miaka ya Themanini* 'katika MULIKA, Nambari 20. Dar es salaam: TUKI.

Malmgren D, C (2001). *Anatomy of Murder: Detective and crime Fiction.* Popular Press (www.powells.com.)

Mandera bus attacks Daily Nation (www.nation.co.ke...attack …/-/index.html www.ifrc.org Saving lives,changing minds. Accessed20 October.

Mazrui, A.M na B .K.Syambo (1992). *Uchambuzi wa Fasihi* .Nairobi: East African Educational Publishers.

Mgeni, A. (1983*). "The Elements of Mystery in the novels of Mohamed Said Abdalla".* Jarida la Kiswahili Toleo la 50/2. Dar es Salaam: TUKI.

Miller, G. A. (2004). *The Social Psychology Of Good and Evil.* New York: The Guilford publications. .

Mlacha, S.A.K. (1991*). Linguistic Study Of the Novel.* Berli Verlag: Screiber Publishers. Model.

Mtobwa R, B (1984). *Salamu Kutoka Kuzimu*. Dar es Salaam: Mkuki Publishers.

Mtobwa, R B (2004). *Mtambo wa Mauti.*Nairobi: Vide –Muwa Publishers.

Mtobwa, R. B (1987). *Tutarudi na Roho Zetu*. Dar es Salaam: Mkuki publisher.

Mtobwa R, B (1997). *Zawadi Ya Ushindi*. Dar es Salaam: Heko Publishers

Muhammed, S.A (1968) *Kisima Cha Giningi*.London. Evans Bros

Muindi, A. (1990). '*Usawiri wa Wanawake Makahaba Katika Vitabu vya Said Ahmed Mohamed.*' Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Murray, A. H (1943). *Analysis of personality of Adolf Hitler*. Washinton *D.C.* Office of strategic services

Mwita, M. (1995). "*Nafasi ya Riwaya Pendwa Katika Fasihi ya Kiswahili*" katika Baragumu, Nambari 1&2. Dar es salaam: TUKI.

Naivasha 'Vampire' (http://www.ktnkenya.ty...m.youtube). Accessed 20/10/2015

Njogu, K na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. (1997*). "Uhakiki Wa Riwaya Za Visiwani Zanzibar.*" Nairobi: University Press.

Njogu, S. K. (1987). *Maudhui Ya Mapinduzi Katika Riwaya Za Visiwani Zanzibar*.Tasnifu ya M. A Chuo kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Ntaragwa, M. (2004). *Uhakiki Wa Kazi Za Kiswahili*. PHD. Augustana College: Rock Island IL 61201.

Oruka H.O (1990). *Ethics*, Nairobi: Nairobi University.

Palmer, F. (1992). *Literature And Moral Understanding.* Oxford: Clarendon Press.

Price-Anisman, M. P. (1982.Vol.i*). Finding The Key: Detective Fiction For Developmental reader*. Yale: New Yale Haven Teachers Institute.

Petit, F.O (1962) *The Problem of Evil*. NewYork: Hawthorn.

Plato, *The Republic*, from Books 2 and 3.trans.B. Jowett, (1888) 3rd edn Oxford: Clarenton Press, Publishers.

Rana, F. (1999). *The type of Evil Personalities* www.hal-pc.org/-canup/evil.html

Reamer, G . F (2005). *Heinous Crime: Cases causes and consequences*. Columbia: Columbia University Press.

Roman, S (1988). *The Theory of Criticism: From Plato To Present*. NewYork: Longman

Rousseau, J. (1994). *Discourse On Origin Of Inequality*. Frankline, P. (Trans), Oxford: Oxford University Press.

Scaggs, J. (2005). *Crime Fiction*. New York. Routledge

Senkoro, F.E.M.K. (1987). *Fasihi wakati wa Ubepari*. Dar es salaam: Press Publicity

Shaaban, R (1968). *Adili na Nduguze.*University of Califonia: Mac Millian Publishers

Shaaban, R (1968) *Utubora Mkulima.* Dar es Salaam. Nelson Publishers

Shengold, L. (1991). *Soul murder*: *The Effects of Childhood Abuse and Deprivation*. New York.

Svendsen,L.F.H. & Pierce, K.A. (2010).*A philosophy of Evil*. Champaign [Ill.: Dalkey Archive Press.

The Journal of Aesthetics and Art Criticism (1953). http://www.jstor.org/stable/426305

Topan, F. M. (1971). *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*. Dar es salaam: Oxford -University Press.

Wellek, R & Warren, A (1973). *Theories of Literature.* England: Peguin Book.

Wamitila K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi Focus Publications.

Wamitilla, K.W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix

Wilson, E. (1944). katika The New Yorker *Why People Read Detective Stories*.(www.ekitabu.com) accessed on 17/5/2013

Winks, R. W. (1980). *Detective fiction: A collection of critical essays*. Englewood Cliffs, N.J: Prentice-Hall.

www.qucosa.de./.../15-11-mtobwa Interview.pdf Accessed on 12/5/201/2013

www.qucosa.de/fileadm/data/qucosa/documents/.../15-02-Gromov pdf accessed on14/8/2013

www.qucosa.de/fileadm/data/qucosa/documents/...3-10-Gromov pdf Accessed on 14/8/2013

www.yale.edu/ynhti/curriculum/units/1982/1/82.01.01.x.html .May 2013.Accesed on 2/6/2013

www.zum.de/whkmla/sp/1213/jeannerd/mdhlog.html Accessed on 12/5/2013York.Columbia

## VIAMBATISHO

### KIAMBATISHO CHA 1: MAHOJIANO KATI YA MTAFITI NA REYSTUTA MTOBWA MTANDAONI (18/04/2015)

1). **Ben R. Mtobwa alilelewa wapi?**

Ben Mtobwa alizaliwa tarehe 28/08/1958 Mkoa wa Kigoma kijiji cha Ujiji katika hosptal ya Mission Baptist Nchini Tanzania. Alikua mtoto wa 2 kuzaliwa katika watoto 7 waliozaliwa na mama yao Rebeka Ibrahimu.Alililewa Kigoma Ujiji na baadae walihamia Kigoma vijijini Mgambo, Kijiji cha Muhingu,

**2). Ben R. Mtobwa alisoma wapi?**

hapo ndipo alipoanzia darasa la kwanza mpaka darasa la 4 na baadae akahamia shule ya Karuta akaendelea na darasa la 5 mpaka la 7. Sekondari alisoma Dodoma kijiji cha Kondoa Nchini Tanzania kidato cha kwanza mpaka cha 4 na chuo alisomea Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam Tanzania.

**3) Alifanya nini kabla ya kuwa mwandishi**

Kabla ya kuanzisha kampuni yake binafsi, alifanya kazi Mkoa wa Arusha nchini Tanzania katika kiwanda cha nguo cha Tanfrag Tanzania LTD. Na baadae alipandishwa cheo na kua Muangalizi mkuu hapohapo Tanfrag.

Baada ya hapo aliacha Tanfrag na kushirikiana na rafiki yake anaeitwa Mdoe na kuanzisha gazeti la Mwana habari. Baadae alishirikiana tena na rafiki yake mwengine anaeitwa Kajubi Mukajanga wakaanzisha gazeti lilioitwa Wakati ni Huu.

Baada ya hapo ndipo akafungua kampuni yake binafsi iliyoitwa Heko Publishers LTD. Kampuni hiyo ilihusika na Uchapishaji wa Magazeti ambayo ilikua ni gazeti la Heko pamoja na Kalulu, na baadae Kalulu ikabadilishwa na kuitwa jina la Kabumbu, pia kampuni hiyo ilihusika na utoaji wa mikanda ya filamu ambayo ilitoa filamu kama Lazima Ufe Joram, Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe pamoja na Oloiboni na Layoni na ilihusika na uchapishaji wa vitabu vya riwaya ambavyo ameviandika ye mwenyewe kama Mikononi mwa Nunda, Lazima Ufe Joram, Tutarudi na Roho Zetu, Salamu Toka Kuzimu, Mtambo wa Mauti, Malaika wa Shetani, Roho ya Paka, Mikataba ya Kishetani, Zawadi ya Ushindi n.k na vitabu vya watoto alivyoandika ni kama Nani kama Mimi, Kipofu mwenye miwani Myeusi, Mpishi mwenye Kibiongo, Mwalimu mwenye Mkono wa Bandia, Maskini Mashaka, Kimbia Hellena Kimbia, Cheka Kidogo Helena, VIpaji vya Helena n.k. Na vitabu vya shule alivyoandika kwa shule za msingi ni kama Kusoma na kuandika, mwandiko n.k.

4) **Ben Mtobwa alibarikiwa na watoto wangapi?**

Alikua na watoto 7, wakiume 3 na wakike 4.

**5) Unaweza kutuelezea sifa zozote za Ben R. Mtobwa mbali na tajriba yake kazini**?

Ben Mtobwa kipindi cha kuanzia utoto wake na makuzi yake kiujumla hakua mtu wa kuongea sana mara nyingi alipenda kutumia karamu yake kuongea kuliko maneno aidha ilikua ukisoma atakachokiandika ni tofauti na yeye utakavyomuona kiasi kwamba wengi walikua hawaamini kama kweli ni yeye ndo anaandika vitabu hivyo.

Alikua ni mtu mwenye marafiki wengi lakini marafiki wengi walikua wanashindwa kumuelewa kwa sababu ilikua kila wanapokua pamoja yeye alipenda zaidi kuongelea maswala ya vitabuni kuliko stori za kawaida na maranyingi ilikua kila unapokutana nae lazima utamkuta na kitabu chochote mkononi hata ikiwa ni muda wa chakula kipindi yupo shuleni alikua anaenda na kitabu mkononi.

katika historia muhimu aliyoifanya utotoni akiwa na umri wa miaka 13 aliweza kumuokoa kijana mmoja waliekua wanaogelea nae katika ziwa la Lake Tanganyika Mkoani Kigoma, kijana huyo alikua amezama kwenye maji hivyo alifanya jitihada mpaka akafanikiwa kumuokoa.

Zaidi ya yote pia likua ni mtu asiependa uonevu ama kuona mtu ananyanyasika, alikua ni mtu mwenye roho ya kupenda kutoa kuliko kupokea, mimi binafsi ni baba yangu na niliyashuhudia mengi katika hilo kwa sababu nilikua nae karibu muda mwingi na aliwahi kuniambia pia hata mimi niwe hivyo.

Pia kuhusu uandishi wake kwa ufupi alianza kuandika tangu akiwa kidato cha 3 alipokua shule ambapo kitabu chake cha kwanza kuandika kiliitwa Nitakusubiri na cha pili ni Zawadi ya Ushindi ambapo baadae kilikuja kutumika mashuleni kidato cha 3 na cha 4.

Ninafikiri nimekupa maelezo marefu kidogo pengine tofauti na ulivyohitaji, basi unaweza ukasoma ukachukua yale utakayoyahitaji na ambayo huyahitaji basi utayaacha tu, nimejaribu kukupa historia yake kiufupi na pia kama una maswali mengine yoyote basi unaweza ukaniuliza tu nitakujibu.

kila la kheri

**KIAMBATISHO CHA 2: MAHOJIANO MTANDAONI KATI YA MTAFITI NA PROFESA MLINZI MULOKOZI (11/06/2014)**

**Ben R. Mtobwa alizaliwa lini?**

Nashukuru kwa ujumbe wako Bi. Pamela,

Mtobwa Alizaliwa Kigoma Tanzania, na alifariki mwaka 2008. Alikufa akiwa na umri wa miaka 50.

**Unaweza kutuelezea kazi yake tajriba na Mielekeo ya watu wengine kumhusu?**

Aliandika zaidi ya riwaya 10 za fasihi pendwa. Ben Mtobwa alikuwa na kampuni iliyoitwa Heko Publishers. Ukiwasiliana na Heko Publishers wanaweza kukupatia. Kuna maelezo machache katika mtandao. Sina taarifa nyingi za kumhusu, na ninanakili hapo chini yale nilikusanya mtandaoni. Rafiki na waandishi wenzake walimuenzi kiasi cha kumuandalia makumbusho mwaka mmoja baada ya kifo chake.walisema yafuatayo:

Ben Mtobwa, who published several exciting works in Swahili popular literature, died exactly one year ago (9 November, 2008) at the age of fifty. Mtobwa was a Tanzanian, and like the late Cyprian Ekwensi, he was fascinated with the allure of the city (mainly Dar es Salaam)

Ben Mtobwa was quite popular among readers in east Africa (where Swahili is a lingua franca) To put it in continental context, Mtobwa was a writer who appealed to many readers at grassroots level: like David Maillu (of Kenya), the late D.O Fagunwa (and later Kalu Okpi) in Nigeria; Osare Konadu initially, and now Ike Tandor (both of Ghana); and perhaps Gomolemo Mokae of South Africa.

By writing in Swahili, Mtobwa commanded a vast readership in his native Tanzania and in east Africa in general. Quite a number of his works have been translated into English, which further enhanced the popularity of this author.

Ben Mtobwa was bitten by the writing bug since he was a youngster and was already writing extensively whilst in school. His shorter fiction was published in many publications locally, which served as a spur for him to continue to write, experiment with forms, and later become socially conscious through literature. He also wrote non-fiction, and children's books. His many books ranged from Lazima ufe Joram (1983) to Mtambo wa Mauti (2004)


Mtobwa, as a key Director of Heko Publishers in Tanzania used this opportunity to develop and encourage other writers, publish a newspaper and promote pertinent documentaries. His death shocked his many readers and the literary world in general, but his works (books) remain a monument to his memory.

Remembering Ben Mtobwa at the weekend, Ladybrand literary activist George Rampai said: "Ben Mtobwa was a remarkable, prolific writer; no doubt a born writer. He died young, but the likes of Emily Bronte and D.H Lawrence died even much younger. I think of a popular black African writer like the late Ben R. Mtobwa, and my mind e.g goes to Leseli Mokhele of Lesotho, who also writes exciting fiction, is an expert with the short story, publishes a popular newspaper, and has had works broadcast on air…Africa must encourage her exciting writers and keep their legacy alive…hence we celebrate Ben Mtobwa's great legacy"

**KIAMBATISHO 3: MUUAJI WA KIKATILI, ONYANCHA AKIONYESHA ALIKOZIKA WAHASIRIWA**



**KIAMBATISHO 4: KIONGOZI WA KIIMLA WA UGANDA**



**KIAMBATISHO 5: KIONGOZI WA KIIMLA WA UJERUMANI, ADOLF HITLER**

